

**Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Nne - Tarehe 7 Novemba, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Kituo cha Uwekezaji Raslimali Nchini kwa Mwaka 1998 - 2001 (*The Annual Report and Accounts of Tanzania Investment Center for the year 1998 - 2001*)

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 45

**Vifaa vya Matibabu na Jengo la *Physiotherapy* Hospitali ya Mkoa wa Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa jengo la *Physiotherapy* katika Hospitali ya Mkoa wa Singida limezekwa kwa vigae; na kwa kuwa jengo hilo sasa linavuja sana wakati wa mvua kutokana na uchakavu na pia halina umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliezeka upya jengo hilo na kulipatia huduma ya umeme?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga choo kwenye jengo hilo ili kuondoa kero na adha wanayopata wagonjwa wanaofika katika Kitengo hicho kwa matibabu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa vya matibabu kama vile *Infrared Machine, Short Wave Diathermy Machine* na *Ultra Sound Machine* kwenye hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jengo la *Physiotherapy* lililoko katika Hospitali ya Mkoa wa Singida lilijengwa na mfadhili toka Norway anayeitwa *Norad Bente Nilsen* mwaka 1993 kupitia kampuni ya Kikundi cha Umoja wa Vijana. Kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo tabia ya watu kurusharusha mawe katika paa la jengo hilo ambalo limezekwa kwa vigae, ilisababisha baadhi ya sehemu za paa la jengo hilo kuvuja.

Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Mkoa umefanya juhudi ya kukarabati jengo hilo na tunaamini jengo hili hivi sasa halitavuja tena. Aidha, Mkoa tayari umefanya makisio ya kufunga umeme katika jengo hilo lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti, makadirio hayo yatawekwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati michoro ya jengo la *Physiotherapy* ilipokuwa ikitayarishwa, michoro ya choo haikujumuishwa na hivyo kusababisha choo kutojengwa katika jengo hilo. Kutokana na hali hiyo, Mkoa umetayarisha makisio ya ujenzi wa choo na yatawekwa katika mwaka wa fedha 2004/2005.

(c) Mheshimiwa Spika, jengo la *Physiotherapy* linahitaji vifaa vingi vikiwa ni pamoja na vifaa alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Hospitali hiyo ya Mkoa imeweza kupata baadhi ya vifaa hivyo kutoka Shirika la *Dantan, Denmark* vikiwemo *wheel chairs* kumi, *walking frame* moja, *walker on wheels* 26, *arm chairs* 25, *bathing chairs* mbili na *rehabilitating apparatus* moja.

Aidha, Hospitali hiyo pia inavyo tayari vifaa kama vile *short wave diathermy* na *Ultra Sound Machine*. Mashine ya *Infrared* haikupatikana na Mkoa umepanga kuiweka kwenye makisio ya mwaka wa fedha 2004/2005.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa mtaalam huyu amefanya kazi kwa miaka mingi bila kuwa na vifaa akitumia nguvu zake na kwa kuwa ana miaka mingi kazini zaidi ya miaka kumi je, Serikali haioni kwamba wana haki ya kumzawadia hata kwa kumpandisha cheo?

(b) Kwa kuwa mtaalam huyu naye ni binadamu kama sisi anaweza kuugua, kusafiri ama akapata dharura yoyote, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuongeza

mtaalam mwingine katika Hospitali hiyo kuliko ilivyo sasa ambapo yuko peke yake na ukizingatia sasa hivi ongezeko la wagonjwa wenye matatizo ya viungo ni wengi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mtaalam huyo amefanyakazi pale kwa muda mrefu karibu miaka 10 lakini nachelea tu kusema kwamba hiyo peke yake haiwezi kuwa ndio kigezo cha kumpandisha cheo. Vyeo vina utaratibu wake na kwa hiyo lazima taratibu hizo zizingatiwe. Lakini nilitaka vile vile nimkumbushe kwamba masuala ya vyeo sio zawadi lakini ni vitu vya msingi kabisa ambapo kama anastahili anapewa kwa misingi ya taratibu na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtaalam mwingine, tunakubaliana naye na tayari tulishaanza kulifanyia kazi kujaribu kuona kama Wizara ya Afya inaweza kutusaidia kupata mtaalam wa pili ili kupunguza mzigo ambao hivi sasa ameubeba.

**MHE. HAMISI JUMANNE NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa pamoja na upungufu wa watumishi wengine katika Hospitali hiyo mara nyingi Serikali imekuwa ikiahidi kuongeza watumishi hasa Madaktari katika Hospitali ya Singida na mara nyingi tumeahidiwa kupata Madaktari kutoka nchi ya Cuba, je, ni lini Madaktari hao wataletwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumewahi kueleza, swala hili la wataalam katika vituo vyetu mbalimbali vya afya na Hospitali za Wilaya na Mikoa ni tatizo kubwa sana, ninachoweza kusema ni kwamba kwa sababu tumemsikiliza na yeye basi tutajitahidi kuona ni namna gani tunaweza kumsaidia.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kusema kwamba Wizara ya Afya tayari imeshawekeana mkataba na Madaktari kutoka Cuba ambao watapatikana hivi karibuni. Idadi ya Madaktari hao ni 63 na tunategemea Mkoa wa Singida utapata katika mgao huo. *(Makofi)*

Na. 46

### **Ujenzi wa Vituo vya Afya - Tarafa ya Mondo na Farkwa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa ya Mondo na Farkwa katika Jimbo la Kondoza Kusini hazina Vituo vya Afya; na kwa kuwa Vituo vya Afya vilivyopo kwenye Tarafa za Kwamtoro na Goima vipo mbali sana na wananchi wa Tarafa hizo mbili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya katika Tarafa hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoza Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Afya, ili kituo cha Afya kiweze kujengwa, ni sharti kuwa na idadi ya watu wasiopungua 50,000 katika eneo linalohusika. Serikali kwa kigezo hicho inaona kuwa Tarafa ya Mondo yenye wakazi 56,771 na Tarafa ya Goima yenye wakazi wapatao 69,233 zinastahili kila moja kuwa na kituo chake cha afya.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wakazi wa Tarafa ya Mondo wanapata huduma kutoka katika kituo cha Hamai ambacho kipo katika Tarafa ya Goima. Kituo hiki kinahudumia wakazi wa Tarafa mbili za Mondo na Goima wapatao 126,004. Huu ni mzigo mkubwa hata kwa Mganga anayehudumia wakazi hao.

Kwa hiyo, tunaomba tu tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge suala hili liweze tena kuwasilishwa katika Halmashauri yake ili waweze kupata michoro inayostahili kutoka kwa Mganga wa Wilaya, michoro hiyo ndio itakayotuwezesha kujua ukubwa wa gharama za kujenga kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niseme kwamba jukumu la kujenga kituo hicho ni la Halmashauri yenyewe lakini tunachoweza kusema tu ni kwamba kama wataharakisha jambo hili linaweza kabisa kuingizwa katika bajeti ya 2004/2005.

Vile vile tunaomba wananchi washirikishwe kwa kiasi kitachowezekana kuweza kutumia nguvu zao na tunaiomba Halmashauri itafute wahisani kutoka sehemu mbalimbali. Kwa upande wa Serikali, jambo hili litakapokuwa limewasilishwa kwa utaratibu wa kawaida na sisi tutajitahidi kuliwekea msisitizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha afya kujengwa katika Tarafa ya Farkwa yenye wakazi 28,299, Shirika lisilo la Kiserikali la *World Vision* kwa kushirikiana na wananchi wameanza ujenzi wa kituo cha afya katika kijiji cha Makorongo tangu mwezi Oktoba, 2002. Serikali iliridhia ujenzi huu kwa sababu ya hali ya kijiografia na umbali wa eneo hilo kutoka katika kituo cha Afya cha Kwamtoro kilichopo kilomita 40 katika Tarafa ya Kwamtoro.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya katika Tarafa ya Farkwa yanachukua muda mrefu na kwa kuwa baadhi ya majengo haya ambayo yameanzwa kujengwa na Shirika la *World Vision* hasa la tiba limekwishakamilika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawasaidia vipi wananchi wa Tarafa ya Farkwa wapatiwe huduma kabla majengo haya hayajakamilika ili waweze kuhamasika kuendelea kujenga majengo hayo wakati wanapata huduma ya afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunaomba tumpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyojitahidi kusukuma suala hili ambalo ni la msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu nimtake radhi kwamba inawezekana rai yake ikapingana na juhudi nyingine za Serikali. Wakishaanza kutumia kituo hicho kutakuwa na mwingiliano mkubwa na inawezekana kabisa katika hali ya kawaida ya kutoa huduma za afya isiwe jambo jema.

Kwa hiyo, nadhani tushirikiane tu tujaribu kusukuma ujenzi huo ukamilike ndani ya muda ambao tunafikiri unahitajika ili wananchi waweze kupata huduma hiyo kikamilifu bila kubughudhiwa tena na ujenzi utakaokuwa unaendelea.

Na. 47

### **Kiwanda cha Kutengeneza Dawa**

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Tanzania ina ubia na Serikali ya China ya Kiwanda cha Kutengenezea Dawa za Binadamu ambacho kipo chini ya Jeshi la Kujenga Taifa:-

(a) Je, dawa hizo zinachangia kwa kiasi gani katika mapato ndani ya Serikali yetu?

(b) Je, kiwanda hicho kimeshafikia kiwango gani cha kusafirisha dawa katika soko la nje?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali Na. 47 la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Kiwanda cha *TANZANSINO* kilianzishwa Desemba, 2000 kwa dhamana ya dola za Kimarekani milioni 2.15. Kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 19 Machi, 2001. Kiwanda kinamilikiwa kwa pamoja kati ya *SUMAJKT* (Tanzania) na *Shanxi Provincial Technical Renovation and Equipment Corporation* toka Jimbo la Yabai, China.

*TANZANSINO* ina jumla ya wafanyakazi 73 kati yao 46 ni Wanajeshi, 17 ni raia wa Tanzania na 10 ni Wachina.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kiwanda kinatengeneza dawa aina nane za vidonge ikilinganishwa na mwaka 2001 kilipokuwa kinatengeneza dawa aina mbili tu za vidonge. Dawa nyingine ya kutibu malaria iitwayo *Artecom* itaanza kutengenezwa. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2003/2004, kiwango cha uzalishaji kiwandani hapo kimeongezeka toka vidonge 400,000 mwaka 2001/2002 hadi 1,400,000 mwaka 2002/2003 kwa siku na mauzo ya kiwanda yamefikia shilingi 488,309,287.75 kwa mwaka badala ya shilingi 175 milioni kwa mwaka, kwa kipindi cha 2001/2002. Kiwanda cha *TANZANSINO* kimepeta tuzo ya Kimataifa inayoitwa *The 17th International Quality Summit Award for Excellency and Business Prestige in Gold Category* ambayo ilitolewa Mjini New York, Marekani tarehe 14 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *TANZANSINO* kina mpango wa kuboresha na kuongeza uzalishaji wa dawa nyingi aina mbalimbali. Mpango huu unakisiwa kugharimu Dola za Kimarekani 651,776 ambazo ni nyongeza ya Dola 2.15 milioni zilizotolewa na mbia kwa ajili ya kununua na kufunga mitambo ya kisasa, kukarabati majengo na kuanza majaribio ya awali ya uzalishaji dawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

(a) Kiwanda cha *TANZANSINO* kimechangia pato la Serikali kwa kulipa Kodi ya Mauzo, Ushuru wa Kuingiza Bidhaa na Ushuru wa Stempu zenye jumla ya shilingi 66,703,063. Vile vile hulipa kodi nyingine za Halmashauri ya Jiji. *TANZANSINO* hailipi kodi ya *VAT* na Kodi ya Mapato kutokana na sheria ya nchi inayotoa msamaha kwa baadhi ya kodi kwa wawekezaji. Msamaha huo wa miaka mitano unatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2004.

(b) Kiwanda kinaendelea na mpango wa kuboresha na kuongeza uzalishaji wa dawa za aina mbalimbali kwa wingi zikiwemo dawa za kutibu *Malaria*. Mpango huu utakapokamilika utagharimu Dola za Kimarekani 651,776. Baada ya kukamilika kwa mpango huu, Kiwanda cha *TANZANSINO* kitakuwa na uwezo wa kuzalisha dawa za aina mbalimbali kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa kiwanda hiki kina sifa za Kimataifa je, kina mpango gani wa kutengeneza dawa za kuwasaidia waathirika wa ugonjwa wa Ukimwi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze sana kwa kuuliza swali hilo. Ni jambo muhimu sana kwamba kiwanda hiki kipewe jukumu la kupambana na janga hili la Ukimwi ndio maana

tumeingia ubia na ndugu zetu Wachina ambao wako mstari wa mbele kuhusu tiba ya tatizo hili la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba mpango wa kuboresha na kupanua kiwanda unaendelea utakapokamilika suala hili la kuzalisha dawa za kurefusha maisha ya walioathirika na Ukimwi litazingatiwa.

Na. 48

### **Uboreshaji wa Huduma ya Maji - Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Mpwapwa na Vitongoji vyake vya Vinghawe, Hazina, Majengo, Igovu, Bahelo, Manghangu, Mji Mpya na Ng'ambo unakabiliwa na matatizo makubwa ya huduma ya maji; na kwa kuwa hivi sasa mji huo una wakazi zaidi ya 50,000 lakini vyanzo vya huduma hiyo bado ni vile vile vya zamani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mpwapwa na vitongoji vyake vyote nilivyovitaja?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja ya kufanya utafiti wa vyanzo vingine vya maji badala ya kutegemea vyanzo vilivyopo sasa ambavyo havitoshelezi mahitaji ya huduma hiyo katika mji wa Mpwapwa na vitongoji vyake kutokana na ongezeko kubwa la watu na taasisi zilizopo katika mji huo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba mji huo, pamoja na kuwa na wakazi zaidi ya 50,000 lakini pia kuna Taasisi za Serikali kama Shule ya Sekondari ya Mpwapwa, Chuo cha Maafisa wa Afya, Chuo cha Ualimu, Chuo cha Mifugo (*LITI*), Hospitali ya Wilaya, Magereza, Kituo cha Polisi na Kituo cha Utafiti na Maendeleo ya Mifugo na Mafunzo Kanda ya Kati na kwamba iko haja ya kuboreshwa kwa huduma ya maji ili kusaidia kupunguza kero hiyo kwa wakazi wa Mji wa Mpwapwa na taasisi zake?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa George Lubeleje, kuwa mji wa Mpwapwa na Vitongoji vyake unakabiliwa na uhaba wa maji. Katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji mjini Mpwapwa mwaka jana, Serikali iliimarisha huduma hiyo kwenye Kitongoji cha Mazae kwa kujenga mradi unaotumia maji ya mtiririko kutoka kwenye chemichemi ya Kwamdianga yenye uwezo wa kuzalisha meta za ujazo 225 za maji kwa siku. Mradi huo ulitekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa gharama ya shilingi milioni 100 na huduma imeongezeka kutoka asilimia 28 mpaka 31. Mradi huu umekamilika mwezi Septemba, 2003.

Kadhhalika katika mpango wake wa muda mrefu, Serikali ya Tanzania iliingia makubaliano na Serikali ya Ufaransa mwezi Julai, 2003, kuhusu kuboresha huduma ya maji katika baadhi ya miji midogo humu nchini. Mradi huu utanza kwenye miji midogo tisa ya Utete, Ikwiriri, Kibiti, Turiani, Mvomero, Kilosa, Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa. Mradi huu utanza kwa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu vyanzo vya maji pamoja na kutayarisha makisio ya gharama za ujenzi wa miundo mbinu kwenye miji hiyo. Hivi sasa Wizara yangu iko kwenye hatua ya kumtafuta Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi hiyo ya uchunguzi na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi hiyo kukamilika, utekelezaji wa mradi utanza kulingana na fedha zitakazotengwa na Serikali ya Ufaransa. Kama nilivyosema hapo awali, mji wa Mpwapwa, vitongoji vyake na taasisi zilizopo vitanufaika na mradi huu. Utekelezaji utanza mara baada ya uchunguzi huo kufanyika.

Aidha, Wilaya ya Mpwapwa ni moja kati ya Wilaya 12 zilizopo kwenye mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira unaotekelezwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Kwa kupitia mradi huu, Halmashauri ya Wilaya itaweza kupata fedha za kupanua mradi wa maji Mjini Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ipo haja ya kuboresha huduma ya maji kwenye mji wa Mpwapwa sambamba na upanuzi wake. Ili kutekeleza hilo, mji wa Mpwapwa ni mmoja kati ya miji ya Wilaya ambayo imeanzisha Bodi ya Majisafi na Majitaka mwaka 2003. Wizara ilikwishatoa madaraka kwa bodi hii kusimamia shughuli za mamlaka hiyo kwa nia ya kuboresha hali ya huduma ya maji Mjini Mpwapwa. Wizara kwa kushirikiana na Bodi hiyo itaendelea kusaidia Mamlaka ya Maji Mjini Mpwapwa kuongeza ufanisi wa utendaji kazi zake pamoja na kusaidia upanuzi wa miundo mbinu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kwanza napenda niishukuru sana Serikali pamoja na Benki ya Dunia kwa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mpwapwa. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuitembelea Wilaya ya Mpwapwa na hasa kuona vyanzo vya Mayawile kufuatana na majibu yake ili kuwapa wananchi matumaini kwamba haya aliyosema kweli yatatekelezwa?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa George Lubeleje, kwa jinsi anavyofuatilia suala la maji katika Wilaya yake. Napenda kumhakikishia kwamba nikipata nafasi nitatembelea Mpwapwa. *(Makofi)*

Na. 49

### **Mashine ya Kusukuma Maji Mbawala Chini**

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME** aliuliza:-



Kwa kuwa Serikali katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 imepania kuondoa kero ya maji kwa wananchi wake waishio vijijini na mijini; na kwa kuwa kutokana na kuharibika kwa mashine ya maji iliyopo Mbawala Chini eneo la Mtwara Mjini kumesababisha matatizo makubwa ya huduma hiyo katika Vijiji vya Mbawala Chini, Naliendele, Mbawala Juu, Litumbu na Nyengedi:-

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu mkubwa wa kufufua mradi huo ili kuondoa tatizo la maji linalowakabili wananchi wa vijiji nilivyovitaja?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Mbawala Chini ulijengwa kwa msaada wa Serikali ya Finland mwaka 1981 na kukabidhiwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ili wauendeshe na mradi huu ukaendelea kutoa huduma ya maji hadi mwaka 1991. Mradi huu ulishindwa kutoa huduma ya maji kutokana na kuharibika kwa visima vyake vyote viwili ambavyo vilijaa mchanga na hivyo kusababisha pampu zote mbili kukwama ndani ya visima. Juhudi za kuzikwamua pampu hizo kutoka ardhini zimeshindikana kabisa. Ili kurejesha huduma hii, mradi wa maji Mbawala Chini unahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa unaokadiriwa kugharimu shilingi 80,302,000/=.

Vijiji vya Naliendele, Mbawala Chini, Mbawala Juu, Litumbu na Nyangedi vinapakana na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Naliendele kinachosimamiwa na Wizara ya Kilimo na Chakula ambacho pia kinategemea huduma ya maji kutoka kwenye mradi huo. Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kutambua tatizo la maji, imekubali kutatua tatizo hili kwa ajili ya kituo chake pamoja na vijiji nilivyovitaja kwa msaada wa fedha kutoka Benki ya Dunia, kiasi cha shilingi 72,271,800 na fedha iliyobaki ya shilingi 8,030,200 zimetengwa kwenye Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2003/2004. Mhandisi wa Maji wa Mkoa wa Mtwara ameanza kutekeleza mradi huu kuanzia tarehe 04 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya ukarabati huo kitakachobaki ni kurekebisha sehemu ya mabomba ya kusambaza maji kwenye maeneo ambayo hayakuhusika na mradi.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya kuweka mradi huu kwenye mipango ya maendeleo ya Wilaya na kuutengea fedha za kukamilisha kazi za ukarabati zilizobakia ambazo zitagharimu kiasi cha shilingi milioni 10 tu.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa vijiji nilivyovitaja vinaathirika sana na ukosefu wa maji na kwa kuwa mategemeo yao makubwa ni mradi huo niliou sema wa Mbawala Chini na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri una ziara inayoanza tarehe 10 Novemba, 2003 kutembelea Mkoa wa Mtwara sasa utakubali kupokea ombi langu kupitia ziara yako hiyo ukautembelea mradi huo wa maji wa Mbawala Chini ili ukajionee wewe mwenyewe?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nakwenda Mtwara kuanzia Jumatatu na nitajitahidi kufika huko Mbawala Chini nikaone kazi inavyoendelea. (*Makofi*)

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuja Mtwara na kutembelea mradi wa Mbawala Chini na kwa kuwa Waziri Mkuu tulimwonyesha miradi ya maji ya Chipwalapwata, Minyembe na Kitele je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufika Chipwalapwata, Minyembe na Kitele? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kama nitaweza kufika vijiji vyote lakini nitajitahidi kadri inavyowezekana nifike katika vijiji vile ambavyo vina matatizo.

Na. 50

#### **Uwekezaji wa Benki Kuu ya Tanzania katika *Afrexim Bank***

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye urari wa Benki Kuu (*Balance Sheet of Bank of Tanzania*) ya kuishia 30 Juni, 2001 imeonyesha kwamba imewekeza shilingi 1,065,636,000 katika Benki ijulikanayo kama *Afrexim Bank*:-

(a) Je, Benki hiyo inafanyia shughuli zake wapi hapa Tanzania au kwenye nchi gani?

(b) Je, kama Benki hiyo inafanyia kazi yake hapa Tanzania mbona taarifa zake hazijawahi kuletwa hapa Bungeni na imechangia kiasi gani cha faida?

(c) Je, wajumbe wake wa Bodi ni akina nani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *Afrexim Bank* (Benki ya Afrika ya Biashara ya Nje) ilianzishwa rasmi mwezi wa Oktoba, 1993 huko Abuja nchini Nigeria na nchi wanachama wa nchi za Kiafrika aidha kupitia Wizara za Fedha au Benki Kuu za nchi

zao. Makao Makuu ya *Afrexim Bank* kwa sasa ni Cairo Misri, baada ya kuhamia kutoka Abuja Nigeria tarehe 30 Septemba, 1994. Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki kama mwanachama mwanzilishi wa Benki hii na ilinunua hisa zenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,200,000.00 (milioni moja na laki mbili).

Madhumuni ya *Afrexim Bank* ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukuza na kuendeleza biashara ya nje katika Bara la Afrika na baina ya nchi za Kiafrika.

(ii) Kutoa mchango wa kuunganisha Afrika kiuchumi kupitia biashara za nje na hasa kuondokana na vikwazo vinavyofanywa na vyombo vya fedha vya Kimataifa kwa wakati huo.

(iii) Kutoa na kusaidia upatikanaji wa mikopo nafuu ya muda mfupi na muda wa kati kwa wauzaji bidhaa nje kutoka katika Mabenki na taasisi mbalimbali za fedha katika nchi wanachama.

(iv) Kukuza na kugharamia usafirishaji wa bidhaa na huduma zisizokuwa na asili za Afrika.

(v) Kusaidia utaratibu wa malipo yanayolenga kupanua biashara ya Kimataifa miongoni mwa nchi za Kiafrika.

(vi) Kufanya tafiti za masoko na kusaidia huduma zinazolenga kuongeza biashara na bidhaa zinazosafirishwa miongoni mwa nchi za Afrika na nje ya Bara la Afrika.

(b) Mheshimiwa Spika, taarifa za *Afrexim Bank* haziwasilishwi Bungeni kwani Benki hiyo ni asasi ya Kimataifa ambayo Makao yake Makuu ni Cairo na ina wanahisa wengi ikiwa ni pamoja na nchi za Kiafrika 30, asasi za fedha za nchi za Kiafrika 24 na asasi za fedha za Kimataifa 6.

Gawio la faida kwa Benki Kuu ya Tanzania tangu *Afrexim Bank* ianzishwe ni dola za Kimarekani 153,484.55 ambapo ilikuwa dola za Kimarekani 16,329 mwaka 1997 na kuongezeka mwaka hadi mwaka mpaka kufikia dola 35,974 mwaka 2002. Kabla ya mwaka 1997 hakukuwa na gawio lolote lililotolewa.

(c) Mheshimiwa Spika, wajumbe wa Bodi ya *Afrexim Bank* ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Bwana C.C. Eordu, ni Rais wa *Afrexim Bank* na ni Mwenyekiti, Dr. Kaleb Fundanga kutoka Zambia na ni Mkurugenzi, Bwana M.M. Khalil wa Egypt na ni Mkurugenzi, Dr. S. Usman wa Nigeria na ni Mkurugenzi, Bwana M. H'midouche wa *ADB* na ni Mkurugenzi, Bwana C. Chikaura wa Zimbabwe ni

Mkurugenzi, Bwana M. Daouas wa Tunisia ni Mkurugenzi na Bwana E. Ahotou wa Ivory Coast na ni Mkurugenzi.

*(Hapa umeme ulikatika na kurudi baada ya muda mfupi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, wengine ni Dr. O.H. Saeed wa *BADEA* na ni Mkurugenzi, Bwana F. Kennedy wa UK na ni Mkurugenzi na Bwana Getachew Telahun wa *Afrexim Bank* na ni Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza napenda nifahamu Benki hii imewasaidiaje Watanzania na ni Watanzania au wafanyabiashara wa Tanzania wangapi wamenufaika na benki hii?

Mheshimiwa Spika, la pili, nilitaka kuuliza kwamba kwa kuwa Serikali imejitoa na kuuza benki zake hapa nchini, kuwekeza katika benki za nje ina maana gani badala ya kusaidia kujenga benki zetu za hapa nchini kama *Microfinance Bank*? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba benki hii mbali na gawio ambalo nimelitaja wakati najibu jibu la msingi hatujafaidika sana kwa maana ya kukopeshwa ama kutumia *facilities* mbalimbali za mikopo kutoka benki hiyo. Taarifa zilizopo ni kwamba waliofaidika na mkopo huo ni *Vodacom Tanzania* peke yake, lakini mazungumzo yanaendelea hivi sasa baina ya Benki hii na *NDC* kwa ajili ya kutoa mkopo ambao utafinanse *EPZ*. Ni kweli kwamba bado hatujafaidika na kuna haja kujipanga kama nchi tuweze kutumia benki hii kwa manufaa ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, Benki ilipoanzishwa kulikuwa na matatizo ya kupata fedha ambazo zingeendeleza biashara ya nje ya Afrika. Kwa hiyo, lengo lilikuwa ni kutoa mchango wa kuunganisha Afrika kiuchumi kupitia biashara za nje na hata kuondokana na vikwazo vilivyokuwa vinafanywa wakati huo na vyombo vya fedha vya Kimataifa. Lakini pia inachangia kuunganisha nchi za Kiafrika kiuchumi na kuleta umoja wa nchi za Kiafrika.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo sisi kwetu ni darasa, lakini nilikuwa naomba atusaidie kutupa maelezo, kwa sababu sasa hivi mwelekeo wa biashara kufuatana na hali ya uchumi wa Taifa letu ni kwamba shughuli za kibiashara na kiuchumi zinaendeshwa na watu binafsi, ni dhahiri kabisa kutokana na madhumuni ya hiyo benki hao watu wanaoendesha shughuli za biashara na uchumi wangependa sana kusaidiwa na hii benki.

Je, ni taratibu gani hawa watu wanatakiwa wazifuate ili waweze kupata huduma za benki hiyo katika kutafuta masoko ya bidhaa zao katika nchi za nje? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kuna njia mbili za kufuata; moja ni wafanyabiashara binafsi kutuma maombi kule na kuandika *write-up* ama mchanganuo kwa ajili ya kuombea mkopo moja kwa moja kwenye benki hii huko Cairo, Misri. Lakini njia nyingine ambayo inatumika na wenzetu wa Zambia wameitumia wamefikia makubaliano na benki hii kwa kukopesha Benki ya Maendeleo ya Zambia ambayo ndiyo inatoa mikopo ya muda mfupi na wa kati.

Kwa hiyo, utaratibu pia ulikuwa unaangaliwa kwa ajili ya kutumia benki yetu ya maendeleo ya *TIB* ili tuweze kupata mikopo hasa ya muda wa kati na muda mrefu. Kwa hiyo, wafanyabiashara wenye kuhitaji mikopo hasa ya maendeleo ya muda wa kati na mrefu waweze kuomba moja kwa moja huko lakini pia kama nilivyosema kwenye jibu la nyongeza la Mheshimiwa Derefa, kwamba *NDC* wanafanya mazungumzo sasa hivi ili tuweze kupata mkopo kwa ajili ya ku-*finance EPZ*. (*Makofi*)

Na. 51

### **Mikopo ya Taifa kwa Ujenzi wa Miradi Mikubwa ya Umeme**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imenufaika na msamaha mkubwa wa madeni ya nje na kwamba fedha hizo zingetumika kuboresha huduma za jamii ili kuondoa umaskini:-

(a) Je, mikopo ya Taifa iliyotumika kujenga miradi mikubwa ya umeme kama ile ya Kidatu, Hale (*Pangani falls*) na kadhalika ni miongoni mwa madeni ambayo Tanzania imesamehewa na ni ya kiasi gani?

(b) Kama jibu kwenye sehemu (a) ya swali hili ni ndiyo na iwapo Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) ndilo lililokuwa likilipa deni la mikopo hiyo kwa niaba ya Serikali; je, Serikali inaipatia *TANESCO* punguzo la deni hilo kwa kiasi gani?

(c) Kama upo msamaha wa madeni hayo, je, ni kwa nini unafuu huo sasa usijengewe hoja kwa ajili ya *TANESCO* ili utumike kupunguza viwango vya gharama za umeme (*tariffs*) viwandani na majumbani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania imekuwa ikidaiwa madeni ambayo yalitokana na mikopo kutoka Mashirika mbalimbali ya fedha pamoja na nchi wahisani kwa ajili ya kusaidia miradi mbalimbali ikiwamo miradi inayoendeshwa na *TANESCO*. Miradi inayoendeshwa na *TANESCO* inahusisha ujenzi wa vituo vya kuzalishia umeme pamoja na kusambaza umeme huo kwenda Mijini na Vijijini. Madeni hayo yametokana na mikopo ambayo Serikali ilidhamini Shirika ili liweze kukopa kutoka nje na ile ambayo Serikali imekuwa ikikopa kutoka nje na kisha kuikopesha *TANESCO*.

Aidha, Serikali imekuwa ikikopa moja kwa moja ili kusaidia *TANESCO* pamoja na mashirika mengine ya Serikali na kuna madeni mengine ambayo *TANESCO* ilikuwa ikikopa bila kupitia Serikalini ambapo *TANESCO* inatakiwa kulipa kwa mdai. Hata hivyo baada ya Tanzania kufikia *HIPC Completion Point*, Mashirika hayo ya fedha pamoja na baadhi ya nchi wahisani walikubali kufuta madeni yote au sehemu ya madeni hayo kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa madeni. Fedha ambazo zimekuwa zinaokolewa kutokana na msamaha wa kulipa madeni zimekuwa zikitumika kuboresha uchumi na huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji na barabara chini ya mpango wa kuondoa umaskini na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya mikopo ya Taifa iliyotumika kujenga miradi mikubwa ya umeme kama vile Kidatu, Hale, Pangani na kadhalika ni miongoni mwa madeni ambayo Tanzania imefutiwa na Mashirika ya fedha pamoja na nchi wahisani. Chini ya mpango huo Serikali inategemea kupata msamaha wa madeni ya kiasi cha shilingi 1.9 trilioni kwa thamani ya sasa yaani *Net Present Value* ambayo ni sawa na *USD* 1.2 bilioni katika miaka 20 ijayo. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni, 2003, jumla ya shilingi 2,730.97 bilioni ambazo ni sawa na *USD* 2,6909 milioni zilikwishasamehewa

(b) Mheshimiwa Spika, mzigo wa madeni ambayo *TANESCO* inadaiwa ni sehemu ndogo tu kati ya mambo yanayochangia kupanda kwa gharama za viwango vya umeme. Sehemu kubwa ya gharama hizi za umeme zinatokana na ukubwa wa gharama za uendeshaji pamoja na ufanisi wa shirika hilo. Hata hivyo kwa sasa mwelekeo wa sera hautoi stahili ya unafuu wa madeni kwa mashirika na taasisi zake zinazodaiwa kwa msingi wa msamaha wa madeni unaotolewa kwa Serikali Kuu, kwani hatua hii inaweza kuvuruga juhudi za kuleta ufanisi katika mashirika husika na pia kwenda kinyume na makubaliano na wafadhili juu ya kuboresha mgao katika sekta zenye kipaumbele.

(c) Katika maelewano baina ya Tanzania na wakopeshaji wake chini ya makubaliano na kundi la Paris, misamaha ya madeni inayotolewa kwa nchi husika si shirika moja moja lililokopa. Aidha, misamaha yote ya Tanzania inatakiwa itumike kupambana na umaskini katika Taifa kwa ujumla, si kulinusuru au kulinufaisha shirika lililokopa. Kwa sababu hizo hakuna msingi kwa Tanzania kulitetea shirika lolote, likiwemo *TANESCO* ili lisamehewe kipekee na kunufaika kipekee na misaada iliyofutwa na wakopeshaji wake.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, hesabu za awali za ukaguzi za *TANESCO* zinaonyesha kuwepo kwa baadhi ya madeni ambayo hakuna Mikataba yoyote au kumbukumbu za Mikataba kati yake na Serikali. Je, Serikali inafanya nini ili kurekebisha hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, pili, ili kuwezesha wananchi wa Vijijini kutumia umeme kwa maendeleo yao, je, Serikali itachukua hatua gani za kuitaka *TANESCO* kupunguza gharama za *service line* hasa katika maeneo ya Vijijini na kutenganisha gharama hizo kati ya Mijini na Vijijini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, madeni yote ya *TANESCO* yanaeleweka, yale ambayo *TANESCO* ilikopa moja kwa moja na yale ambayo Serikali ilikopa halafu ikaleta na kuwakopesha *TANESCO* yaani *on lending*.

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba hakuna madeni ambayo hayana Mikataba, madeni yote yana Mikataba na nilisema katika jibu langu la msingi kwamba madeni haya ya *TANESCO* hayawezi kulipwa kipekee kwa upendeleo, vinginevyo mashirika yote yangeomba yapewe kama *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANESCO* ipunguze gharama za *service line* hilo *TANESCO* tutawaomba waliangalie. Lakini swala kubwa tunalozungumza ni kwa *TANESCO* kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi ili uzalishaji uongezeke na gharama zipungue na bei zitapungua kutokana na mzigo wa gharama kubwa kupungua.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mwelekeo wa ukuaji uchumi nchini unaelekea kukua mwaka hadi mwaka na dalili zinaonyesha kwamba *capacity* ya umeme nchini haiwezi kuja kutosheleza kwa siku chache zijazo. Kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kuendeleza miradi kama ya *Stigler's Gorge* ili tuondokane na matatizo mengi ya kuongeza gharama za uzalishaji umeme hapa nchini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali haina kigugumizi katika kuendeleza miradi ya umeme ili kukidhi haja ya ukuaji wa uchumi na hivi sasa tunavyozungumza iko miradi mbalimbali ya umeme ambayo inafanyiwa kazi ikiwemo ya *Mnazi Bay*, Songosongo, Mchuchuma, Luhuji na mingineyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Stigler's Gorge* miradi ya umeme ambayo inaingizwa katika uendelezaji, imepangwa katika orodha na *Stigler's Gorge* ni moja ya mradi ambao hapo baadaye utatiliwa maanani katika uzalishaji wa umeme hapa nchini.

**Soko la Uhakika kwa Zao la Korosho**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo mazao mengi ya biashara yanayolimwa hapa nchini na korosho ikiwa zao mojawapo la biashara:-

(a) Je, ni zao gani la kwanza kati ya mazao ya biashara linaloongoza kwa kulipatia Taifa fedha nyingi za kigeni?

(b) Je, zao la korosho ni la ngapi katika orodha ya mazao yanayoliingizia Taifa mapato makubwa?

(c) Kwa kuwa wakulima wakubwa wa korosho ni wanawake, je, Serikali ina mipango gani ya kuwapatia wanawake hao soko la uhakika na vifaa vya kubangua zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchango wa mazao ya biashara katika kulipatia Taifa fedha za kigeni hubadilika kutokana na kiwango cha uzalishaji na bei inayopatikana katika soko la dunia. Mazao ya kahawa, korosho na tumbaku yamekuwa yakishikilia nafasi za juu katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2001 zao la kahawa liliongoza kwa kuliingizia Taifa jumla ya Dola za Marekani milioni 57.05 likifuatiwa na zao la korosho ambalo liliingiza dola za Marekani milioni 56.58.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 zao la tumbaku liliongoza kwa kuliingizia Taifa dola za Marekani milioni 50.50, likifuatiwa na zao la korosho ambalo liliingizia Taifa dola za Marekani milioni 46.26. Zao la kahawa liliingiza dola za Marekani milioni 35.14.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wakulima wa korosho ambao wengi wao ni wanawake kupata soko la uhakika na pia kuwapatia vifaa vya kubangua korosho, Serikali inafanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuwahasisha wakulima kujiunga katika vikundi vya uzalishaji na ubanguaji wa korosho ili kuweza kuwa na kiasi kikubwa cha korosho zilizobanguuliwa na hivyo



kikidhi mahitaji ya soko. Aidha, kujiunga katika vikundi kutawezesha wanachama kuwa na kauli ya pamoja katika kupatana bei na wanunuzi.

(ii) Kuwapa wakulima mafunzo ya kubangua korosho yaani uchomaji (*roasting/steaming*), ubanguaji (*shelling*), ukaushaji (*drying*), umenyaji (*peeling*), upangaji katika madaraja (*grading*) na ufungaji (*packing*), kwa kuzingatia viwango vya ubora unaotakiwa katika soko.

(iii) Kuwapa wakulima ushauri na mwongozo wa kisheria ili waweze kujiunga pamoja katika Vyama na kupata usajili kwa lengo la kuwawezesha kuendesha biashara zao kwa uwazi zaidi.

(iv) Kuwapatia taarifa za masoko ili kukuza soko la ndani na nje la zao la korosho.

(v) Kudhamini baadhi ya Vyama na vikundi ili viweze kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya biashara na kilimo kama Saba Saba na Nane Nane kwa ajili ya kukuza soko la ndani na nje.

(vi) Kuwahasisha wabanguaji wadogo kuungana ili waunde Vyama vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*) vitakavyowasaidia katika kuongeza mitaji yao na kupata mikopo kwa ajili ya kukuza biashara zao.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa zao la korosho linaingizia pato kubwa Taifa hili na kwa kuwa wakulima Mkoa wa Mtwara kwa vipindi vitatu uzalishaji umeshuka. Je, Serikali itawasaidiaje hao wananchi kupata pembejeo ili waweze kuzalisha kwa uhakika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa msimu huu zao la korosho limekumbwa na ugonjwa wa kupukutika majani na kukosa kuzaa kabisa korosho, je, Serikali inajua tatizo hilo na kama inajua inachukua hatua gani za haraka.? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kushuka kwa uzalishaji wa korosho Mkoani Mtwara kutokana na kukosekana kwa pembejeo, ningependa tu niseme kwamba jitihada za Serikali siku zote zimekuwa ni kuhakikisha tu kwamba wakulima wanaongeza uzalishaji na kwa hiyo suala la kupatiwa pembejeo ni jitihada ambazo zinafanywa na Serikali kwa ujumla na hata ukizingatia katika huduma zote za bajeti zilizopita katika kipindi hiki suala hili limezingatiwa kwa ukamilifu na kwa hiyo tuna uhakika kabisa kwamba suala hili Serikali inalishughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, juu ya ugonjwa wa korosho ambao umekumba wakulima wa Mkoa wa Mtwara halikadhalika ningependa kujibu kwamba Serikali inazo taaarifa hizi

na wakati itakapowezekana itaendelea kuyafuatilia matatizo haya ili kuwaondolea wakulima wa korosho tatizo la ugonjwa huu.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mazao ya biashara kama pamba, korosho, kahawa, alizeti yanahusisha wananchi wengi katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Je, Wizara ina mikakati gani na dira ipi yenye kutia matumaini kuyafanya mazao haya kama mojawapo ya vitovu vikuu vya kuleta magaeuzi ya haraka ya kiuchumi na kijamii na kusaidia kuondoa umaskini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza na jinsi ambavyo yeye mwenyewe akiwa mmoja wa viongozi wa Bodi ya Pamba ambalo ni moja ya zao kuu linalopandisha uchumi hapa nchini jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba mazao haya yanazidi kuongezeka kwa ubora pamoja na wingi ili kuwezesha kukuza uchumi wa Taifa.

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tukishirikiana wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge na hususan mwuliza swali ambaye yeye ni Mwenyekiti wetu wa Bodi ya Pamba, nadhani tunaweza kuongeza ubora wa mazao yetu yakaweza kuinua uchumi wa nchi yetu.

Na. 53

### **Vyama vya Ushirika Nchini**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Ushirika hapa nchini unazidi kuzorota siku hadi siku huku soko huru likizidi kushamiri na kuchukua nafasi ya Vyama vya Ushirika:-

(a) Je, ni nini juhudi za Serikali za kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini?

(b) Kama Serikali imeshindwa kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini, je, kwa nini isiunde Wizara ya soko huru na masoko kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, napenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa ushirika hapa nchini unazidi kudorora siku hadi siku ingawaje ni kweli kwamba katika miaka ya nyuma hali ya ushirika hapa nchini haikuwa nzuri kutokana na sababu mbalimbali. Kufuatia hatua mbalimbali za Serikali za kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika hivi sasa wananchi wengi wameanza kurudisha imani kwa Vyama vya Ushirika

na hivyo kuvifanya kuanza kiumarika tena. Mfano mmojawapo mzuri ni Vyama Vikuu 16 na Vyama vya Msingi 11 vya mazao vilivyofanya vizuri katika msimu wa 2002/2003.

Aidha, kumekuwapo na ongezeko kubwa la Vyama vya Kuweka na Kukopa kutoka Vyama 701 mwaka 2000 hadi Vyama 1236 mwaka 2003. Vyama vya Ushirika vya Wafugaji viliongezeka kutoka Vyama 70 mwaka 2002 hadi Vyama 95 mwaka 2003. Vyama vya aina nyingine vinaendelea kuongezeka japokuwa kasi yake si kubwa sana na jumla ya wanachama imeongezeka kutoka 500,000 hadi 750,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Ushirika ni chombo muhimu cha kuwawezesha wananchi kupita vita umaskini na kujiletea maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, hivyo Serikali kupitia Wizara ya Ushirika na Masoko imeandaa mazingira mazuri na inaendelea kuyaboresha ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kufanya kazi.

Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kutayarisha sera mpya ya maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002, kuwawezesha wanachama kumiliki na kusimamia Vyama vyao vya Ushirika kwa kutoa mafunzo kupitia Mpango wa Elimu ya Ushirika Shirikishi yaani *Member Empowerment in Cooperatives*, kuanzisha Mfuko wa *Export Credit Guarantee Scheme* na kutunga Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika inayokidhi mahitaji ya sasa ya kuviimarisha Vyama vya Ushirika. Muswada wa sheria hiyo utawasilishwa na kujadiliwa Bungeni leo hii.

Serikali pia inaendelea kuandaa na kukamilisha programu kabambe ya kurekebisha mfumo na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika nchini yaani *Cooperative Reform Programme* ambayo itashughulikia hatua zote zinazotakiwa katika kufufua, kuimarisha na kuendeleza Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza katika maelezo yangu ya awali, Serikali haijashindwa kuimarisha Vyama vya Ushirika. Kwani kwa kupitia hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Wizara yangu, Serikali imefanikiwa kurejesha imani ya wananchi iliyokuwa imepotea kuhusu uwezo wa Ushirika na matokeo yake yameanza kuonekana wazi kama nilivyoeleza kwa kina katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004 ambayo nawaomba Waheshimiwa Wabunge warejee kuisoma.

Na. 54

**Upatikanaji wa Cheti cha Kuzaliwa**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGILEHI (k.n.y. MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipokuwa akijibu swali Namba 287 hapo tarehe 22 Julai, 2003 katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge alikubali kwamba kazi ya Idara ya Vizazi na Vifo ni kusubiri kusajili tu watoto wanapozaliwa ili kabla ya miezi mitatu mzazi alipe shilingi 3,500/= ili kupatiwa cheti na kwamba kama ukipita muda huo mzazi anawajibika kulipia shilingi 4,000/= kwa cheti hicho na zaidi ya muda huo mzazi huwajibika kukifuatilia cheti hicho kwenye Makao Makuu ya Wilaya kwa gharama zake na kulipa faini ya shilingi 10,000/=; na kwa kuwa kuna vituo vya Afya, Zahanati kwenye kila Kata na hata hospitali kwenye baadhi ya Kata ambako Msajili wa Vizazi na Vifo anaweza kuwepo huko ili kutoa vyeti hivyo pale mtoto anapozaliwa na kuokoa gharama na muda unaopotea kufuatilia hati hizo:-

(a) Ikiwa akina mama wengi hawana uwezo hata wa kununulia hata vifaa kama nyembe, *gloves* na kadhalika vya kuhudumia mtoto wakati anapozaliwa. Je, hizo fedha za kulipia cheti cha kuzaliwa atazipata wapi?

(b) Kwa kuwa asilimia 50 ya watoto wa Kitanzania hawana vyeti vya kuzaliwa kutokana na umaskini wa akina mama wa Vijijini na Mijini. Je, Serikali haioni kwamba wakati sasa umefika wa kutoa vyeti vya kuzaliwa bila malipo yoyote kwa sababu ni haki ya msingi ya mtoto?

(c) Kama Serikali imeweza kusamehe kodi ya maendeleo kwa Watanzania wote, je, haina njia nyingine yoyote ya kufidia gharama ya cheti hicho ili vitolewe bila malipo na kwa wakati ili kuwaondolea kero akina mama hao?

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu ambayo ndiyo inahusika na usajili wa vizazi na vifo pia ina majukumu mengineyo muhimu kama vile kusimamia udhamini na usimamizi wa mirathi, usajili wa ndoa na talaka, masuala ya watoto na kulea, ufilisi na usimamizi wa mali zisizo na wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya jumla, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kwa sababu yote yanataka mtoto anayasajiliwa apewe cheti bure kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la kumhudumia mtoto anapozaliwa siyo la mama peke yake bali ni la wazazi wake wote. Hivyo wazazi sharti watimize wajibu wao kwa mtoto anayezaliwa ikiwa ni pamoja na kulipia shilingi 3,500/= ambazo ni mchango kwa ajili ya gharama za upekuzi na hati ya kusajiliwa katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza tangu mtoto azaliwe.

Mheshimiwa Spika, ada ya shilingi 4,000/= hutozwa kutoka kwa wazazi ambao watoto wao wanasajiliwa baada ya miezi mitatu na kutozidi miaka 10. Shilingi 10,000 hutozwa kwa kupatiwa cheti kizazi kitakachosajiliwa baada ya miaka 10 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kumsajili mtoto limewekwa kisheria kuwa ni la wazazi wa mtoto huyo sambamba na majukumu mengineyo ya kumpa mtoto huyo haki za msingi kama vile chakula, malazi na kadhalika kulingana na hali halisi ya gharama za maisha viwango hivi ni vya chini kabisa ili kutoa unafuu kwa wazazi. Mathalani iwapo utadhamiria kupata mtoto kila mwaka utahitajika kuwekeza shilingi 11/= kila siku kiasi ambacho si kikubwa kwa jambo unalotenda la kutafuta mtoto. *(Kicheko)*

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haina uwezo wa kutoa huduma zote za jamii bure.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika Bunge la Bajeti lililopita Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliona kwamba watu hawawezi kulipa kodi ya shilingi 3,000/=; na kwa kuwa hizi shilingi 3,500/= anazosisema hazijajumlisha gharama za mtu kusafiri kutoka vijiji vya mbali kwenda Makao Makuu.

Je, sasa Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba ni wakati muafaka wa kufanyia tathmini utaratibu mpya wa hizi kodi zinazopaswa kulipwa ikiwa pamoja na muda na utaratibu wenyewe ili kuubadilisha na kuondoa kero hii kwa wananchi?

(b) Kama Mheshimiwa Waziri hajafanya uchunguzi wa utaratibu huo je, kwa kupitia swali na kwa kupitia Bunge hili, anaahidi kufanya zoezi zima hilo la uchambuzi wa kutosha ili awe na majibu ambayo yanawahisishia wananchi na kuwaondolea kero hii ambayo tumeisema?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, suala ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni kero. Nasema hii si kero kwa sababu hiki ni cheti ambacho kinaambatana na shughuli ambayo ni ya raha, kwa hiyo haiwezi kuwa kero kwa kweli. Wewe umemtafuta mwanamke umemuoa na mmetaka watoto na mmewapata, mshukuru Mwenyezi Mungu. Sasa inakuwaje tena ni kero. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba hiki ni chombo tulichonacho cha Kabidhi Wasii ni *Executive Agency* ambayo ina gharama zake. Fomu lazima zitengenezwe na ma-*registrar* katika Wilaya lazima wawepo. Kwa hiyo, kuna gharama nyingi za *record keeping* na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, tunahitaji hizi *Executive Agency* ziwe *financially self support*. Kwa hiyo, umuhimu wa kuwa na ada kama hizi ni muhimu kwa kweli kuweza kuifanya Ofisi ya Kabidhi Wasii ifanye kazi zake vizuri.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa nchi zilizoendele zina *register* ya watoto wote waliozaliwa, na kwa kufanya hivyo kunarahisisha *register* ya wapiga kura. Je, ni lini sisi Watanzania tutakuwa tayari au tuna mikakati gani ya kufanya hivyo ili tufanane na hizo nchi zilizoendele hasa ikizingatiwa ni karne ya 21 hii?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko mbioni kuandaa *register* ya namna hiyo na ni mategemeo ya Serikali kwamba ifikapo mwaka 2005 tunaweza kuwa *voters register*.

Na. 55

### **Kuanzishwa kwa *International Criminal Court***

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kuna harakati za kuanzisha Mahakama ya Kimataifa (*International Criminal Court*) itakayokuwa inashughulikia uhalifu wa halaiki na kadhalika na kwa kuwa nchi yetu imeridhia Mkataba wa kuanzishwa kwa Mahakama hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali italeti Bungeni Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuanzishwa kwa chombo hicho?

(b) Je, Serikali imejifunza nini kutokana na *International Tribunals* zilizopo hivi sasa, mfano ile ya Arusha na kadhalika?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YAKATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) naomba nitoe maelezo ya jumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba wa kuanzishwa kwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (*Rome Statute of the International Criminal Court*) tarehe 20 Agosti, 2002.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu unatoa mamlaka ya kwanza kabisa kwa Mahakama za ndani ya nchi mwanachama kuendesha mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa yanayohusika, yaani mauaji ya halaiki, makosa ya kivita na makosa dhidi ya ubinadamu. Mahakama hiyo ya Kimataifa itakuwa na mamlaka (*complementarity*) pale tu ambapo Mahakama za nchi mwanachama hazina uwezo au nchi mwanachama haitaki kuendesha mashitaka dhidi ya watuhumiwa hao kwa nia ya kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kupitia Wizara yangu, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na wadau wengine wanaandaa utaratibu muafaka utakaoweza utekelezaji wa mkataba wa Mahakama ya Kimataifa wa jinai.

(b) *International Tribunals* zilizopo kama vile ile ya *International Criminal Tribunal for Rwanda* iliyopo Arusha ni Mahakama ambazo siyo za kudumu ni *ad hoc* tofauti na itakavyokuwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (*International Criminal Court*). Mamlaka ya Mahakama (*Tribunals*) hizo yana kikomo kinachozingatia muda na eneo au nchi ambayo uhalifu huo unafanyika.

Tumejifunza mengi kutoka kwa hizo *International Criminal Tribunals*. Moja ni kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kukwepa uwajibikaji kwa kutenda mauaji ya halaiki, makosa ya kivita na makosa dhidi ya ubinadamu kwa kuzingatia nafasi yake katika jamii au Serikali. Tumeshuhudia kukamatwa na kushtakiwa kwa aliyekuwa Rais wa Yugoslavia wa zamani, na pia kushitakiwa na kuhukumiwa kwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa zamani wa Rwanda.

Pili, tumejifunza kwamba mtu atawajibishwa na hatimaye kutiwa hatiani kwa kutochukua hatua zozote kuzuia utendaji wa makosa tajwa, pale ambapo alikuwa katika nafasi au wadhifa wa kuweza kuzuia utendaji wa makosa hayo lakini hakufanya hivyo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa suala la kuwepo vyombo vya Kimataifa katika nchi mbali na zile shughuli walizokusudia, lakini pia huwa ni kitengo uchumi kwa nchi husika. Mheshimiwa Waziri haoni pamoja na kuwa jambo hilo bado lakini angalau kwa sasa kukatafutwa sehemu ya kutosha tu ambayo kama ikitokea patajengwa. Kwa sababu uzoefu unaonyesha wenzetu wanaofanya hivyo *in the long run* wanaweza kupata fedha nyingi kama wanavyopata Kenya leo kwa masuala ya Umoja wa Mataifa?

(b) Vyombo hivyo vya Kimataifa mbali na kuwa vinatumia lugha ya Kiingereza na kama tulivyozoea, lakini huwa vinatumia lugha nyingine zaidi na uzoefu wa nchi yetu inaonekana kidogo tunadharau masuala ya *by linguistics* na mambo mengine. Haoni ni wakati umefika wa Serikali kuchukua mkakati maalum wa kufundisha vijana ili linapotokea suala kama hilo tuweza kuwaajiri kwa wingi na hizo nafasi zisichukuliwe na watu wa nchi nyingine?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YAKATIBA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kabisa kwamba tukiwa na vyombo hivi vya Kimataifa vinakuwa kwa kweli vinasaidia kuendeleza uchumi wetu, kulitangaza jina la nchi yetu na kuweza

kuwa na watu mbalimbali wanaokuja kuitembelee nchi yetu, na hivyo hata kujionea hata rasilimali zetu na kuweza kukuza utalii na mambo mengine. Hilo ni suala njema kabisa, lakini kutokana na makubaliano yaliyotokea basi ikabidi kwamba Mahakama hii iweze kukaa mjini Brussels.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwaendeleza vijana wetu nakubaliana na Mheshimiwa Khalifu Suleiman Khalifa, kwamba lazima tujaribu kuwaelimisha vijana wetu katika fani mbalimbali za kisheria hasa sheria za *International Law* ikiwa pamoja na lugha ya Kifaransa, Kilatini na Kiarabu ili waweze ku-*qualify* na kuingia katika *Institutions* za Kimataifa.

Na. 56

### **Vituo vya Kulelea Watoto Yatima**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa tafsiri ya Taifa ni watu waliozaliwa ndani ya mipaka ya Taifa husika; na kwa kuwa katika Taifa wapo watoto wanaozaliwa na wanatakiwa kulelewa ipasavyo kufikia kuwa watu kamilifu na viongozi wa Taifa; na kwa kuwa hapa kwetu tunazo Wizara mbili zinazoshughulikia masuala haya kwa ushirikiano yaani Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto:-

(a) Je, kuna vituo vingapi vya kulelea watoto yatima nchini, viko katika Mikoa ipi na idadi yake kwa kila Mkoa kwa kutaja majina ya vituo husika?

(b) Je, ni vituo vingapi vimesajiliwa na ni vingapi havijasajiliwa kwa kutaja majina ya kila kituo na Mikoa viliko?

(c) Je, Serikali itakubali ushauri kwamba, vituo hivyo viwekwe chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili viweze kueleweka vizuri na kuhudumiwa kwa ufasaha zaidi?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna Makao 57 nchini ambayo yanatunza na kulea watoto yatima na wenye shida mbalimbali za kijamii Makao hayo 57 yanatambuliwa na Serikali chini ya Wizara yangu na yamepewa leseni ya kuyaendesha. Kwa kuwa orodha hiyo ni ndefu, naambatanisha orodha hii na jibu la swali hili ili nimpatia Mheshimiwa Mbunge baadaye.



(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a), Makao yaliyopo ni 57 na yote yamesajiliwa na kupata leseni ya kuyaendesha, hivyo hatuna Makao ambayo hayajasajiliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, huduma ya kuendesha Makao ya kutunza watoto yatima na wenye shida za kijamii hutolewa kulingana na sheria ya Makao ya Watoto Na.4 ya mwaka 1968 na taratibu (*regulations*) za kuendesha Makao za mwaka 1968. Sheria hii inatoa mamlaka kwa Wizara yangu kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu kupokea, kutunza na kuendesha Makao ya Watoto Yatima na wenye shida hapa nchini. Chini ya Sheria hii Wizara ina majukumu ya kusajili Makao, kukagua Makao, kusimamia Malezi ya Kambo (*Foster care*) na kuasili (*adoption*).

Aidha, Wizara yangu inao Maafisa Ustawi wa Jamii wenye taaluma na uzoefu wa kutosha katika kusimamia na kutoa ushauri sahihi katika suala la kuanzisha, kuendesha Makao ya watoto, kusimamia na kutoa ushauri kuhusu huduma za kijamii zitolewazo kwa ajili ya matunzo, maendeleo na ulinzi kwa watoto wanaotunzwa kwenye Makao ya Watoto Yatima na wenye shida.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu nguvukazi na raslimali tuliyonayo Wizarani kwangu, mimi naamini kabisa kuwa vituo hivi vinahudumiwa ipasavyo kwa kuzingatia uwezo wa Serikali. Isitoshe kwa kuwa Wizara zote mbili, yaani Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Wizara ya Maendeleo na Jamii, Jinsia na Watoto ni za Serikali moja inayoongozwa na Ilani moja. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tunafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana, na kwa hiyo kuvifanya vituo hivi viendeleo kueleweka vizuri na pia kuhudumiwa vizuri.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri ana habari kwamba sababu ya Wizara hizi mbili kufanana fanana katika matamshi yake, hii ni Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na nyingine ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Hizi Wizara ana habari kwamba zinawachanganya watu wenye matatizo hasa katika kipindi hiki ambacho janga la Ukimwi limekuwa ni kubwa zaidi hivyo wahusika wanashindwa kupata mahali pa kupeleka matatizo yao hata kuweza kupeleka watoto kulelewa?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, wala majina ya Wizara hizi mbili hayachanganyi haya, mimi naona yako waziwazi kabisa, kila Wizara jina lake linajitegemea. Lakini vilevile kuna kukanganyikiwa kwa wananchi ni juu yetu sisi Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha. Ni sawasawa kwa mfano, sasa hivi kuna kukanganya kati ya Michezo na Utamaduni, lakini tunaendelea kusaidiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni kufahamisha wananchi kwamba haya mambo ni ya utamaduni yanakwenda katika Wizara ya Elimu na Utamaduni na haya mambo ni ya Michezo yanakwenda katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. (*Makofi*)

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali ndogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa maendeleo ya vijana ni pamoja na maadili ya vijana. Kuna utaratibu gani kuendeleza zile *Juvenile Courts* ambazo zilikuwepo pia zinashughulikia matatizo yanayowakabili vijana nchini. *Juvenile Courts* (Mahakama Maalum) za watoto sisikii chochote kabisa. Je, Serikali ina mpango gani kuendeleza Mahakama hizo?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MCIHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni swali jipya, lakini pamoja na hayo nitajitahidi kulijibu. Mahakama za Watoto au zinazohukumu watoto bado zipo na jela za watoto bado zipo. Kwa hiyo, ule utaratibu anaoufikiria wa kujaribu kuwalea watoto katika mazingira yanayofanana na hali zao bado upo na kama anataka Mheshimiwa Mbunge namkaribisha nimpeleke akazitembelee baadhi ya Taasisi hizi.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango kuhusiana na Mahakama hizi za watoto katika Progamu ya *Quick Start*. Katika hotuba yangu ya mwaka huu wa fedha 2003/2004 tulizungumzia suala hili na inaelekea kwamba tutapata pia wafadhili na Serikali ya Canada imeonyesha nia kwa kweli ya kutusaidia. Kwa hiyo, sasa hivi tuna Mahakama Dar es Salaam ya Watoto na pia kuwa mpango wa kuwa na Mahakama Mbeya, Mwanza pamoja na Mtwara hivi karibuni. (*Makofi*)

Na. 57

### **Chombo cha Kuwasaidia Vijana kupata Kazi Nje**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inao mpango mzuri wa kuanzisha chombo kitakachowasaidia vijana wa Kitzania kupata kazi nje ya nchi yetu:-

(a) Je, ni vijana wangapi walioko nje ya Tanzania?

(b) Je, ni wangapi ambao wamefungwa nje ya nchi?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina kumbukumbu zinazohusu idadi ya vijana wa Kitzania waliopo nje. Kwa sababu vijana hawa wanapokwenda nje kufanya kazi hupitia sehemu mbalimbali.

Kwa mfano, wapo waliondoka kupitia Serikalini, wapo waliondoka kupitia Mashirika ya Umma, wapo waliopelekwa na Makampuni ya Watu binafsi, wapo waliobaki nje baada ya kumaliza masomo na wapo waliotoroka au kuzamia kama wanavyojiita wenyewe na kadhalika. Mbaya zaidi ni kwamba wengi wa vijana hawa huwa hawaripoti kwenye Balozi zetu za nje hata baada ya kutangaziwa kufanya hivyo mara kwa mara.

(b) Kuhusu vijana waliofungwa nje ya nchi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa upo uwezekano kuwa baadhi ya vijana wa Kitanzania wamefungwa nchi za nje kwa makosa mbalimbali, na ukusanyaji wa takwimu zao unaendelea ili idadi kamili ifahamike.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, swali langu lilikuwa linauliza Serikali ina mpango kuanzisha chombo? Lakini naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa vijana wengi wasomi wanapomaliza Vyuho wanapoomba ajira hukumbana na kikwazo cha uzoefu wa kazi kwa zaidi ya miaka mitatu, jambo ambalo husababisha vijana wengi kukimbia nchi hii. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kipengele hicho? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa sasa tunaingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, na moja ya vipengele ni kwamba kutakuwa kuna ajira huru; na kwa kuwa itagusa zaidi kwenye elimu na taaluma. Je, nchi yetu imejiandaa vipi katika hilo?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu matangazo ya kazi kuhitaji waombaji wawe na uzoefu wa miaka mitatu na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba tufahamu kwamba tupo katika soko huru la ajira. Tunachofanya sisi kama Wizara ni kuzungumza na waajiri mbalimbali kuwashawishi na kuwaelevesha kwamba wakiendelea kufanya hivyo watakuwa wanajenga mazingira ambayo hayatatuletea amani na utulivu katika nchi yetu. Baadhi ya Makampuni wameanza kutuelewa.

Kwa mfano, ukiangalia Kampuni ya *CAT* sasa hivi wanachukua vijana waliomaliza tu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanawaajiri na kuanza kuwafundisha kazi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Makampuni ya Migodi yanayochimba dhahabu wameweza kuchukua vijana *fresh* kutoka Chuo Kikuu wanawaajiri na kutoka hata *VETA* wanawaajiri halafu wanawaongezea ujuzi wa kazi wenyewe. Kwa hiyo, hilo tumeanza kulifanyia kazi.

Kwa hiyo, ingewezekana kama mwajiri mkuu bado ni Serikali kama ilivyokuwa zamani kusema kwamba tunapiga marufuku. Lakini unapokuwa na Makampuni au ajira huru kama tuliyonayo sasa haiwezekani kulikabili hilo kwa kutoa amri. Kama mnavyoona katika matangazo ya kazi yanayotolewa na Serikali huwa hawasisitizi sana uzoefu wa miaka mitatu na kuendelea, kinachohitaji ni taaluma za aina fulani.

Kwa mfano, sisi Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo tumetangaza kazi kwa kupitia ile Wakala wa Serikali, tulichosema pale ni kwamba tunahitaji mwenye Shahada ya *Psychology* hatukusema tunahitaji aliyekaa na Shahada ya *Psychology* kwa miaka kumi. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya Afrika Mashariki, ni kweli itazingatia taaluma, lakini kabla hatujafika huko tumeshaanza kuzungumza na wenzetu jinsi ambavyo kwanza sheria zenyewe za ajira na kazi zitakavyokuwa harmonized ili kuleta mazingira yanayowiana.

Vile vile hata katika *forum* mbalimbali ni juu yetu sisi Waheshimiwa Wabunge na wale wote ambao tunahusika katika kuwahamasisha wananchi tuhakikishe wananchi wetu nao wanajitahidi na kujizatiti katika kuendelea kujizatiti kitaaluma na katika stadi za kazi. Kwa sababu huko tunakokwenda katika soko la ajira huru itakuwa ni vigumu kuweka *quarter*, mwajiri atakuwa huru kuchukua wale ambao anaona wanamfaa.

Hivyo hivyo, hata katika nidhamu ya kazi na *attitude* ya kazi tunapozungumza na Vyama vya Wafanyakazi, tuwasihi nao wajue kwamba mazingira yamebadilika lazima nao wabadilike, wawe wanajielekeza katika kudai haki inayoambatana na wajibu. (Makofi)

Na. 58

### **Wapiga debe kwenye Vituo vya Mabasi**

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU (k.n.y. MHE. ADELASTELE E. MKILINDI)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika siku zilizopita lilitolewa agizo kuwa wapiga debe kwenye vituo vya mabasi kuacha kazi hiyo kwa kuwa imekuwa ikileta usumbufu kwa abiria hasa akinamama na kwamba baadhi ya wapiga debe hao ni vibaka hivyo huwanyang'anya abiria vitu mbalimbali kama vile saa, simu za mkononi na wengine hudiriki kutoweka na mizigo ya abiria:-

(a) Je, kwa mara ya kwanza agizo hili lilitolewa lini?

(b) Je, ni vituo gani vya mabasi ya Mkoa ambavyo vimeweza kutekeleza agizo hilo (vitajwe kwa majina) na vile ambavyo havikutekeleza agizo hilo ni vipi kwa majina na ni kwa sababu zipi?

(c) Je, Serikali itatumia mbinu gani ili kukomesha adha hiyo kwa Mikoa ambayo haijafanikiwa kumaliza tatizo hilo ukiwemo Mkoa wa Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa wapiga debe kwenye vituo vya mabasi wamekuwa wakileta usumbufu na adha kwa abiria hasa akinamama na kwamba baadhi ya wapiga debe hao ni vibaka hivyo huwanyang'anya abiria vitu mbalimbali kama vile saa, simu za mkononi na wengine hudiriki kutoweka na mizigo ya abiria. Kutokana na kero hii ya wapiga debe, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka za Usafirishaji za Mikoa, lilitoa agizo la kukomesha vurumai za wapiga debe kwenye vituo vya mabasi. Agizo hili lilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2001.

(b) Mheshimiwa Spika, agizo la kutaka wapiga debe waache kazi hiyo lilitokelezwa na Jeshi la Polisi nchi nzima kwa njia ya operesheni. Mikoa ambayo tatizo la wapiga debe lilijitokeza sana na Jeshi la Polisi kuelekeza nguvu zake zaidi ni Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mbeya, Dodoma, Shinyanga, Mara na Mwanza. Muda baada ya operesheni hiyo, tatizo hilo lilibuka tena katika baadhi ya Mikoa kama vile Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. Hili linatokana na hali ya wapiga debe kujichanganya na watumishi wa mabasi na kulipwa ujira kila siku na wenye mabasi. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka za Wasafirishaji za Mikoa pamoja na Vyama vya Wamiliki wa mabasi linaendelea kupambana na kero za wapiga debe kwa kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kukomesha adha ya wapiga debe katika Mikoa ambayo haijafanikiwa kumaliza tatizo hilo, Serikali itatumia mikakati au mbinu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya misako na doria za mara kwa mara katika vituo vya mabasi ya abiria na kuwakamata wapiga debe na kuwachukulia hatua za kisheria.

(ii) Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mamlaka za Mikoa, wamiliki wa mabasi na wadu wengine litatoa elimu kwa umma kuhusu adha ya wapiga debe na hivyo wasaidie kupambana na wapiga debe; kwa mfano, wenye mabasi kuacha kuwalipa wapiga debe ujira wa kila siku.

(iii) Kuwataka wamiliki wa mabasi ya abiria wawaajiri madrevu na makondakta ambao wamehudhuria mafunzo ya utoaji wa huduma kwa wasafiri katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

(iv) Mamlaka za Miji, hutenga maeneo maalum kwa ajili ya ofisi za utoaji wa huduma kwa wasafiri ikiwa ni pamoja na ukataji wa tiketi za mabasi.

(v) Wamiliki wa mabasi wanatakiwa kutoa sare na vitambulisho maalum kwa ajili ya madreva na makondakta ili waweze kujitofautisha na wapiga debe na pia waweze kutambulika kwa kiurahisi na wasafiri wa mabasi.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya wapiga debe, kama ilivyo katika aina zingine za uhalifu haiwezi kuendeshwa kwa mafanikio kwa kutumia Jeshi la Polisi pekee. Vita hii inahitaji wadau mbalimbali washiriki, hasa wamiliki wa mabasi, madreva na makondakta, mamlaka za utoaji leseni za magari Mikoani, na wananchi wote kwa jumla.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu marefu sana yasiyo ya msingi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wewe uliza swali la nyongeza usipige porojo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu marefu naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ikitamka kitu na ikiwa na nia inatekeleza. Kwa mfano, vibanda vya akinamama lishe na wamachinga vilivunjwa *within a day* kwa kutekeleza agizo la Serikali. Inakuwaje Serikali inasuasua katika kuhakikisha akinamama na wasafiri wote wanapata tiketi zao kwa utaratibu unaoeleweka bila kuvurugwa na kuanguka na wakati mwingine kudhalilishwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali haisuisui katika kupambana na wapiga debe na vita dhidi ya wapiga debe inaendelea. Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba baada ya muda si mrefu vumbi litatimka katika kumaliza kabisa zoezi la wapiga debe. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Msekela, swali lako litatafutiwa nafasi nyingine, naona muda wa maswali umekwisha. Tunaendelea na shughuli nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo ya vikao vya leo pamoja na ya semina, lakini kabla sijatoa matangazo hayo, napenda kuomba ruksa na kutoa taarifa kwamba, Spika (mimi) sitakuwepo Bungeni kuanzia Jumatatu, sababu yake ni kwamba nimepokea barua ifuatayo kutoka kwa Mheshimiwa Rais, anasema: “Nilikuwa nimekubali mwaliko wa *African Wildlife Foundation* kuhudhuria kongamano na chakula cha usiku vyote vikiwa na kauli mbiu isemayo “Hifadhi ni Biashara Nzuri”(*Conservation is a Good Business*).”

Kongamano na chakula vinafanyika Mjini Washington, Marekani wiki ijayo. Katika chakula hicho ningepewa kwa niaba ya nchi yetu nishani kwa kutambua mchango wetu katika kuhifadhi wanyamapori. Niliombwa pia nitoe hotuba *key not address*. Kwa bahati mbaya kwa sababu ya matatizo yangu ya kiafya, Madaktari wamenishauri nisifanye safari hii ndefu, lakini shughuli yenyewe ni muhimu na ni vizuri apatikane

kiongozi mwingine mwenye uzoefu wa masuala haya na hadhi ya kutosha kuniwakilisha mimi. Kwa hiyo, nimeamua nikuombe wewe Spika uniwakilishe kwenye kongamano hilo na chakula.” Kwa ajili hiyo, sitakuwepo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hamumwoni kwa sababu yeye ananiwakilisha kwenye Mkutano wa Maspika wa *Commonwealth Africa* kule Mauritius, lakini mkutano unakwisha leo. Jumatatu atakuwa amesharudi na ataendelea kusaidiana na Mwenyekiti kuongoza Shughuli za Bunge. Kwa hiyo, hatutakuwa na shida yoyote kwa upande wetu. (*Makofi*)

Sasa ni matangazo ya vikao vya leo. Kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, ndiye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, anaomba Wajumbe wakutane chumba namba 81 kuanzia saa tano asubuhi hii.

Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba Wajumbe wa Kamati wakutane kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kufikiria Muswada wa Usafiri wa Majini saa tano hiyo hiyo, namba ya chumba hakutaja, lakini nadhani Waheshimiwa wataelekezwa.

Matangazo kuhusu semina, nakumbusha kwamba kesho itakuwepo ile semina iliyopangwa, inahusu Mbinu na Mikakati ya Kupambana na Malaria, inafunguliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais. Kesho kutwa Jumapili kama mlivyoandikiwa leo asubuhi, vile vile nimeidhinisha semina nyingine inahusu Tathmini ya Shughuli za Sekta ya Madini hapa nchini. Kwa hiyo, ni mfululizo wa semina siku mbili.

Kwa kuwa kesho kuna matembezi ya hisani yanayoongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na yatachukua muda, tumepanga semina ianze saa tano asubuhi badala ya saa tatu asubuhi ya kawaida ili kuwapatia muda Waheshimiwa Wabunge watakaoshiriki kujiweka tayari kwa semina. Hali kadhalika ile ya pili kwa sababu ni Jumapili huwa tunapanga shughuli zinaanza saa tano asubuhi ili wale wanaokwenda makanisani wawe wamekwishamaliza shughuli zao. Kwa hiyo, ni semina mbili kesho na keshokutwa na zote mbili zitaanza saa tano asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, katika barua mliyoandikiwa semina ya Jumapili ilielezwa kwamba itakuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, hapana haitakuwa hivyo. Utaratibu wetu ni kwamba, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na suala hilo ndiye anakuwa Mwenyekiti. Kwa hiyo, itakuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo.

Matangazo mengine ni kwamba, yale matembezi ya kesho wawakilishi wa yale Mashirika yanayowafadhili watakuwa hapa kwenye viwanja vya Bunge leo kwa ajili ya kugawa fulana na kofia kwa watakaotembea. Watakuwa katika maeneo yetu yale ya *pigeonholes*. Kwa hiyo, wanaojiandaa kutembea waonane na mwakilishi huyo.

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Dr. Pius Ng’wandu; Waziri, anawaomba Wabunge wanaotoka Wilaya zile zinazofadhiliwa na Waholanzi katika

mpango unaoitwa *District Rural Development Program (DRDP)*, nadhani Wilaya hizo si nyingi, mkutane naye hapo nje mara baada ya maswali. Anasema ni taarifa fupi tu anataka kuwapatia.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*.  
Katibu.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2003 (*The Cooperative Societies Bill, 2003*)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 (*The Cooperative Societies Bill, 2003*) sasa usomwe mara ya pili kama ulivyopangwa kwenye shughuli za leo.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze hotuba yangu kwa kutoa shukrani za dhati kwa vyombo vyote vilivyoweza Muswada huu kukamilika na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli na Wajumbe wa Kamati yake kwa uchambuzi wao wa kina wa Muswada huu na kwa mapendekezo yao ambayo nimeyatumia katika kuboresha Muswada huu. Mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika nyongeza ya marekebisho ya Muswada (*schedule of amendments*) ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau wa Sekta ya Ushirika ambao walishiriki kikamilifu katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo juu ya vipengele vyote vya Muswada huu. Hawa ni pamoja na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Nchini, Vyama vya Ushirika Vikuu na Kilele na pia Vyama vya Msingi. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Taasisi za Utafiti na Mafunzo, Bodi za Mazao, Mabenki, Idara mbalimbali za Serikali pia zimeshirikishwa katika kutoa mchango wao wa mawazo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba Sheria ya Vyama vya Ushirika namba 14 ya mwaka 1982 ilirekebishwa na tukapata sheria namba 15 ya mwaka 1991. Sababu ya msingi ya kufanya hivyo ilikuwa kutoa uhuru kwa wanachama kuvitawala Vyama vyao kulingana na misingi ya Ushirika duniani.

Mheshimiwa Spika, tangu Sheria ya Ushirika ya mwaka 1991 ianze kutekelezwa, uzoefu umeonyesha mapungufu mbalimbali ambayo yanachangia kukwamisha jitihada za kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini.

Aidha, tangu wakati huo yametokea mabadiliko katika Sera za Uchumi za Taifa na Mfumo wa Uchumi na Biashara Ulimwenguni ambayo hayana budi kuzingatiwa na



Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kuviwezesha Vyama kuendeshwa kulingana na mahitaji ya wakati.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa pia kwamba Sera mpya ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2000 ilipitishwa na Serikali mwezi Aprili, 2000. Sera hiyo ambayo pamoja na mambo mengine imetokana na Taarifa ya Kamati Maalum ya Rais ya Kumshauri juu ya Kufufua, Kuimarisha na Kuendeleza Ushirika Tanzania ya mwaka 2000 ina mwelekeo wa kutekeleza azma ya Serikali ya kutatua matatizo yanayokabili Ushirika nchini kwa madhumuni ya kujenga ushirika imara. Utekelezaji wa Sera hiyo kupitia mikakati ya utekelezaji wake unahitaji kutungwa kwa Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika itakayowezesha kuwepo kwa mazingira muafaka yatakayoufanya Ushirika ukidhi mahitaji ya wanachama, wadau wengine na umma wa Tanzania kwa ujumla. Aidha, tunahitaji sheria hii mpya ili kuboresha utendaji na uwajibikaji katika Vyama vya Ushirika kwa kusisitiza mambo yafuatayo: -

(i) Kutambua umuhimu wa Vyama vya Ushirika kuwashirikisha wanachama kuvitawala Vyama vyao.

(ii) Kujenga dhana ya ujasirimali na kuondoa tabia ya kuwa tegemezi kwa Serikali wakati wote.

(iii) Kuwezesha Vyama kujenga mitaji endelevu ili viweze kuhimili ushindani wa soko huru; na

(iv) Kuainisha maadili ya uongozi kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika na Watendaji.

Mheshimiwa Spika, Sera mpya ya Ushirika na Sheria ya Ushirika inayotarajiwa ni hatua muhimu za kufanikisha mabadiliko makubwa katika Sekta ya Ushirika. Mabadiliko hayo na utekelezaji wake vinaendelea kuainishwa katika *Cooperative Reform Program* ambayo inategemewa kukamilishwa mwishoni mwa mwezi Desemba, 2003. Aidha, mabadiliko yanayotarajiwa kufanywa katika Sheria ya *COASCO* namba 15 ya mwaka 1982 na marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine yatachangia kikamilifu katika kuleta mageuzi katika Sekta ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuleta Muswada huu ni kufuta Sheria namba 15 ya mwaka 1991 na rekebisho lake namba 5 la mwaka 1997 na kutunga Sheria mpya badala yake.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika vina nafasi kubwa katika kuleta maendeleo ya Wananchi na kupiga vita umaskini kwa njia ya kujitegemea. Sheria inayopendekezwa inakusudia kukidhi mabadiliko makubwa katika Sekta ya Ushirika ili kuwezesha Wananchi kumiliki uchumi kwa ajili ya maendeleo yao. Mabadiliko yaliyomo kwenye Sheria hii pia yanalenga kupambana na ubadhilifu na kuweka utaratibu wa kuendesha kesi za Ushirika haraka kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada uliopo mbele yako unazingatia Misingi ya Kuendesha na Kusimamia Ushirika Duniani (*Cooperative Principles*), mabadiliko ya kiuchumi na kijamii (mathalani ujio wa soko huru na utandawazi) na mabadiliko katika Sheria mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria hii sharti ulenge katika uadilifu na uaminifu kutoka kwa makundi yote yanayohusika. Kwa hiyo, Sheria hii ikisimamiwa vizuri itaongeza imani ya Wananchi na Wawekezaji watakaotaka kufanya biashara na Vyama vya Ushirika (kupitia *Joint Ventures*). Kuungwa mkono kwa Sheria hii na kuziwezesha Taasisi zake kufanya kazi ipasavyo ndiyo njia muhimu ya kuimarisha Sekta ya Ushirika iweze kuchangia uchumi wa nchi kwa manufaa ya jamii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uzoefu kutoka nchi nyingine zilizoendelea na zinazoendelea unaonyesha kwamba ushirika ukiimarika una uwezo wa kutoa mchango mkubwa wa maendeleo ya uchumi kwa vile chombo hicho kipo karibu sana na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 16. Sehemu ya kwanza, inaelezea mambo ya kiutangaulizi, yaani jina fupi la sheria (*The Cooperative Societies Act, 2003*) na tarehe ya kuanza kutumika, tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumiwa katika Muswada imetolewa.

Sehemu ya pili, inaelezea maudhui ya Vyama vya Ushirika na misingi yake (*Cooperative Principles*). Sehemu hii pia inaeleza majukumu ya Serikali katika kuendeleza Vyama vya Ushirika na inatoa mwongozo utakaofuatwa na Waziri mwenye dhamana katika kuendeleza Ushirika. Kamati Maalum ya Rais ya mwaka 2000 ya Kumshauri Kuhusu Ushirika ilibaini kuwa kitendo cha Serikali cha kutoweka kipaumbele katika masuala ya Ushirika kilichangia katika kuuzorotesha. Kwa hiyo, sehemu hii inazingatia maoni ya Kamati hiyo kwa kuainisha majukumu ya Serikali katika kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini.

Sehemu ya tatu, inaelezea majukumu ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na wasaidizi wake. Majukumu hayo ni pamoja na kusimamia Sheria, kuandikisha au kufuta Vyama, kufanya ukaguzi, kuhamasisha Elimu ya Ushirika na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika. Mrajisi amepewa majukumu haya muhimu sana kwa kuwa hiki ni kipindi cha mpito cha kutekeleza mpango mahsusi wa kubadilisha Ushirika nchini (*Cooperative Reform Program*).

Utekelezaji wa mpango huu unahitaji usimamizi mahiri. Hata hivyo, sehemu hii inaelezea kuwa kadri Ushirika unavyoimarika, Mrajisi atakabidhi baadhi ya madaraka yake *gradually* kwa Vyombo vya Wanaushirika wenyewe vitakavyosaidiana na Shirika la Ukaguzi la Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) na Chuo cha Ushirika Moshi.

Sehemu ya nne, inaeleza kinaganaga utaratibu wa kuunda Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali. Majukumu ya Vyama hivyo kwa wanachama wake pia yanafafanuliwa katika sehemu hii. Lengo la sehemu hii ni kuhakikisha kwamba Vyama

vinavyoandikishwa vinakuwa na nguvu za kiuchumi, yaani ni lazima viwe *economically viable*.

Katika sehemu hii pia, Sheria inaainisha muundo wa Vyama vya Ushirika unaoendana na mahitaji ya wanachama. Sheria itatambua kwamba kuna umuhimu wa kuwa na Vyama vya Msingi na Shirikisho. Vyama vya Kati, yaani Vyama Vikuu na vya Kilele vitakuwepo kutegemeana na mahitaji na matakwa ya wanachama.

Sehemu ya tano, inaelezea kwa kirefu taratibu za uandikishwaji wa Vyama mbalimbali vya Ushirika. Aidha, sehemu hii inaonyesha kuwa Sheria ya Ushirika itavitambua vikundi vidogo vidogo vya akinamama, walemavu, vijana na wengineo kwa kuandikisha na kuwalea kuwa Ushirika kamili.

Sehemu ya sita, inaelezea haki za wanachama na mipaka ya haki hizo na wajibu. Hii ni pamoja na upiga kura na viwango vya hisa kwenye Chama.

Sehemu ya saba, inafafanua majukumu ya Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kutengeneza masharti (*bylaws*) na Kanuni za Chama wakisaidiana na Mrajisi. Sehemu hii pia inafafanua suala la ukaguzi wa mahesabu ya Vyama.

Sehemu ya nane, inaelezea faida kwa Vyama vilivyoandikishwa (*privileges*). Hii ni pamoja na haki ya kutoza malipo mbalimbali na uwezekano wa kupunguziwa au kufutiwa baadhi ya kodi kunapokuwa na sababu za msingi.

Sehemu ya tisa, inaelezea taratibu za Uongozi wa Vyama vya Ushirika na kuainisha umuhimu wa mikutano mikuu ya wanachama. Sehemu hii pia inaainisha vipindi vya uongozi na utaratibu wa uendelezaji (*continuity*) wa uongozi kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Kufuatia michango ya wadau iliyotolewa wakati wa kujadili Muswada huu na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Halmashauri (*Management Committee*) itajulikana sasa kama Bodi ya Uongozi (*Management Board*).

Sehemu ya kumi, inajihusisha na mali za Vyama vya Ushirika, mikopo, uwekezaji na matengu ya fedha za maendeleo. Suala la kujenga mitaji ya Vyama vya Ushirika lipo katika sehemu hii na itafafanuliwa zaidi kwenye masharti na Kanuni za Vyama.

Sehemu ya kumi na moja, inajihusisha na uandikishaji wa mali mbalimbali za Ushirika zinazoweza kuwekwa rehani au kuuzwa na kadhalika. Sehemu hii inasaidia Vyama vya Ushirika kuwa na utaratibu mzuri wa kutunza mali na kuzitumia kwa usahihi kama dhamana pale inapobidi.

Sehemu ya kumi na mbili, inajihusisha na masuala ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Sehemu hii pia inafafanua kipengele cha malipo ya adhabu (*surcharge*) kwa Watendaji na Wajumbe wa Bodi waliosababisha upotevu au kufanya ubadhirifu wa mali ya Chama.

Sehemu ya kumi na tatu, inafafanua taratibu za Vyama kuungana au kutengana kwa hiari kufuatia sababu za kiuchumi, maamuzi ya mikutano mikuu au ushauri wa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Kuungana au kutengana kwa Vyama kutazingatia sababu za kiuchumi yaani vinavyoangana au kutengana ni lazima viwe *economically viable*.

Sehemu ya kumi na nne, inaelezea taratibu za kufutwa kwa Chama cha Ushirika pale inapobidi kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mfilisi na utaratibu mzima wa jinsi mali husika itakavyouzwa na kugawanywa kwa wadai.

Sehemu ya kumi na tano, inajihusisha na aina ya makosa (*offences*) yanayoweza kutokea kwenye uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na adhabu zitakazotolewa kama makosa hayo yatabainika.

Sehemu ya kumi na sita, inajihusisha na mambo mengineyo (*miscellaneous*) yanayohusu Ushirika. Hii ni pamoja na uteuzi wa Maafisa maalum (*Special prosecutors*) watakaofuatilia na kusimamia kesi za Vyama vya Ushirika. Utaratibu huu utahakikisha kesi zinaamuliwa haraka na kwa haki.

Sehemu hii pia inaainisha ada mbalimbali ambazo zinatakiwa kulipwa na Vyama vya Ushirika katika kuandikishwa, kurekebisha masharti na kadhalika. Ada hizo zimepunguzwa kutoka 11 za awali mpaka 7 katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwapunguzia Wananchi gharama na kero zinazotokana na utitiri wa kodi. Sehemu hii inamalizia kwa kutoa maelezo ya kufutwa kwa Sheria namba 15 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1991 na rekebisho namba 5 la 1997. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia una sehemu ya nyongeza (*Schedule to the Act*) inayojihusisha na Maadili ya Uongozi (*Code of Conduct*) ambayo inakamilisha maudhui ya kifungu namba 125 cha Muswada wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika nyongeza hii Maadili ya Uongozi katika Ushirika yamefafanuliwa na taratibu za kupata Viongozi na kuajiri Watendaji zimewekwa wazi. Dhumuni kubwa la kuwa na *Code of Conduct* ni kuziba mianya ya ubadhirifu na ufujaji wa mali za Wanaushirika.

Hivyo, inategemewa kwamba utekelezaji wa Maadili ya Uongozi katika Sheria mpya utarudisha heshima ya Ushirika ya kuwa chombo madhubuti cha kutegemewa na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yanayowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, yamezingatia maoni ya wadau mbalimbali pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati Maalum ya Rais ya mwaka 2000 ya kumshauri kuhusu kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa michango yao mazuri. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati

kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kwa maoni yao mazuri. Kamati hiyo chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake; Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli pamoja na kufanya kazi kubwa katika kupitia Muswada na vile vile kutoa mapendekezo ambayo yameboresha Muswada huu tokea kuundwa kwake imekuwa ikishirikiana vizuri sana na Wizara yangu katika maswali yote yanayoihusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada uitwao *The Cooperative Societies Bill, 2003* na kuupitisha uwe Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla Mheshimiwa William Shellukindo, hajaitwa kutoa maoni ya Kamati namwomba Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti anipokee.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa mwaka 2003 *(The Cooperative Societies Act, 2003)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 *(The Cooperative Societies Act, 2003)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa ushirikiano na umakini wao katika Kamati wakati wa kutekeleza jukumu la kutazama Muswada huu.

Aidha, nawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati chini ya utaratibu wa *Public Hearing* na kutoa maoni yao kuhusu Muswada wa Sheria hii kwa mujibu wa Kanuni ya 88(6) na Kanuni 69(1) ya Toleo la Kanuni la mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, tulipata wadau wengi tu na kwa kuwa Waziri aliwataja sina haja ya kurudia kuwataja hapa. Wote walielewa vizuri kwamba nia ya Serikali kwa kweli ni kuimarisha Ushirika na wala siyo kuuffifisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu wa kualika wadau kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao unasaidia sana katika kuhakikisha ubora wa Sheria

zinazotungwa na Bunge lako Tukufu, hivyo utaratibu huu uendelee na uboreshwe zaidi hasa kwa Miswada inayogusa maisha na maslahi ya watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu uliipangia kazi ya kufikiria Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 88 (9) ya Kanuni za mwaka 2003. Kamati ilikutana Dar es Salaam tarehe 30 na 31 Oktoba, 2003 na kutekeleza jukumu hilo.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 70 (2) cha Kanuni hizo sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada huu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati yangu inaunga mkono hoja ya Serikali ya kutunga Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika ikizingatia mabadiliko mengi yaliyofanyika katika Sheria ya Vyama vya Ushirika namba 15 ya mwaka 1991 pamoja na kuasisiwa kwa Sera mpya ya Maendeleo ya Ushirika hapa nchini ya mwaka 2002 ambayo utekelezaji wake unahitaji kuwepo kwa Sheria mpya ambayo inaondoa matatizo yaliyovikumba Vyama vya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao ili kuboresha Muswada wa Sheria unaotazamiwa kutungwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Wajumbe wa Bodi zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Sehemu ya 9 Kifungu cha 62 cha Muswada huu wajulikane kwa jina la Bodi za Uongozi au Bodi za *Management* za Vyama vya Ushirika au *Management Board of Cooperative Societies* badala ya Halmashauri kama ilivyokuwa inatumika zamani.

Tunadhani tukiweka utaratibu huu hata bodi hizi zitaingia kwenye kujifunza namna ya kuongoza Vyama vya Ushirika kisasa kwa sababu masomo ya *management* siyo lazima yafundishwe katika maeneo ya ushirika tu, yanaweza kuwa ni ya jumla yanatofautiana kwenye *specialization* ya eneo lenyewe. Kwa hiyo, tunadhani tukitoa jina hili ambalo linaonekana linaeleweka Kimataifa kuliko Halmashauri ni jambo zuri. *(Makofi)*

Aidha, Mwenyekiti na Makamu wa Bodi hizo kwa sasa waendeleo kuitwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti, kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada. Kamati ilipata mapendekezo ya wadau, baadhi wakafika wakasema twende *international*, Kiongozi wa *Apex Organization* aitwe Rais *(President)*. Sasa nikawakumbusha kwamba kuna siku moja nadhani miaka miwili iliyopita Gazeti moja liliandika kwenye *headline* (kabisa ukurasa wa kwanza) kwamba Rais akung'utwa. Kwa hiyo, Gazeti lile lilinunuliwa sana. Kwenda ku-*check* ndani kule kumbe ni Rais wa Chama cha Ngumi na watu wengi walidhani ni Rais wa nchi ndiyo kakung'utwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inafurahi kutoa taarifa kuwa badiliko hili limezingatiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ina maoni na ushauri kuhusu sehemu ya 9 kifungu cha 63 (4) kinachotamka kuwa: “*No member of the committee shall serve for more than two consecutive terms,*” kwamba pia kirekebishwe.

Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba uongozi uwekewe utaratibu ili usiwe uongozi wa kukaa tu muda wote. Lakini vile vile uongozi unaondoka haraka haraka hauweki mwendelezo katika kuongoza.

Kwa hiyo, Kamati ilishauri kuwa Mjumbe wa Bodi aweze kugombea tena uongozi baada ya kumaliza kipindi kimoja cha miaka mitatu. Lakini kipindi kingine cha miaka mitatu awe mwanachama tu wa kawaida. Baada ya kukaa nje ya uongozi kwa muda wa miaka mitatu aweze kugombea tena uongozi. Kwa hiyo, katika muda wa miaka 12 atakuwa katika safu ya uongozi kwa muda wa miaka 9 na hapo ndiyo ukomo wa uongozi wake. Nadhani Mheshimiwa Waziri haya ndiyo ambayo tulikubaliana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni vizuri ikaeleweka vizuri ili kuweka uongozi endelevu au *continuity* katika Vyama vya Ushirika. Vile vile kuzuia watu wengine kukaa pale kwa muda mrefu kana kwamba ni machifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilizingatia umuhimu wa uongozi bora na endelevu katika Vyama vya Ushirika kwa hiyo tumekubaliana vizuri sana na Serikali, imekubali kuweka utaratibu huo ambao unalenga kabisa katika kutekeleza maudhui ya kuimarisha Vyama vya Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ina maoni na ushauri kuwa kifungu cha 81 (3) kinachotoa adhabu ambacho kwenye Muswada ilikuwa imewekwa kiwango cha shilingi 1,000 kwa siku kwa vyama vya ushirika kutokana na kutotekeleza maelekezo ya *charges for registration* kwamba kifungu hicho kabadilishwe na adhabu hiyo iwe shilingi 10,000 kwa siku. Kamati inaona kuwa kiwango hicho cha shilingi 1,000 kama kingeendelea kuna watu wachache ambao kutokana na uwezo wao wa kifedha wangeweza kuchukulia kiwango kidogo cha adhabu hiyo, kuwa siyo kitu chochote na hivyo kuendelea kufanya makosa ambayo yanakatazwa. Hata hivyo Kamati inaishukuru sana Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na kufanya mabadiliko kwenye kifungu hiki muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati inakubaliana na sehemu ya 14 kifungu 101 kinachompa Mrajisi mamlaka ya kumteua Mfilisi (*Liquidator*) wa mali za Chama cha Ushirika pamoja na kukagua shughuli za vyama na matumizi ya fedha kama inavyoonyeshwa kwenye sehemu ya 12 kifungu cha 61 (1).

Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa ili Maafisa Ushirika waweze kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi, Serikali iwapatie nyenzo za kufanyia kazi pamoja na mafunzo ili waweze kutekeleza jukumu hili ipasavyo.

Aidha, Kamati pia inapendekeza kuwa sehemu ya tatu kifungu cha 10 kwenye jedwali kinachoweka masharti ya mwanachama kuhudhuria mikutano mikuu miwili ya

mwisho ya chama hicho ndipo achaguliwe kuwa Mjumbe wa Bodi ya Uongozi kiondolewe kwa kuwa kila chama kina masharti ya Uanachama wake. Nadhani hili vile vile lilikuwa limezingatiwa na litazidi kudumisha demokrasia katika Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imechukua hatua kadhaa zinazolenga katika kupunguza na kuondoa kodi zinazowakera wananchi. Mojawapo ya hatu hizo ni kuunganisha kodi mbalimbali ili kumwondolewa mlipa kodi kero na usumbufu pamoja na kuweka ufanisi katika ulipaji kodi chache husika. Kwa mantiki hiyo, Kamati inapendekeza kuwa kodi mbalimbali zilizopendekezwa kwenye sehemu ya 16 kifungu 128 (1) viunganishwe ili kuletwa ufanisi wa ulipwaji wake na zile zilizopitwa na wakati zifutwe. Kamati inafurahi kuona kuwa Serikali vile vile imezingatia ushauri huu na kufanya mabadiliko katika kifungu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fedha zinazotolewa kwa wakulima chini ya Mfuko wa *STABEX* limeleta manung'uniko miongoni mwa wadau wa zao hilo kutokana na utaratibu wa matumizi yake kutokuwa wazi. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Serikali iweke jambo hili wazi kabisa kwa kuainisha kiasi cha fedha zilizotolewa chini ya utaratibu huo na namna zilizvyotumika au zitakavyotumika.

Tunaishauri Wizara ya Fedha iandike waraka wa maelezo ya matumizi ya fedha hizo na usambazwe kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wabunge ili wasaidie kutoa maelezo yasiyoleta utata. Suala hili limejitokeza kwa sababu kamati yangu inahusika na Wizara ya Ushirika na Masoko.

Kwa hiyo, haya ni baadhi ya matatizo ambayo yapo. Tunasema kwamba hakuna ambaye anapinga matumizi ya mfuko wa *STABEX* yaliyokubaliwa na Serikali kwa jinsi walivyokubaliana na wanaotoa *STABEX*. Lakini ni vizuri maelezo ya kina yatolewe kama hazina wanavyotoa kwenye magazeti kwamba fedha hizi zimetolewa sasa zitatumika kwa hoja moja, mbili, tatu, nne. Mimi naamini kabisa kwamba wakulima wa Tanzania ni watu wanaoelewa mambo wakitoa maelezo ya kutosha watakubali na kuungana na Serikali kwamba fedha hizo zitumike kama Mkataba ulioingia Serikali na wanaotoa *STABEX* hiyo. Tumelileta hili kwa sababu katika kuboresha Vyama vya Ushirika hii ni mojawapo ya kero ambazo ziko kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yanayoletwa na Muswada huu yanawahusu wanaushirika ambao wengi wako vijijini. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali kwamba kuwe na programu ya uhamasishaji na utoaji wa elimu ya ushirika kwa wananchi ili waelewe sheria yao hii vizuri na kusaidia kutekeleza maudhi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasisitiza hili kwa sababu Ushirika ndiyo utaratibu ambao unawezesha wananchi wa kawaida kuweza kuungana na kupata uwezo waweze kuingia katika shughuli za kiuchumi za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii sasa kumpongeza Waziri wa Ushirika na Masomo Mheshimiwa Balozi George Clement Kahama, pamoja na Naibu



Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa ushirikiano walioipa kamati yangu wakati wa kufikiria Muswada huu wa Sheria. Aidha, napenda kwa niaba ya kamati kuwapongeza watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Ladislaus Komba, kwa ushirikiano wao na umakini katika kujibu hoja za kamati. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Musa, pamoja na Katibu wa Kamati yetu Ndugu Daniel Eliufoo, kwa kuihudumia kamati hii ipasavyo wakati wa kutekeleza jukumu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hii hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AISHA P. MAGINA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani.

Awali ya yote ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliorejea baada ya kutumikia adhabu ya Bunge. Tunashukuru mmerejea tufanye kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kurejea katika kifungu cha 63 (2) cha Muswada huu kinachosema kwamba hakuna mjumbe wa Kamati ya utendaji atakayekaa au kuchaguliwa kwa vipindi zaidi ya viwili. Kambi ya Upinzani haioni tatizo kwa kifungu hiki. Sheria hii itaondoa mtindo wa kizamani ambapo watu walichaguliwa kuongoza ushirika wakafanya ni mali yao na hivyo kuzuia wana ushirika wengine wenye mawazo mapya kuongoza ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inahusu tu viongozi wa ushirika wa kuchaguliwa. Kwa sababu hiyo viongozi hao watalipwa posho tu ya uongozi kufuatana na taratibu walizojiwekea wanaushirika. Hivyo ni tegemeo letu kwamba wana ushirika waliochaguliwa kama wajumbe wa bodi ya utendaji hawatakuwa waajiriwa wa ushirika na hivyo hawatapata mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wa Bodi ya utendaji wanatakiwa kuwa ni waadilifu, hivyo kama itaonekana kama wana historia ya udanganyifu, ubadhirifu au wanakwenda kinyume na maadili ya kiushirika basi viongozi hao waondolewe katika uongozi. Hayo yapo kwenye kifungu cha 65 (1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mahali ambapo Mwenyekiti wa Ushirika anatumia ofisi kwa faida yake kwa kufanya biashara zinazofanana na ushirika anaouongoza na kutumia *facilities* za ushirika huo, hivyo kwa kuwa *competitor* wa ushirika huo. Sheria hii itaondoa mapungufu kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika una *management* ya utawala hii ni kada ya wataalam kama vile *General Manager, Chief Accountant* na wengine hawa ni watumishi wanaostahili kulipwa mishahara kwa mwezi na hivyo stahili zao za ajira zitatakiwa kuwa

wazi na hivyo ingekuwa ni bora wasije wakafikirika kuwa na wao wanatakiwa kuwa ofisini kwa kipindi kisichozidi miaka 6. Masharti ya Bodi na management nayo yana masharti kama yafuatayo:-

Moja uadilifu, pili wawe na wadhamini ili itokeapo mjumbe kusababisha hasara kwa ushirika aadhibiwe kwa sheria zilizopo na fidia ilipwe na yeye mwenyewe au mdhamini wake.

Katika kifungu cha 67 imetajwa kwamba Mrajisi wa Vyama vya Ushirika kwa kushauriana na Waziri na anaridhika kwamba haya yote ni kwa manufaa ya ushirika na umma unaweza ukavunja bodi ya utendaji ya ushirika na kuteua *care taker committee* ambayo itafanya shughuli zote za Chama cha Ushirika na kwamba baada ya muda mfupi wa siku 30 mrajisi ataitisha mkutano mkuu wa chama hicho ili waweze kuchagua kamati mpya ya utendaji. Jambo hili ni la maana kama kweli itakuwa hivyo.

Lakini sheria hii haizungumzii hali itakuwaje pale uongozi wa kiutawala unapokuwa umesimamishwa na kuletwa uongozi mpya kusimamia shughuli za kila siku za ushirika kama vile *General Manager na Chief Accountant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshatokea mara nyingi uongozi kama huu kuondolewa na Serikali na kupeleka watu wake kushughulikia jambo hilo. Tulitegemea kuwa sheria hiyo *register* anapoteua *General Manager* aweke *time frame* kwamba walioteuliwa watakaimu kwa muda na siyo kuwaacha tu indefinite rejea katika kesi ya *SHIRECU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 127 (2) kinasema iwapo mwakilishi wa mrajisi hatakubaliwa na hoja ya Kamati ya utendaji maamuzi hayo yatakuwa batili mpaka pale mrajisi atakapo *approve*. Huu ni uimara wa Kiserikali kwa namna hii hakuna sababu ya kamati ya kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona ni vema maamuzi ya wengi yaheshimiwe kama maamuzi hayampendezeshi mwakilishi wa mrajisi na mrajisi mwenyewe. Mrajisi na mwakilishi wake wajenge hoja ya kutetea na kuwashawishi wajumbe juu ya athari za uamuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 15 (2) na (4) kinasema kwamba mtu mwenye umri wa miaka 15 anaweza kuwa mwanachama katika ushirika isipokuwa hawezi kuwa katika kamati ya utendaji hadi afikishe umri wa miaka 18. Hii ina-*create awareness* ya ushirika kwa jamii. Hivyo tunaishauri Serikali ianzishe somo la ushirika kuanzia elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 kinachozungumzia madhumuni ya chama cha msingi yakiwemo kuboresha maisha ya wanachama wake ikiwa ni pamoja na kutoa huduma kwa wanachama wake kama kusindika na kuuza mazao ya wanachama. Jambo hili linaonekana kama vile chama cha msingi nacho kinaruhusiwa kuuza mazao yake bila kupitia chama cha kati au cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in practice* au kwa kupitia kanuni zitakazotengenezwa na Waziri, Chama cha Msingi hakiruhusiwi kuuza mazao yake kwa mtu yeyote atakayetaka kununua mazao hayo kwa bei ya juu kuliko ile inayotolewa na chama cha kati au juu au chama kikuu. Sisi Kambi ya Upinzani tunaona sasa ni wakati muafaka kwamba chama cha msingi kisizuiliwe kuuza mazao yake kwa yeyote atakayetoa bei nzuri zaidi ya ile inayotolewa na chama cha kati au cha juu. Chama cha msingi kiwe na uhuru wa kuuza mazao yao popote pale watakapoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwa kifupi Muswada huu.

Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu sasa ingawa imechelewa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mambo mazuri yote aliyoyazungumza ambayo yako ndani ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kwa jumla kwanza nchi yetu kwa kweli itapata maendeleo ya haraka zaidi kama Vyama vya Ushirika hasa vile vyaama vya msingi vikiimarishwa. Iwe jukumu la Serikali ijue kwamba sasa hivi wakati wa kuanzia mambo juu, yaende chini umekwisha. Wawahamasishe wananchi wenyewe na sasa hivi wananchi wako tayari na walishaungana na wako tayari kufufua vyama vyao vya ushirika ambavyo vilikufa miaka mingi iliyopita. Sisi tunaomba tu Serikali isaidie kuwawezesha wananchi hawa, kwanza tatizo lililoko sasa hivi ni ule uhaba Maafisa Ushirika kule Wilayani, kada hii imezorota sana maeneo mengi maafisa wa ushirika hawapo. Tunakwenda vijijini wananchi wanapiga kelele kila siku, tunataka kuanzisha chama cha msingi cha ushirika lakini wa kwenda kuwapa elimu hiyo hawapo.

Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, hiki akichukulie kitu cha kwanza. Vile vile nipongeze sana sheria hii kwa kuvitambua vikundi vya uzalishaji mali na uchumi, vikundi vya akina mama, vijana na walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndiyo vikundi ambavyo vinazalisha mali hapa nchini kwetu, hivi ndiyo vikundi ambavyo vimeungana na vinaleta maendeleo. Akina mama na vijana, tumeona mifano hela ndogo wanazopewa kutoka Serikalini, wanaungana wanafanya mambo ya ajabu sana. *(Makofi)*

Sasa hivi Dar es Salaam kuna Maonesho ya hawa akina juakali, vikundi vidogo vidogo ambavyo wanajitafutia wenyewe uwezo wa kuendeleza shughuli zao. Lakini ukienda kuona vitu wanavyofanya ni vitu vya ajabu na ni vizuri sana ambavyo vinaongeza Pato kwa Taifa hili. Mimi naomba Serikali isiishie kuvitambua tu bali ivipe uwezo iwaelekeze mahali ambapo wanaweza kupata mikopo ili waendeleze ushirika wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wako tayari kurudisha vyama hivi vya Ushirika kwa moyo mweupe kabisa, lakini wao watambuliwe kwamba ndiyo watakaovisimamia na kama wenzangu waliotangulia walishasema wapewe uwezo wa kuuza vitu wanavyotengeneza mahali popote wasiwekewe masharti. Hata wakipata soko kule nje wawezeshwe kupeleka vitu vyao. Hii itakuwa imetengeneza ajira na itakuwa imewaunganisha wakulima wetu. Tunajua nchi hii ya Tanzania ni ya wakulima na wafanyakazi. Kwenye wakulima kuna wafugaji, wavuvi nakadhalika. Hawa wote wahamasishwe kuanzisha Vyama vyao vya Ushirika na kama vilishaanza basi wapewe msukumo zaidi waweze kuendelea. Asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali hapa Bungeni, alisema sasa hivi kuna vyama 11 vya msingi ambavyo vimekomaa. Vyama 11 ni nini mbele ya Tanzania hii? Tunataka kila kijiji kiwe na chama cha ushirika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vyama vya kuweka na kukopa hata hivyo bado vingi havijaimarika na bado vingi havijafika vijijini. Hivi vikiwezesha na sheria hii ikivilinda kule, sasa hivi tumeona mfano wananchi wanakwenda Benki ya NMB wanakopa fedha zao 200,000/=, 300,000/= wanalima mwishoni mwa msimu anarudisha fedha. Lakini tukianzisha hivi vyama vya kuweka na kukopa vitawasaidia sana. Mifano iko hai ukienda kule Mbeya wameanzisha Benki Kata ambazo zinafanya kazi nzuri sana. Hayo yote ni mambo yanahusika na Ushirika.

Kwa hiyo, mimi ningeomba sheria hii isiishie kwenye vitabu, iishie kwenye utekelezaji. Tunaambiwa vyama vya wavuvi vimeongezeka kutoka 70 hadi 95. Tuna maziwa mengi, tuna mabwawa mengi, tuna bahari hivi vyama bado ni vichache sana. Hivi viko kwa sababu ni wale wenye uwezo lakini bado kuna wavuvi wengi maeneo yote ya Tanzania ambao wanataka waungane na kufanya uvuvi wao uendele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo kuongezeka kwa wanachama kutoka 500,000 hadi 750,000 bado ni ongezeko dogo ukilinganisha na idadi ya Watanzania tuliopo. Mimi nashauri Wizara ya Ushirika na Masoko iende kwa walengwa. Vile vile tukumbuke wananchi wetu hawajasahau matatizo waliyoyapata karibu kila Mkoa ulikuwa na Chama cha Ushirika, baadaye hivi vyama vikafutwa. Lakini wananchi walikuwa bado wanaidai Serikali fedha zao. Wananchi watajisikia vizuri zaidi kama yale madeni yao yatalipwa, watakuwa na moyo wa kujiunga na vyama hivyo. Sasa hivi kwa kweli moyo wanao, lakini watakuwa wanaishia kwa kufikiria kuwa hawa lengo lao ni kuja kutokopa kama kule nyuma.

Wananchi wa Mkoa wa Singida mpaka leo wanadai shilingi milioni 23,000,000/= kwa hiyo hii sheria mpya inayoanza isaidie na kufuta tofauti zilizopo kati ya vyama vya ushirika vilivyokuwa huko nyuma na vitakavyoanzishwa. Kwa sababu Serikali ndiyo mama wa Ushirika, ichukue haya madeni iwalipe wananchi wake.

Pia Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba kutakuwa na *Cooperative Reform Program* itaanzishwa. Hii ndiyo itatusaidia sana kuendeleza ushirika. *Local Government Reform* imefanya mambo mazuri sana kwa upande wa Halmashauri, Halmashauri zetu sasa zinaendelea, kwa hiyo tunaomba na hii *reform* ya ushirika iige mfano na itafanya

vizuri kama itakuwa na watu wenye moyo wa kufufua ushirika. Kama itakuwa na watu ambao watakubali kwenda kuishi na wavijiji waone wanataka nini. Tuna wakulima wazuri sana wa mazao yetu, tuna wafugaji wazuri wako kule vijijini wanaohitaji kupewa mwamko. Mimi nashukuru sana Sheria hii inawalinda na itawalinda na kuwawezesha wafanye mambo yao kwa faida yao na kwa faida ya maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge, ni lazima twende kule na Wizara ituwezeshe kuna mambo ambayo Mbunge anaweza kufikisha kirahisi zaidi kule kwenye vyama vya msingi. Tusiwategeme watendaji ambao ni wachache sana.

Kwa hiyo, Wizara itutumie sisi kueneza sheria hii mpya kusaidia wananchi wetu waweze kuanzisha vyama vilivyo imara. Vile vile Wizara bado inaitwa Wizara ya Ushirika na Masoko lakini mazao ya wananchi hayana mahali pa kuuza. Washirikiane na nchi mbalimbali na wadau wengine ili wananchi wote waweze kuuza yale wanayouza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie hapa nirudie kusema kwamba naiunga mkono hii sheria mpya kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote niseme kwamba leo katika kipindi hiki ni siku yangu ya kwanza kuongea na inawezekana kabisa nilikuwa na matatizo mengine.

Jambo la kwanza ambalo kabla sijarejea kwenye Muswada wenyewe, nilitaka tu niwapongeze watu wa Chama cha Mapinduzi kwa kusaidia *UDP* kutoboa jipu ambalo lilikuwa limekaa pabaya na nawapeni hongera na pia niwaambieni kwamba karibuni katika uchaguzi huo utakaokuja uwe wa kidemokrasia. Kama itakuwa ni matumizi ya nguvu kama inavyoandikwa kwenye magazeti, basi wawe *ready for any eventuality*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee sasa katika Muswada. Muswada huu natumaini ulikuwa unangojewa kwa muda mrefu sana. Tulijaribu mwaka 1997 ikatokea siasa humu, wakasema hapana hawa watu walitakiwa wakae *two terms*, ikatokea siasa kwamba mtavuruga demokrasia. Tukarudi pale pale, tukawaendeleza wale watu wakaendelea kukaa katika vile viti, wakajijengea umungu mtu. Leo sheria hii imekuja, sasa lazima tuitekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo. Tatizo lililopo ni kwamba uanzishwaji wa Ushirika uliopo kama utaendelea jinsi ulivyo, hatutajenga Ushirika. Nataka Ushirika uwe Ushirika wa kuanzia kwenye *primary* kwenda juu, siyo kutoka juu kuteremka chini kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Msindai. Kwa muda mrefu sana tumekuwa na hiyo tabia, tuna-*impose* Ushirika wa aina gani? Tuache watu wawe huru kule kwenye *grassroots* wajiandalie Ushirika wao na waamue jinsi wanavyoona wenyewe na wasimamiane wao wenyewe. Wanafahamiana hawa watu. wanafahamiana, ukimuingiza fulani pale kwenye Ushirika wenu atavuruga. Sasa hawa watu tuwaache wawe na uhuru wao wa kuandaa ushirika wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja hapo kimetajwa, Kamati *to serve two terms*. Ni kweli kwamba ukikaa miaka mitatu, kuna uchaguzi mwingine na mitatu vile vile kuna uchaguzi mwingine. Lakini kuna tabia hii ambayo ipo kwamba wale ambao wako kwenye Ushirika wamejiingea himaya na ni marafiki wale wale wanakaa kwenye Ushirika. Hii sheria haizungumzi moja kwa moja kwamba zile *two terms* lazima ile *Board* nzima iondoke, tutabakiwa na watu wale wale wanaojibadilisha tu. Aliyekuwa Mwenyekiti ana-*step down* anakuwa Mjumbe wa Bodi, aliyekuwa Makamu wake anakuwa Mwenyekiti. Ni watu wale wale!

Mimi nilifikiri ingetajwa moja kwa moja kwamba wale waliokuwa kwenye Bodi ikishatimia *two terms* waondoke.

Mheshimiwa Waziri pale anajua kabisa jinsi sisi Shinyanga pale tulivyokuwa na matatizo. Ni matatizo makubwa kweli, watu wanajenga umungu. Ni wale wale! Leo mwingine atasema leo huyu simtaki. Anaitisha Kamati anapangua hawa, anaweka wengine, sura ni zile zile na za mazoea yale yale. Natumaini sasa ni wakati muafaka kabisa Mheshimiwa Waziri kwamba hata utakapokuwa unatunga kanuni, utunge kanuni zinazosema kama wewe ulikuwa katika Bodi ya *Management*, vipindi vyako viwili vikishapita, basi *hack off* waachie watu wengine waje wenye mawazo mapya na Ushirika mpya uweze kujengeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine hapa kinaitwa Mwakilishi wa Mrajisi. Huyu Mwakilishi wa Mrajisi anakaribishwa kwenye Kamati ya utendaji na pale wanaweza wakazungumza mambo wakakuliana yafanyike. Lakini kama yeye hayatampendezesha, akiyakataa, basi yale maamuzi ya Kamati ni *null and void*, mpaka pale Mheshimiwa Waziri atakapo-*approve otherwise*.

Sasa nilikuwa nafikiria kwamba maamuzi ya wengi ndiyo demokrasia hiyo. Inawezekana hayatakupendeza, kama hayatakupendeza lakini wengi wameamua yafanyike vile, basi uache uamuzi wa wengi utimilike lakini Mrajisi na yule mwakilishi wake wao wakae na wajenge hoja ya kwenda kuwashawishi wale Wajumbe wengine kwamba hiyo hoja waliyoipitisha haifai kwa msingi moja, mbili tatu. Hawa ni wanadamu, mimi naamini kabisa watakuwa wamekubaliana namna gani waweze kurekebisha hiyo hali. Lakini la kusema kwamba mwakilishi asipopendezeshwa na jambo ndani ya hiyo Kamati, basi hayo maamuzi hayafai, mimi naona huu ni uimla wa kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumziwa juu ya uhuru ya uandikishaji wa ushirika. Lakini uhuru wa Vyama vya Ushirika hasa vya msingi, kwa muda mrefu sana umekuwa umebanwa na kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri anatunga. Mara nyingi anatunga kanuni kwamba Vyama vya Msingi havitaruhusiwa kuuza mazao yao au chochote kile bila kupitishia Chama cha kati au Chama cha juu.

Mimi naona hapa kufanya hivyo ni kuzuia ule uhuru wa watu kushirikiana na watu kuanzisha Ushirika wao wa msingi. Hivi Vyama vya Msingi vinatofautiana na madhumuni yako tofauti na ni watu wa aina moja, wamefikiria jambo moja,

wamekubaliana kwa misingi ya aina moja, kwa hiyo, tuache wawe na uhuru wa kuchagua wafanye nini na mazao yao. Tumesema hivyo kwa sababu zao kama la pamba na leo ni biashara huria, watu wa *Primary Society* pale wakikusanya wakakubaliana kukusanya pamba yao kwenye sehemu moja na akaja *say Vilian Kagel* na mtu mwingine ambaye ana bei nzuri zaidi zaidi ya Ushirika ambao umezungumzwa na Serikali basi watu wapewe uhuru wa kuuza kule kwa sababu kuna *a better price*.

Mimi nafikiria hili Mheshimiwa Waziri katika kanuni zake atakapokuwa anatunga awaachie wanaushirika katika hiyo misingi waweze kuuza mazao yao pale wanapofikiria na wakati mwingine si ajabu wakaweza kupata soko la nje kule, kahawa ya Bukoba ikauzwa sehemu nyingine ambako kuna *a better price* na *Primary Society*, hawa watu watapata bei nzuri na wale Wanachama wao wataweza kuneemeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika vifungu fulani fulani humu ndani ya Sheria hii amezungumza kwamba watu wote ambao hawajafikia umri wa miaka 18, wanaweza wakajiunga na Ushirika na kwamba hawataweza kuwa ndani ya Kamati na wale waliopo kwenye shule, hakutaja ni shule za namna gani, sidhani kama ni *Primary*, natumaini anazungumza *Secondary Schools* kwamba na kule wanaweza kujiunga na Ushirika.

Mimi nakubaliana na hili kwamba linajenga moyo au uelewa wa Ushirika wa watu wetu wakiwa chini. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani lingekuwa ni jambo la msingi kwamba Elimu ya Ushirika iende mpaka *Secondary Schools*. Watu watakaomaliza *Secondary Schools* wanajua Ushirika ni nini. Wanaweza wakatoka pale wakaenda kujitengenezea Ushirika wao wakajitengenezea ajira zao na *take into consideration* kwamba ajira sasa ni ngumu hawa watu wakitoka pale watatengeneza Ushirika wao na hivyo watakuwa wanaushirika hasa ambao wanaelewa wanataka kufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nasema ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Ushirika iliyopo mbele yetu. Kwanza labda nikiri tu kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mheshimiwa William Shellukindo na nilishiriki katika kuupitisha Muswada huu na kimsingi ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sihitaji kufafanua umuhimu wa ushirika katika mpango mzima wa kujaribu kukuza ama kufufua uchumi wa nchi yetu, lakini labda tu ningependa kuainisha masuala kadhaa ambayo ningemwomba Mheshimiwa Waziri, masuala ambayo nitaainisha yatakuwa ni ziada ya yale ambayo tulizungumza kwenye Kamati, kumwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wayaangalie na watilie mkazo waone namna ambavyo wanaweza kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wasiwasi wangu uko kidogo tu katika *role* ya Halmashauri za Wilaya katika masuala ya Ushirika. Huo ndiyo wasiwasi wangu

mkubwa, kwamba pamoja na nia njema sana ya Serikali kujaribu kuacha uhuru mkubwa wa mawazo na maamuzi kwa Vyama vyenyewe vya Ushirika, lakini bado lazima tuweze kuchukua *a fallback position* kama *a safety gauge* kwamba pale panapokuwa pana tatizo la msingi, basi ni lazima Halmashauri ya Wilaya iweze kuingilia ama ku-intervene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Muswada wa sheria ambao tutaupitisha hapa leo, ukurasa wa 14(7) na ukurasa wa 13(2) inaonesha kwamba Mheshimiwa Waziri anaweza aka-delegate na hiki kifungu kidogo cha 2(a) na (b) kinasema, naomba ninukuu: *“The Minister may make consultation with the Minister responsible for Regional Administration or Local Government as the case may be in carrying out some of its responsibilities.”*

Sasa hapa ni kwamba Waziri anaweza akashauriana na Mheshimiwa Waziri mwenzake, lakini bado sheria haijaleza *specifically* kwamba Halmashauri ambazo ziko chini ya huyu Waziri wa *Local Government* zina *say* yoyote katika masuala ya ushirika. Katika kifungu kidogo cha (d) wanasema: *“The Minister may (ni may wala siyo shall) delegate some of its power in writing to a Regional Commissioner or Regional Commissioners for specific matters relating to Cooperative Societies.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo mimi sina tatizo na hili. Ila tu ninakuwa na wasiwasi kwamba tukija kwa Mkoa kama wa Kilimanjaro ambao una Vijiji zaidi ya 800 na kila Kijiji *literally* kina Chama cha Msingi cha Ushirika halafu Mkuu wa Mkoa ndiye anayepewa Mamlaka na kama tunavyojua, msingi wa sheria ni kwamba *power* ikishakuwa *delegated* huwezi na wewe uka-*subdelegate* tena. Kwa hiyo, kwa maana hii ni kwamba tunampa Mkuu wa Mkoa majukumu mazito mno ya kuweza kuwa msimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa mamia katika kila Mkoa. Mimi nafikiri katika misingi kama hii ufanisi wa utendaji kazi unaweza ukawa una matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, Sheria Na.6 ya mwaka 1997 inayozungumzia masuala ya *Regional Administration* inampa Mkuu wa Mkoa *role* ya kuwa zaidi *facilitator* kuliko *executive* na masuala yote ya utendaji yamerudishwa katika Halmashauri za Wilaya. Sasa hapa kuna kitu kinanichanganya kidogo ambapo labda ningeomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi baadaye. Kama Maofisa wa Ushirika wako chini ya Halmashauri halafu Mkurugenzi wa Halmashauri au Baraza la Madiwani la Halmashauri halina mamlaka juu ya huyu mtu ambaye naye analipwa na Halmashauri, kidogo mimi linanitiza.

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri pamoja na kutupa majibu mazuri, aangalie uwezekano hata kwa kupitia kanuni, inawezekana vipi Mamlaka ya Halmashauri za Wilaya ambapo ndiyo huku Vyama vya Ushirika vya msingi vipo, Mamlaka hii inajihusisha vipi na inahusishwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakiri kwamba sisi Wabunge ni sehemu za Halmashauri zetu za Wilaya na sisi ni Madiwani kwa misingi ya sheria, kwa hiyo tunashiriki katika Vikao vya Halmashauri za Wilaya na pengine ndiyo mahali mahususi



ambapo tungeweza vile vile kushiriki katika kuchangia hoja mbalimbali za Ushirika. Kwa sababu Ushirika na sheria yenyewe ya Ushirika imejaribu sana kulinda wale wanaushirika wenyewe. Kwa hiyo, labda ningepomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kidogo kwenye hili.

Lakini labda vile vile nizungumzie wasiwasi wangu kuhusu hizi *cooperative principles* ambazo zimeainishwa kwenye ukurasa wa 79 kama msingi mmojawapo uliotumika katika kutunga sheria hii mpya kwamba kuna *cooperative principles* ambazo nasema katika *schedule Na.79 Part II - General Provisions; "Cooperative Societies shall be managed according to the ICA cooperative principles which are..."* Sasa kuna moja ambayo inazungumzia *autonomy and independence*, ndiyo hilo swali nilikuwa nazungumzia kwamba kweli sheria imejaribu kutoa mamlaka makubwa sana kwa wanaushirika wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni lazima tukumbuke kwamba Sheria nyingine za Kimataifa tunapokuwa tunaziingiza katika nchi yetu, tujue na watu wetu wana *integrity* kiasi gani, tujue *morals* katika *Society* yetu iko kiasi gani. Tunaweza tukawa tuna nia njema sana lakini baadhi ya watu waka-*take advantage* ya upungufu uliopo na uhuru waliopewa wakautumia vibaya. Tuna uzoefu kwamba Vyama vya Msingi vya Ushirika katika miaka ya karibuni vimekuwa na madaraka makubwa ambapo viongozi wengi wa Serikali wameshindwa kuwaingilia wanachama wa Vyama vya Msingi vya Ushirika kwa sababu sheria ilikuwa inawalinda na ni vyema sheria ikaendelea kuwalinda lakini mimi bado naonya lazima tuweke *fallback position* ambayo iko *clearly defined*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie kidogo kuhusu masuala ya Ushirika katika Jimbo langu la Hai. Sisi katika Jimbo letu la Hai au Wilaya yetu nzima ya Hai, *literally* tuna Vyama vya Msingi vya Ushirika katika kila Kijiji. Unapozungumza Chama cha Ushirika au Chama cha Msingi cha Ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro, kimsingi lazima unazungumzia suala la ardhi na lazima uzungumzie suala la kahawa. Hii ndiyo roho ya Ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro na hakuna ubishi kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili unakuta wananchi ambao ni wengi, kwa sababu kimsingi Chama cha Ushirika kimepewa *role* ya ku-*operate* katika mazingira fulani ya Kijiji kwamba ile *geographical area* ya Kijiji ndiyo eneo ambalo Chama cha Msingi kinafanya shughuli zake. Sasa kwa kule kwetu Hai au Kilimanjaro katika ujumla wake, ardhi ni tatizo la msingi sana.

Kwa hiyo, vijana wengi ambao wana umri wa miaka 40 kurudi chini, wengi wao hawana ardhi kabisa hata robo heka. Wakati huo huo katika maeneo mengi ya Kilimanjaro kuna mashamba makubwa sana yalitaifishwa ambayo yalikuwa ya Wazungu zamani, baadaye yakakabidhiwa kwenye Vijiji, hatimaye sheria ilivyobadilika tena yakarudishwa kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika. Sasa haya mashamba kwa maelekezo ya Serikali na Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo haya, yamebinafishwa, ama yamekodishwa kwa wawekezaji mbalimbali wa nje na ndani.

Mimi nafikiri huu ulikuwa ni mpango mzuri tu wa Serikali ambapo waliona ni muhimu haya mashamba yapewe teknolojia inayostahili na wapewe watu ambao wana uwezo wa mtaji ili waendeleze ikiwa ni pamoja na juhudi la kufufua zao la kahawa. Mimi hapa sina tatizo kabisa na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo langu ambalo ningemwomba vile vile Waziri aliangalie kwa makini sana, namwomba Waziri wa Ushirika kwa sababu ndiyo wenye mashamba haya, aone tatizo la ardhi Kilimanjaro kama tatizo la Zimbabwe ambapo kama halikutafutiwa ufumbuzi ambao utakuwa wa busara, katika siku za usoni linaweza likasababisha machafuko makubwa na umwagaji mkubwa wa damu.

Haya mashamba yamekodishwa na yana mapato makubwa sana. Vyama vya Ushirika vya msingi katika Wilaya yetu ya Hai kwa ujumla wake vina mapato makubwa kuliko mapato ya ndani ya Halmashauri. Sasa hali kama hii ingesaidia basi kama mapato haya ambayo yanatokana na Vyama vya Msingi vya Ushirika yangukuwa yameelekezwa moja kwa moja katika maendeleo ya wananchi wote katika maeneo ya Vijiji ambavyo hivi Vyama vya Msingi vya Ushirika vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi la kuelewa hapa ni kwamba, sizungumzii kwamba Halmashauri ama Mamlaka zozote za Kiserikali ziingilie shughuli za utendaji za Vyama vya Msingi vya Ushirika, hapana. Lakini nazungumzia kuhusu haya mashamba ambayo yalikuwa ni mashamba ya wananchi. Yalikuwa ni mashamba ya Vijiji yakakabidhiwa yakapewa milki yake kwa Vyama vya Msingi vya Ushirika. Haya mashamba yanawapatia Vyama hivi vya Msingi vya Ushirika mapato, vingine zaidi ya milioni 30 kila mwaka. Katika ujumla wake yako mashamba zaidi ya 30 na mapato yake ni makubwa mno kwa mwaka. Lakini ukiangalia kazi za maendeleo ya wananchi zinazofanyika kutokana na mapato haya ni kidogo sana na ndiyo sababu nikasema haziwiani na idadi ya mapato ambayo hivi Vyama vinakusanya.

Wanachama wa Vyama hivi hawa-*constitute* hata asilimia tano ya idadi ya wananchi katika Wilaya nzima. Lakini kwa sababu wao ni wanachama na wana milki ya mali ya Chama cha Msingi, basi wana ardhi maekari kwa maelfu.

Ningeomba sana Serikali iliangalie hili, mashamba haya yabaki kwa wawekezaji, lakini milki ambayo ilichukuliwa.... Maana yake mashamba kwanza yalichukuliwa kwa wawekezaji Wazungu zamani yakaletwa Vijijini, baada ya Sheria ya Ushirika kubadilishwa yakachukuliwa tena Vijijini yakarudishwa tena kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika. Sasa huku kuna watu wajanja, baadhi yao ni waaminifu, lakini wengi wao kwa kweli wanastahili kushughulikiwa na kudhibitiwa. *Otherwise* malalamiko ya wananchi ni mengi, kuna mashtaka mengi sana katika Halmashauri ambayo kutokana na upungufu wa sheria tulishindwa kuyashughulikia, kuna matatizo mengi sana ambayo tayari yako katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika Mkuu wa Wilaya, wana Ushirika wamepigana katika maeneo kadhaa, nikitoa mfano wa Chama cha Msingi cha Sonu Ngira ambapo wanachama wamepigana mpaka gari ya Polisi ilivunjwa na mawe pale. Lakini kuna Ofisa wa Ushirika wa Halmashauri ambaye kimsingi Halmashauri haina uwezo wa kumdhibiti kwa sababu sheria inaizuia.

Kwa hiyo, ningepomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na ningepomba alipe kipaumbele sana wakati anatunga kanuni zake aone je, Serikali inaweza kufanya nini kunusuru hali hii? Tunataka yale mashamba yaendelezwe, sawa, tunataka yapate wawekezaji, lakini tunataka mapato yanayopatikana kwa mashamba haya yatumike kwa faida ya wananchi wote hasa tuki-*consider* kwamba Hai ni eneo la Vijijini na huku Vijijini wananchi hawana ardhi.

Kwa hiyo, siyo rahisi wao kuwa wakulima na kuwa wanachama katika Vyama vya Msingi ambavyo ni vya wakulima. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa kweli na kwa kupitia Waziri ilichukulie hili suala kama suala la msingi sana katika kuleta maendeleo na ufufuaji wa zao zima la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wenzake wote katika Wizara kwa kweli kwa sheria hii. Niombe tu hayo machache niliyoyazungumza aweze kuona namna ambavyo anaweza akashirikisha na ili vile vile ieleweke hata kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba kwa kweli kwa upande wa Kilimanjaro Vyama vya Msingi vya Ushirika tayari vipo, tatizo la msingi ni kuviimarisha na tatizo kubwa la kuviimarisha linalojitokeza ni viongozi kushindwa kudhibitiwa na Mamlaka kadhaa zikiwemo Mamlaka za Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyazungumza hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Ushirika na Masoko kuhusu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa mwaka 2003.

Kabla ya mchango wangu napenda kutoa rambirambi zangu na za Jimbo langu la Arumeru Mashariki kwa wote waliofikwa na vifo vya ajali za magari kule Arusha. Pia natoa rambirambi zangu kwa aliyekuwa Meya wa Mji wa Arusha, Bwana Kivuyo. Mungu aziweke pema Peponi roho za Marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti,....

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Samahani, Waheshimiwa Wabunge, nimekatiza kidogo. Tunaongea juu ya Muswada, tukitaja kifungu cha Muswada huu, cha Muswada huu, bado haijawa sheria. Naomba hivyo kwa sababu nimeona wengi siyo mtu mmoja toka asubuhi tunapochangia, baadhi yetu tunajisahau tunasema sheria hii. Huu ni Muswada lakini bado haijawa sheria. Nimesikia kwa wengi, siyo mtu mmoja. Ni Muswada, tunaongelea Muswada. Kama ni kifungu unatoa kifungu halafu baadaye itakuwa sheria baada ya Rais kusaini.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Muswada wa Sheria.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Siyo wewe peke yako, nilikuwa naweka sawa kwa wengine pia. Ahsante.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa niendeleo kuhusu Muswada huu....

*(Hapa kengele ililia)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** kengele hiyo haikuhusu. Ilikuwa ya Mheshimiwa Freeman Mbowe, alituachia nafasi hiyo. *(Kicheko)*

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Lakini nikimalizia muda wake siyo mbaya pia. Mimi nadhani Muswada huu ni muhimu na ni sehemu muhimu ya juhudi za Wizara kufufua na kuboresha Ushirika. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu nzima ya Wizara ya Ushirika na Masoko ikiongozwa na Katibu wake Mkuu.

Naomba kwa niaba ya Wakazi wa Arumeru Mashariki, nitoe shukrani za pekee sana kwa Waziri, Mheshimiwa Clement George Kahama na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa kauli ya Wizara wakati wa Bunge la Bajeti kuhusu soko la Tengeru kwamba litajengwa. Naomba nifikishe shukrani za wana Arumeru Mashariki na pongezi zao kwa hawa Waheshimiwa na Wizara kwa ujumla na Serikali kwa ujumla kwa kauli hii na wana ari kubwa ya kuona ujenzi wa Soko la Tengeru unaanza. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Kwenye Muswada huu, *role* ya Serikali na ya Waziri katika kuwezesha Ushirika kuendelea kiuchumi na kijamii yamewekwa bayana. Katika sehemu ya pili ya huu Muswada, ule ukurasa wa 12, ibara ya tano, sita na saba ndizo ambazo zinatoa bayana hizi *role* za Serikali na Wizara.

Napenda kujizamisha kidogo kwenye hizo *role* za Serikali na *role* ya Waziri. Niende kwenye ibara ya sita inayozungumziwa *role* ya Waziri. *“The Minister shall take measures,”* iko katika ukurasa wa 12. Ie sehemu A, *“Improving the economic situation of their members,”* naomba nijizamie kidogo kwenye hilo kwamba kwa hali ilivyo sasa hivi na hapa nazungumzia kuhusu hasa Jimbo langu la Arumeru Mashariki na nina imani inahusu pia wakulima wa zao la Kahawa kwa ujumla, hali ya wanaushirika ni mbaya hasa wale ambao walikuwa wanaotegemea zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *role* ya Waziri ni ku-improve hii *economic situation* yao. Nitoe hali halisi ilivyo kwenye Jimbo langu kwamba kuna madeni ambayo wananchi washirika katika Vyama vya Ushirika wanadai kwa miaka karibu zaidi ya kumi au ishirini sasa hivi. Wakulima wa kahawa waliletewa mpango wa kuchangisha fedha ziwekwe kwenye mfuko maalum wakawekewa kwenye vitabu kama vile vya Posta au Benki ili hizo fedha zitumike kununulia mazao yao na kupunguza gharama ya kwenda kukopa kutoka Benki. Wananchi wakawa wanakutwa hela yao kutoka kwenye mauzo ya kahawa yao. Waliendelea kukatwa kwa muda mrefu mpaka sasa wakati ambapo

Ushirika unaonekana kwamba umeshindwa na kuelekea kufilisika tumekata tamaa kwamba huenda hizo hela hazitalipwa tena.

Tumejaribu kupitia vyama Vikuu vinavyoitwa *Secondary* au *Apex Cooperative Societies*, lakini nao pia wamefilisika au kwa taarifa kamili *in fact* kutoka kwenye Wizara kamili ni kwamba Vyama Vikuu husika ukichukua mali zao zote ukazitathmini zote gharama yao au *value* yake haiwezi kutulipa madeni ambayo inadaiwa na wananchi ambao ni wanaushirika waliochukuliwa hela zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu kupitia Bunge lako Tukufu, kuomba wapate msaada na sasa hivi aliyetangulia Mheshimiwa Msindai amepeleka ombi kama hilo kwamba pamoja na sheria hii kutuwezesha ili turudi kwenye hali ambayo ni ya Ushirika tunayotaka, inawezekana hao wananchi hali yao ya kiuchumi ikaboreshwa kwa kurudishiwa hela zao ambazo ni haki yao ilikatwa kwenye jasho lao na wao walidhania kwamba Serikali yao ingewaonea huruma ishirikiane na Ushirika waone ni jinsi gani wananchi wanaweza wakarudishiwa fedha zao zilizokatwa kwenye mazao yao.

Katika taarifa ya tathmini ya hesabu ya *Audit Report* ya Benki Kuu ya mwaka 2000/2001,/2002/2003 kuna sehemu inayoonyesha ya kwamba Benki Kuu imekuwa ina fedha za *STABEX* mwaka wa 1991,1992, nadhani kwa miaka karibu minne zile hela zimelala pale.

Tunakumbuka vizuri sana jinsi ambavyo hili suala la *STABEX* lilileta mvutano hapa Bungeni, lakini kwenye vitabu vya Benki Kuu inaonyesha kwamba zilikuwepo na zimekuwepo fedha za *STABEX* na imani yetu ni kwamba fedha *STABEX* zimekuwepo kwa ajili ya hao wananchi. Tuongeele tu kwa Wizara, kwamba pamoja na kutekeleza huu Muswada utakapokuwa Sheria na hasa hicho kipengele (a) cha ibara ya 6, tunaomba hiyo hela ikatazamwe kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Benki Kuu, ni fedha zipi hizo na ni zipi ambavyo sisi wananchi tunaweza tukafaidi wale ambao tulikatwa hela yetu na kuna madeni ambayo hatujaweza kulipwa kwa muda mrefu kupitia vyama vya ushirika.

Pendekezo langu ni kwamba ionekane, utafutwe uwezekano wa kuanzisha *ka-fund*, *ka-fund* kidogo kwa ajili ya ku-*address Co-operative Bank* ambazo zipo *directly* kwa wakulima. Ikiwa ni pamoja na kutumia *funds* ambazo zimekuwa *hanging* na ambazo hazifahamiki mahali ambapo zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ile ibara ya 7 ukurasa wa 13 kifungu cha kwanza ile (a) pale, kwamba (a) na (b) hapo lengo langu kwa kweli ni kushukuru Serikali. Tunafahamu kwamba *export credit guarantee scheme* imeshaanzishwa na Serikali, tunaipongeza Serikali kwa hili. Lakini tunaomba katika utekelezaji wake itazamwe kwa *scope* ya kwenda chini zaidi. Vyama vya ushirika karibu kila kijijiji kinakuwa *operated society*. Kwenye eneo langu kahawa wameanzisha pia kwenye vikundi vikundi na hivyo vikundi kwenye sheria hii inavyowekwa kufuatana na ibara ya 4 ukurasa wa 11 inakuwa *recognized* kama *Co-operative Society* au Sheria hii inawathamini. Ni vipi vikundi vidogo vidogo vinavyotaka kuboresha zao lao na hasa zao

la kahawa na ambao wanataka kuuza moja kwa moja lakini bila kufikia *Co-operative Society* ambazo zipo sasa hivi, ni zipi hizo, hivyo vikundi vinaweza kufaidi *export guarantee* ni pamoja na facilities zingine za *financial facilitation* wanaweza wakafaidi nazo ili waweze kupata bei kubwa ya mazao yao ambayo wanayafanyia kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukurasa ule wa kumi na nne na ile ibara ya saba inaendelea. Kifungu namba 3 ambacho kinazungumza kwamba, *the minister may direct co-operative college to teach, conduct research and other consultant services.*

Mimi hapo shida yangu kwenye ibara ni hilo neno *direct*. *The Minister may direct*, mimi hapa kidogo inanipa wasiwasi na nitaomba kufafanuliwa, kwamba *co-operative college* itakuwa *ina-associate university* na natazamia kwamba kwa *operative college* itakuwa *autonomy* na itakuwa na *Board* au *instruments* za kuiwezesha katika *decision making* na hasa zile ambazo zinahusu *academic work* na *profession work*. Nilidhania wao wangeruhusiwa ile *autonomy* yao bila kupata *direction* kwa aina hii tena ya kisheria kutoka kwa Waziri. Nina imani kabisa kabisa Mheshimiwa Waziri wetu aliyepo sasa hivi hatakuwa na tatizo kabisa. Lakini hatujui kuifanya sheria hii iwe inatoa *direction* kwa hiki chuo. Mimi nadhani tunakidhalilisha. Nadhani kiruhusiwe kipate, kitumie haki yake ya kuwa *autonomy* katika masuala ya kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu hii inavyozungumza vyama vya ushirika ambavyo viko tayari vinafilisika na vimeamua kuji-*declare* kwamba kuwa wamefilisika na kuna mifano mingi na mimi nina mmoja katika jimbo langu. Lakini ninavyozungumzia huu ufilisi pamoja na *disposal* ya *assets* zao ikiwa ni pamoja na *real property* mimi inanitia wasiwasi, kwa jinsi ambavyo inafanyika sasa hivi na *role* ya *registrar* mimi inanipa wasiwasi kidogo.

Ombi langu hapa ni kwamba tuone ni vipi katika utekelezaji angalau hata kama sasa hivi hali itawezekana, inaweza ikaboreshwa huu Muswada ukaboreshwa ili iweze kufanya ufilisi uwe smooth kuliko ulivyo sasa hivi na *role* ya *registrar* iainishwe waziwazi kwamba kazi ya *registrar* na Mahakama ni wapi ambapo wana-*inter link* na ni wapi ambapo wana-*interface*. Mimi nakuwa na matatizo na hilo na hasa nalizungumzia hilo kwa sababu nina tatizo sasa hivi jimboni kwangu ambako hilo suala lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia Muswada muhimu uliyo mbele yetu. Naomba nianze nami kwa kuwapongeza Wizara pamoja na Wataalam kwa kuandaa Muswada ambao kwa sehemu kubwa utakidhi kiu ya wanaushirika na kwa kweli tulitarajia Muswada huu uje mapema, lakini kwa sababu umekuja basi pamoja na kuchelewa tunawapongeza kwamba walau wameweza kuwasilisha katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea mambo mawili. La kwanza niliongelee kwa ufupi. Kwa sababu vikao vilivyotangulia nilishaliongelea kwa kina. Ni kuhusu jinsi Muswada huu utakavyotusaidia kupambana na ubadhirifu uliokuwa ukijitokeza katika

vyama vya ushirika. Kuna maeneo matatu ambayo ukiyatazama yanaonyesha nia ya Serikali kweli kweli kwamba sasa ubadhirifu utaangaliwa kwa kina. Kwa mfano, kifungu cha 93 kinachoongelea *surcharge* na kinaeleza wazi wazi kwamba ubadhirifu sio tu kudokoa fedha vile vile ni pamoja na kufanya maamuzi ya ovyo ovyo na yanayoonyesha uzembe wa makusudi.

Lakini nilichokifurahia katika Muswada huu wanasema *registrar* atakuwa na uwezo wa kushughulikia wale waliopita, au waliopo. Ni matarajio yangu sasa tukishapitisha Muswada huu na *registrar* akipatikana apitie vyama vya ushirika vyote na aweze kubaini ubadhirifu uliojitokeza na basi atumie kifungu hicho kuweza kupata kile ambacho sisi tunaopongeza Muswada huu kwamba utatusaidia kuelekea huko. (*Makofi*)

Ukiangalia *clause* ya 124 inaeleza kwamba *direct or Director of public prosecution* ata-*appoint prosecutors* ambao warasaidia kuendesha kwa kasi kesi zinazohusisha masuala ya ushirika. Sasa swala hili limekuwa likipigiwa kelele muda mrefu na majibu ya Serikali mara nyingi yamekuwa kwamba kesi zinaendelea lakini zinaenda taratibu. Sasa nadhani labda hii itatusaidia kuweza kuzipeleka kesi hizo kwa kasi, ingawa kwa kweli mimi binafsi sielewi vizuri jambo lipi litatendeka vipi.

Sasa kama Bunge ambalo ndilo linatunga sheria nitamwomba sasa Mheshimiwa Waziri anifafanulie vizuri nilielewe nisije nikatunga sheria ambayo nikitoka nje nikaulizwa umetunga nini, naanza kusema sijui nilichopitisha. Sasa nitamwomba Mheshimiwa Waziri anieleweshe vizuri ili nielewe hao *Prosecutors* ambao watateuliwa na *Director of Public Prosecutions* ni akina nani na wataweza kufanya kazi lini kwa haraka ili iwe tofauti na utaratibu uliopo.

Kwa sababu unaweza ukafanya jambo unafikiri sasa ndiyo itasaidia, kumbe ndiyo kwanza sasa unarudi hatua 100 nyuma. Ndiyo maana namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kunifafanulia kipengele hiki ili niweze kukielewa vizuri.

Swala lingine linaloonyesha kwamba Muswada utatusaidia kupambana na ubadhirifu ni kwenye nyongeza ambapo imeelezwa wazi wazi kwamba wale wote watakaokuwa Maafisa kwenye Ushirika watafanyiwa *vetting*. Lakini ambacho ningependa Mheshimiwa Waziri atusaidie kunifafanulia ni kwa nini amesema watakaofanyiwa *vetting* ni wale tu walio kwenye *Secondary Society* na *Upper Society*.

Mimi ninavyofahamu ubadhirifu hauko tu kwenye vyama vya ushirika vya union pamoja na *federation* na *Apex* bali upo vile vile kwenye vyama vya msingi. Sasa unapofanya *vetting* kuanzia kwenye *secondary society* na ukaacha kwenye vyama vya msingi mambo yakaendeshwa ovyo ovyo, tutakuwa hatujafanya jambo lolote.

Ningependa nimshauri Mheshimiwa Waziri alirekebishe hilo ili hata wale wanaoingia kwenye vyama vya msingi waweze kufanyiwa *vetting*. Lakini kuna swala ambalo hatujalionga ambalo ningependa na lenyewe liwemo kwamba hao watakaokuwa wanaingia kwenye ushirika wanakuwa na uhakika basi waweze kuwa na wadhamini ili

inapotokea kwamba wamesababisha ubadhirifu basi mali zao na za wadhamini wao zote ziweze kutaifishwa mara moja na kuweza kurejesha mali ya mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kulingezea ni suala la kifungu cha 18 ambalo linaelezea malengo ya vyama vya msingi yako matatu. Sasa mimi nitaongelea lile lengo la tatu linalosema kutoa huduma na nimejaribu kufanya *interpretation* ya suala hili ambalo linaweza isiwe sawasawa na yaliyoandikwa kwa kiingereza kwamba kutoa huduma kwa wanachama kutapata pembejeo, kufuata masuala ya *processing*, kutafuta masoko ya mazao na kutafuta masoko ya wanachama, ameishia pale.

Sasa mimi ningeshauri Mheshimiwa Waziri aongeze maneno mawili yafutayo:-

“Kwamba kutafuta mazao ya wanachama ndani ya masoko ya mazao ya wanachama ndani ya nchi na nje ya nchi, *locally and internationally*.” Kwa nini nalisema hilo? Nalisema hilo kwa sababu imekuwepo tabia ya kutoruhusu vyama vya msingi kuweza kujitafutia masoko moja kwa moja nje ya nchi. Waheshimiwa Wabunge kama walivyosema, waliotangulia ni kwamba kuna haja ya kumpa uhuru mkulima anayezalisha mazao yake aweze kuyauza popote kule ambako anaweza kupata soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaopinga hoja hii. Wanaipinga kwa sababu mbalimbali. Lakini ningependa niseme unaposema kwamba mwananchi wa Misenyi anapouza kahawa yake Uganda hachangii uchumi wa Taifa, unakuwa wewe ni mtu kwanza asiyejua uchumi na unaonyesha kwamba mawazo yako yamepitwa na wakati na unaonyesha kwamba haujui hata dunia unayoendelea kuishi. (*Makofi*)

Kwa nini nasema hivyo, Mheshimiwa Mwenyekiti? Wananchi wa Misenyi wa Minziro, wa Nsunga, anapouza kahawa yake Uganda, akapewa shilingi 1,000 kwa kilo, hii shilingi 1,000 hatakaa nayo nyumbani kwake. Ataenda dukani anunue sukari. Ataenda kwenye bucha anunue nyama, ataenda kwenye duka anunue mfuko wa *cement* na unapotoa fedha ukanunua mfuko wa *cement*, unapotoa fedha ukanunua sukari, maana yake unachangia uchumi wa Taifa.

Kwa hiyo, ni aibu na mawazo yaliyopitwa na wakati, kumwambia huyu aliyeuza kahawa yake Uganda kwamba hachangii uchumi wa Taifa eti kwa sababu tu alipewa shilingi 1,000 badala angeuza Tanzania akapewa shilingi 200 kwa kilo. Kwa hiyo mimi nasema wenye mawazo ya namna hiyo, yamepitwa na wakati na inabidi wajirekebishe haraka ili waonekane kwamba sasa wanaenda na karne ya sayansi na teknolojia, karne ya utandawazi. Kwa sababu ya kwanza ni hivi, kwamba kiuchumi hakuna ubishi, kwamba ukimruhusu ukamwekea utaratibu mzuri akauza kahawa yake Uganda bado atasaidia pato la Taifa, la kwanza.

Lakini la pili tuko kwenye *globalization* Mheshimiwa Mwenyekiti na *globalization* mara nyingi jimboni kwangu wananchi walikuwa wananiuliza Mheshimiwa nini maana ya *globalization*. Sasa mimi nilikuwa sijaelewa, nikawa natoa *globalization*



badala ya kusema kama hivyo ndivyo ilivyo, mbona sasa mnasema kahawa yetu tusiuzue Uganda, ndiyo *globalization* hiyo, unauza popote penye soko zuri.

Sasa nimeshagundua kwamba hawa wananchi wa vijijini wanajua sana kuliko sisi tunaofikiri tunajua. Lakini hapa Tanzania tunayo bahati, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa ndiyo Mwenyekiti wa *globalization* kwa nchi zinazoendelea. Lakini tatizo lililopo Rais wetu yuko hatua 500 mbele akihubiri *globalization*, lakini sisi Watanzania tuko hatua 10,000 nyuma tukiwa kwenye giza nene bila kujua *globalization* ni kitu gani.

Sasa mimi nafikiri tuondokane na mawazo ya kufikiria kwamba kwa mkulima *globalization* ni kwa wafanya biashara tu na *globalization* sio kwa mkulima. Ni hoja ya pili ya kwa nini hiki kirekebishwe. Lakini hoja ya tatu, Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingia katika Afrika Mashariki na mwezi wa 11 naambiwa kama mambo yakienda yalivyopangwa, tunasaini, tutakuwa na hii tunaita *Custom Union*. Sasa maana ya *Custom Union* maana yake ni kwamba suala la kusema kuna mpaka wa Tanzania, kuna mpaka wa Kenya halipo tena. Kwa sababu kodi zote ambazo ungefikiri ungezipoteza kwa huyu kuuza kahawa yake Uganda au akauza kupitia Kenya itakuwa haipo tena kwa sababu hizi kodi zote za ndani ya mipaka ambazo zilikuwepo zote zitaondoka moja kwa moja.

Kwa hiyo, kuendelea kumzuia mwananchi wa Kagera asiuzue popote anapoweza kupata bei nzuri kwa hoja kwamba tutapoteza kodi haipo, kwa sababu muda si mrefu tutasaini mkataba wa *Custom Union*. Hiyo ni hoja ya msingi kabisa. (*Makofi*)

Lakini sababu ya nne Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwa nini tuwape wananchi uhuru wao wa kuuza mazao popote wanapoweza kupata kupata soko ni kwamba ziko sheria nyingi ambazo zinatumiwa na wenzetu kwa nia nzuri tu. Utakuta kule mipakani watu wana bunduki na mizinga, wanasema tuko tunapambana na wanaopeleka kuuza kahawa Uganda. Labda ukiuliza wanasema tunasimamia Sheria. Lakini sheria hizi zimepitwa na wakati. Sheria nyingine zimetungwa wakati wa mkoloni, lakini sheria nyingine zimetungwa wakati Tanzania tuliaini kwamba mtu yoyote anayefanya biashara ni mwizi na ni mnyonyaji. Tuliunga sheria hizi kwa kipindi ambacho sisi tulikuwa tunafikiri ukisema bepari ni jambo la hatari na wewe haufai hata kuishi.

Sasa kama sheria zimeshapitwa na wakati ni vizuri hata kama wewe kazi yako ni kusimamia sheria hizi huonyeshi kwamba unaweza ukatumia busara kidogo tu. Ukasema pamoja na kwamba sheria hii ipo, nafikiri sheria hii imepitwa na wakati. Mimi nalisema hilo kwa makusudi kabisa kwa sababu natambua ni vigumu sana kwa sheria zote zilizopitwa na wakati tukazibadilisha. Siyo jambo jepesi.

Lakini sheria hizo mantiki inataka zibadilishwe. Kwa hiyo, mimi nashauri Serikali na wale mnaowatumia kusimamia Sheria zilizopitwa na wakati, basi mtumie busara kidogo mzitazame kama sheria imepitwa na wakati inakuambia kamata, piga viboko, maana yake na wewe peleka kuuza kahawa Uganda basi, unasema lakini kwa nini huyu anapeleka. Anapeleka Uganda kwa sababu anaona kwa kilo moja atapata 1,000 na akiuza Tanzania anapata shilingi 200/=.

Kwa hiyo, wewe unaishauri Serikali iboreshe soko la ndani. Ukifanikiwa kuboresha soko la ndani, huna sababu ya kuweka maaskari mipakani kupambana na wakulima wanaopeleka kahawa hiyo Uganda.

Kwa hiyo, tunayo kazi kubwa zaidi ya kufanya Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliko kuendelea kufikiria kwamba unaweza ukatumia mtutu wa bunduki kumzuia mwananchi kuuza kahawa mpaka anafikiri anaweza kupata soko zuri, haiwezikani kabisa.

Tunaposema maendeleo ni pamoja na uhuru wa kuamua na mkulima kwa jinsi anavyoenda shambani peke yake akalima bila kusimamiwa na polisi apewe uhuru sasa inapofika wakati wa kuuza mazao yake auze bila kusimamiwa na polisi bila kupigwa viboko ili ya kufunguliwa ovyo ovyo kwa kisingizio eti unasimamia sheria. Sasa napenda niseme kama sheria imepitwa na wakati unaitazama, unatumia busara zako, unaachana nayo, wakati unasubiri Waheshimiwa Wabunge wakikutana Dodoma na Serikali ikipata nafasi kuweza kurekebisha sheria hiyo.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme, wale wenye mawazo ya kwamba mkulima wa kahawa akiruhusiwa kuuza kahawa yake Uganda tutapoteza fedha za kigeni, jibu lake ni kwamba tunaweza tukaweka utaratibu mzuri wa hao Waganda wakaja na fedha za kigeni kununua fedha hiyo. Sioni tatizo hilo. Kama unafikiri wakiuza kule tunakosa fedha za kigeni basi unaweza kuweka utaratibu mzuri wa kuwezesha wanaokuja kununua wakaja na fedha za kigeni. La kwanza.

Lakini la pili, kama Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria tulizopitisha katika Bunge hili, zinaruhusu wawekezaji kwenye migodi, inaruhusu wawekezaji kwenye mabenki, kupeleka mamilioni ya dola popote kule duniani, na kuyaweka, inakuwaje sisi hao hao tunakuwa wachungu na wakali kwa ukali usiokuwa wa akili kuzuia mkulima mdogo anayeweza kuuza kahawa yake na akapata dola 10, mimi sielewi. (*Makofi*)

*Quite unbelievable*, kwa hiyo, ndiyo maana nasema lazima tusiwe na *double standards*, kwamba kwa mwekezaji kutoka nje ruksa kukusanya dola kupeleka popote kule na tukasema huo ndio uchumi huria. Lakini kwa mkulima wa kahawa nasema hiyo siyo uchumi, siyo uchumi huria.

Kwa hiyo, mimi nadhani tunakuwa hatuelewi tunachokisema na ni vizuri tukajifunza kwenda na wakati. Tuko ndani ya *globalization* na *globalization* sio kumsaidia mfanyabiashara wa madini tu, wala mfanya biashara wa kwenye mabenki tu. Ni pamoja na mkulima. Tuwape wakulima uhuru wa kuamua, wakulima wana uwezo wa kuamua na kufikia maamuzi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nasema kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye huu Muswada wa

Ushirika. Nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyowasilisha, ilikuwa ni kwa ufupi lakini kwa ufasaha mkubwa. Lakini pia tumeweza kufikia kwenye hali nzuri sana ya kuelewa nia yao kama Wizara na kwa kweli nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na Wizara yake nzima kwa sababu kwa uelewa wangu nafikiri tangia Wizara hii imeundwa huu ndio Muswada wao wa kwanza kuwasilisha hapa. Hongereni sana. Awali nafikiri waliwasilisha Muswada ambao ulikuwa umetokea Kilimo. Ule wa Tumbaku wa mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja hii. Nina msingi thabiti kabisa kuunga mkono hoja hii na moja ni kwamba wananchi wetu walio zaidi ya asilimia 75 au tuseme 80 wako vijijini na njia moja wapo ambayo inaweza kuwafanya watambulike tambulike katika mwenendo wa uchumi wa kisasa ni kupitia mabanki na vyombo vya namna hiyo, ni kupitia kwenye ushirika.

Sasa kumekuwa na matatizo mengi ambayo yalikuwa yanahitaji kuwa *addressed* kwenye ushirika na yalikuwa hayawezekani kuwa *addressed* nje ya Sheria ya Ushirika na ilikuwa na haja ya kurekebisha na wao wameleta marekebisha yao na nyongeza ambazo nafikiri zitaweza sasa kumsogeza zaidi mkulima kwenye kutambulika na taasisi zingine za kiuchumi kama moja kati ya watu ambao na wao wanaweza waka-*incorporate* kwenye zao ili wao na wao waweze kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nianzie suala la kijumla ambalo huwa nalipata unapoongelea hizi *co-operative societies* au ushirika huku. Ukiangalia kwenye *definition* ukurasa wa 9, *definition* imeandikwa pale. Ukiisoma hiyo *definition in fact* inakueleza kitu ambacho huwa nakiona mimi siku zote kwamba ushirika unaweza ukadhani kwamba ni watu waliokuja wamesogeleana karibu sana na wanafanya shughuli zao kwa ukaribu huo, wala si kweli. Huwa naona mara nyingi ukiangalia hata wewe utaona ni kwamba wamesogeleana ili kupata soko la pamoja la kutoa na kupokea nafikiri hili sasa ndiyo nataka niseme nafikiri ni *challenge* kwa Wizara hii ya Ushirika na Masoko.

Labda nilinganishe kidogo kwamba hii *definition* hii ya Ushirika vs ile *Cap. 212* ambapo unazungumzia makampuni kwa sababu huku kuna *share holding* na kule kuna *share holding*, lakini hawa wana *common needs* kama walivyo huku, lakini *they don't have common do*, kama ambavyo kule kwenye *Cap.212* kuna *common do*.

Sasa hii inaweza kuwa ndio madosari ambayo Ushirika na Masoko kama Wizara wanaweza wakajielekeza kuwasaidia hawa watu wawe imara zaidi katika ushirika wao. Kwa sababu huu ujumla wao kwenye kujumuika kwenye soko ndio nafikiri huwa ni chanzo. Mimi nafikiri, huwa ni chanzo cha yale matatizo ambayo yanasababisha mifarakano ndani ya ushirika wao.

Niende moja kwa moja kwenye baadhi tu ya vipengele ambavyo niliamua nivi-*highlight* kwenye mazungumzo yangu. Ukurasa wa 12 kwenye *clause five* yameongelewa majukumu ya Serikali kwa ushirika. Ni mistari mitatu. Sasa sidhani kama hii Wizara kweli iliundwa ili iwe na majukumu ya kiwango hicho kwa mistari mitatu, tena kwa sentensi moja kwa kweli.

Mimi nafikiri kuna haja ya kupanua hapa, kuelewa kwa nini hii Wizara inaweza ikamfanyia mshirika. Nafikiri kuna haja kabisa. Mimi kwa mfano, nilikuwa nafikiria kwa sababu wao wanatakiwa kuwa ndiyo dira na nataka niseme hivi kwa unyenyekevu mkubwa bila kutaka kumweka mtu mwingine kwenye nafasi yoyote mbaya kwamba wananchi wetu wanahitaji kusaidiwa katika kuelewa kwa yale ambayo tunataka washiriki nayo.

Huu ushirika unaweza ukadhani wanauelewa. Lakini ukienda kule ukitoa *test* kwa wale wale ambao wako kwenye ushirika, kwa kweli watapata matatizo sana kufaulu hiyo *test*. Kwa sababu uelewa wao kila mmoja unakuwa ni tofauti sana. Sasa hao wanahitaji elimu na elimu inatakiwa iwe ni ile ambayo itafanana. Kuna pendekezo limetoka hapa kwamba iwe kwenye mitaala yetu, mimi nafikiri hiyo inaweza kuwa ni moja kati ya namna ya kufikiria lakini unahitaji kwa kweli elimu na elimu ya ushirika kwa mapana yake ambayo nafikiri Waheshimiwa ambao wapo kwenye chuo cha Ushirika wanaweza wakatusaidia sana kutueleza ushirika kwa mapana yake kwenye elimu unaweza ukaitoaje kwa mkulima.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri Serikali kwa kweli inatakiwa kujikita kwenye hilo na itamke bayana, kwamba inamsaidia mkulima. Sasa jinsi gani italifanya hilo, nafikiri ni suala ambalo wanaweza wakaendelea kuliongea wao kama Serikali Kuu lakini na Halmashauri na hapa Mheshimiwa Mwenyekiti nilikuwa nataka niingize hilo la pili, kwamba kwa kweli kwenye sheria hii kuna haja ya kuingiza *clause ambayo ita-involve directly* ushiriki wa Halmashauri zetu kwenye hii Sheria kwenye vyama vya ushirika.

Kwa sababu ukienda kwenye ukurasa unaofuata au *clause 7(ii) yes*, kwenye *page 14*. Sasa hapa kuna njia ndefu tena hapo. Unataka kupitia kwa Waziri wa TAMISEMI, kupitia kwa RC, mimi nafikiri haya ndiyo mambo ambayo yanatucheleweshwa siku zote kwenye maamuzi yetu. Mimi nafikiri tusitake na kwanza usisahau kwanza unashughulika na watu ambao hata kufuatilia hawawezi.

Kwa sababu kama kuna kitu cha ku-*rectify*, unaki-*rectify* kule kwenye Ushirika kwa watu wa kule kwenye ushirika. Sisi kama Wabunge wao kwa mfano tunajitahidi sana kuwaeleza namna ambayo tunaweza tukashirikiana nao kwa karibu pindi tatizo linapotokea ili tuweze kulishughulikia. Lakini bado tunakuwa na matatizo ya kuwa na haja ya kushirikiana na sisi, lakini lazima tuelewe pia na wao wana matatizo ya kutaka kupata huo msaada kutoka juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri linaeleweka hili, *logistics*, lakini pia na utayari wao pia vinaonyesha kwamba wana haja ya kusaidiwa zaidi.

Sasa unatakiwa hapa nafikiri uangalie moja kwa moja. Mimi nataka niseme Halmashauri hizi kwanza ukiziangalia, zina kila kitu kule ndani. Wizara zote ziko pale. Sasa mimi sioni kwa nini hapa upitie kwa Waziri wa TAMISEMI. Sasa mimi nafikiri utakuwa ni ucheleweshaji ambao sio wa lazima sana. Tunaweza tukaondokana nao.

Sasa labda niseme tu kwa kujaribu kueleweka, jinsi gani Serikali sasa kwa maana hiyo, Serikali Kuu Wazira yake na hawa Halmashauri, wanaweza wakashiriki, kiuongozi kwenye kuboresha kuimarisha ushirika, kimalengo na utekelezaji, kiutaalam kifedha na vitu vya namna hiyo, elimu, kuwe na *interventions* kutoka kwenye Halmashauri inapobidi, wasiachwe tu. Nafurahi kwamba lugha iliyotumika kwenye huu Muswada kwa kweli inampa hiari ya kutosha kabisa mshirika mwenyewe.

Lakini nataka pia tuisahau kwamba mimi nitoe mfano, katika jimbo langu kulikuwa na vyama vya msingi 9 ambavyo viliwahi kufanya biashara na mtu mmoja ambaye alipokuja huyo mtu, Serikali iliwashauri vyama vya msingi kwamba wasifanye biashara naye, hicho tu pekee Serikali iliona inaweza kufanya kwa sababu ushirika ni hiari na maamuzi yalikuwa ni ya washirika.

Sasa wakafanyabiashara na bwana yule wakaingia kwenye matatizo makubwa sana. Sasa sisi tulikwenda katika ziara tukiwa na Mkuu wa Mkoa, wakulima wakasema mnataka sisi tufanye nini, tunakubali tumefanya makosa mlituambia tukasikia mlichosema lakini bado tukafanya tulichofanya na tumeingia kwenye matatizo sasa tumwambie nani na ninyi ndiyo Serikali? Sasa utaona hapo jinsi ambavyo wanakirudia kile kile ambacho wewe ulikuwa umewaambia ni hiyari yenu lakini bado wanafikiri ni mzigo ambao unatakiwa kuubeba.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri pamoja na lugha ya hiyari ambayo iko kwenye huu Muswada, ni kitu kizuri lakini kuna haja kwa kweli ya mahali pengine kwa kutumia au *by-laws*, kanuni ambazo zinaweza zikatungwa kupitia kwenye huu Muswada, kuwa na haja ya kuwa na *interventions*, kuhalalisha *interventions* za kutoka Serikali Kuu na Halmashauri kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendeele kwenye *clause 13*, ukurasa wa 16, nataka hii niweke dhidi ya *clause 11(3)* ambayo iko kwenye ukurasa wa 15 inasema, “*Registrar upon consultation with the Assistant Registrar in the region.*” Sasa hapa nataka ni *assume* kwamba wanaongelea *structure* ya nchi yetu kwamba kwenye Mkoa kutakuwa na huyu *Assistant Registrar*. Sasa ukienda *clause 13* hapa anasema: “*Appointment of Assistant Registrars,*” anasema: “*There shall be such number of Assistant Registrars who shall be appointed by the Minister from amongst Principal Cooperative Officers.*”

Sasa mimi nafikiri hapa kuna haja ya kuondoa hii *ambiguity*, kwa nini tu isitamkwe moja kwa moja ili ifanane kwamba ni kila Mkoa atakuwepo mtu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause* ya 18 ambapo ni malengo sasa ya Vyama vya Msingi, mimi nilikuwa nafikiri lugha ambayo kwanza hapa inatakiwa kutumika ni iwe ambayo inawaruhusu hawa watu kuendelea, wasiwe *limited* kwenye *functions* fulani ambazo zimetamkwa hapa, wafunguliwe mlango kwa kuanzia hizi na wawe wanaweza kuendelea.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri labda *language* pale, *the objects of a Primary society shall include may be* inaweza kuwa inafungua mlango wakati pia inataka kuyasimamia yale ambayo yamewekwa hapa ambayo nafikiri si mabaya.

La kwanza, (a) anasema, “*To strive to raise the standard of living of its Members.*” Mimi nafikiri hapa kuna *language* nyingine ambayo ingeweza kutumika labda tuseme tu kwamba watengeneze pesa, kwani wamejiunga kwenda kutengeneza pesa. Mimi huwa nawaambia washirika kwamba kama umeingia kwenye ushirika na hutengenezi pesa basi toka. Mimi nilikuwa nafikiri *language* ya namna hiyo kwamba wawe na lengo la kutengeneza pesa *as much as possible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pale kwenye kipengele cha pili kuna haja ya kuongeza neno mahali fulani, nilikuwa nafikiri kwamba *to facilitate the faithful operations of the individual members* ingefaa zaidi. Hapa kuna suala la msingi kabisa, kuna watu wanakopa hapa wanatorosha wanakwenda kuuza kule, tuna tatizo kubwa sana kwenye Vyama vya Msingi vya Tumbaku.

Sasa hapa hawa watu lazima wawe na namna au *mechanism* ya kusimamiana kule ndani ya Ushirika. Nilikuwa nafikiri hapa panapendekeza, panafaa kuingiza hilo la nguvu kwamba matazamio yangu ya haraka haraka nikafikiri, hili ongezo linaweza likasaidia lakini nafikiri wataalam wako wanaweza wakasaidia zaidi hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele cha tatu, nataka tutumie nafasi hii kuwafikiria si tu wale wanachama wa ushirika ambao kwa mfano ni Ushirika wa Tumbaku lakini tutumie pia nafasi hii ya ushirika kuwapo kwenye sehemu fulani, kuwajumuisha na wale ambao hawako kwenye ushirika na wanajishughulisha na mazao mchanganyiko kwamba wao wawe *provided* pia na kupitia nguvu ya ushirika ambayo itakuwa imejengwa hapa na nafasi ya kupokea na wao pembejeo kama hiyo itawezekana na kuendeleza shughuli kwenye mazao ambayo ni mbali na lile la msingi ambalo linashughulikiwa na ushirika.

Kwa hiyo, hapa kuna haja nafikiri ya kuingiza matamshi ya namna hiyo ili hawa wakulima ambao hawalimi, kwa mfano kwenye Jimbo langu hawalimi tumbaku na Vyama vya Msingi na Ushirika kweli ni vya tumbaku, waweze nao kwa namna fulani kufikiriwa katika mahitaji yao. Nataka niseme tu kwa mfano tuna njaa mwaka huu na mwaka kesho, nafikiri hali inaweza isiwe nzuri sana maana ni mwaka unaoishia na nne.

Sasa kwa mfano, kama Chama cha Msingi cha Ushirika kingekuwa kina pesa ya kutosha badala ya kuwaacha washirika wake na wananchi wa eneo lile kwenye ile *locality* ambayo iko Chama cha Msingi, wauze tu mahindi wanavyotaka, kwa mfano kama kingenunua yale mahindi kwa bei nzuri na kuyaweka pale na kuyatunza, sasa hivi wangekuwa wanawauzia washirika wao na wananchi katika *locality* yao kwa bei nzuri tu na ingeweza kupunguza matatizo ya njaa. Sasa vitu vya namna hii nilikuwa nafikiri vinaweza kuwa *considered* hapa.

Mwisho, nataka niende kwenye *clause 44*, ukurasa wa 29. Kwa uzoefu wangu sasa kutokea kwenye Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001, tatizo limekuwa ni uelewa wa hii Sheria kwa sababu iko kwenye lugha ya kiingereza. Wenzetu wa ardhi kwenye Sheria yao Na. 4 na Na. 5, walitoa tasfiri za kiswahili na mimi napenda kuwapongeza sana. Kwa kweli nataka niseme, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliwasilisha ile ya tumbaku ya mwaka 2001 tafadhalini sana, haraka sana tengenezeni *translation* rasmi ya hiyo Sheria ya kiswahili. Hapa nataka mu-include sasa *may be in future* labda muwe mnafanya hivyo, kwenye hii 44(b) anasema: “*Keep a copy of this Act, halafu imeendelea rules and so on.*”

Mimi nilikuwa nafikiri hapa muongeze *and official* kiswahili *version of the act* ambayo muwe *obliged* ninyi kuitoa baada ya kuwa Mheshimiwa Rais amekwishakusaini hiyo Sheria na kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bado nina dakika mbili nataka nirudi tena niseme kwa ujumla tu kwamba napenda kuipongeza Serikali kwanza kwa kuleta huu Muswada, natambua unaweza usiwe umekumbatia kila tatizo ambalo tunatakiwa tutatue kupitia kwenye Muswada huu lakini walau umetoa nafasi ya kushughulikia yale matatizo ambayo yalikuwa yamejitokeza kutokana na ile Sheria ya nyuma na isitoshe kuna ile *optional language* ambayo iko kwenye huu Muswada ambayo ni nzuri lakini nataka niseme ya kwamba kuna haja ya Serikali walau sasa kupitia kwenye kanuni za Sheria hii kuweka dhamira ya Serikali bayana kabisa kwamba itataka kusimamia, mambo ya kipuuzi puuzi yasiwepo eti kwa sababu watu wana uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nirejee kwenye haya niliyoyasema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nami napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wake na Wizara nzima kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu. Kama walivyosema wenzangu, Muswada huu umechelewa kwa sababu ndiyo hasa ungeleta uhai na matumaini makubwa katika ushirika ambao kwa kweli ndiyo tegemeo la wananchi wetu. Kwa hiyo, Muswada huu ninauunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ni mzuri na unajitosheleza kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya Muswada huu inaweka bayana misingi ya ushirika, misingi ambayo inakubalika Kimataifa. Kwa kweli Muswada huu unamaliza utata ambao tulikuwa nao huko nyuma wa aina gani ya ushirika tulionao, Muswada huu unamaliza hili ingawa kumetokea hoja hapa kwamba pengine hii misingi itazamwe kulingana na mazingira ya nchi yetu kulingana na dhamira na taratibu zetu. Lakini mimi napenda kusema ya kwamba hii ni dunia ya utandawazi tusirudishe viwango, tushikilie viwango ambavyo vinakubalika Kimataifa na pia tushikilie kanuni

ambazo zinakubalika Kimataifa. Kwa hiyo, mimi napenda kusema ya kwamba sasa Muswada huu umejibu ile hoja ya aina ya ushirika ambao tunataka tuujenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya msingi ambayo ipo katika sehemu hii, ni kwamba wananchi watajiunga na ushirika kwa hiyari na wataendesha shughuli zao kwa misingi ya kidemokrasia. Sasa mimi kama walivyosema wenzangu ni kwamba ili wananchi wafanye uamuzi wa hiyari wa kuunda ushirika wao, lazima waelimishwe, wahamasishwe, hilo ndiyo jambo la msingi Serikali, Taasisi na sisi wote Waheshimiwa Wabunge tusikwepe huu wajibu wa kuelimisha na kuhamasisha ili wananchi waweze kuona faida na umuhimu wa ushirika lakini uamuzi wa kuunda ushirika waachiwe wenyewe, hiyo ndiyo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitegemee ya kwamba wananchi wetu watakuwa tayari kujiunga na ushirika bila kuelezwa, bila kufafanuliwa na bila kuelemeshwa juu ya faida na hasara za ushirika. Kwa hiyo, kuna kazi mbili hapa ambazo lazima tuzifanye kwa pamoja.

Kwanza, ni kuhamasisha na kuelimisha lakini pili, kuwaachia wananchi wenyewe wafanye uamuzi wa kuunda ushirika. Ule mtindo wa wataalam na viongozi kuwaangalia na kuwapelekea wananchi ushirika, mimi nasema utahatarisha na utauwa uhai wa ushirika wenyewe. Tusiwapelekee ushirika, ushirika utokane na wao wenyewe na hiyo ndiyo njia mojawapo na nafikiri ndiyo tulichokosea miaka iliyopita tukawa tunawapelekea wananchi wetu ushirika tunafikiri unaweza kuwafaa lakini kumbe hautokani na wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kujenga hoja hapa kwamba elimu ya ushirika ndiyo itakayokuwa msukumo wa kujenga na kuimarisha ushirika huu unaozungumziwa katika Muswada huu, elimu ya ushirika. Bila elimu ya ushirika Muswada huu utapata taabu sana kutekelezwa. Katika kifungu cha 74 uko Mfuko, unaitwa Mfuko Mkuu wa Ushirika, hiyo ni tasfiri yangu lakini katika Muswada wenyewe imeandikwa, *Central Cooperative Fund*, mimi ninaita Mfuko Mkuu wa Ushirika. Kifungu hiki cha 74(3) ndicho hasa nataka nikisemee kwamba Mfuko huu tutakapouunda au Serikali itakapounda Mfuko huu, ufike na utumike kwenye ngazi ya wanachama wenyewe kule chini, usiishie kwenye ngazi ya kati au ngazi ya juu maana iko tabia ya kufikiri kwamba wakubwa wakipata semina basi inatoshwa na wananchi wa kawaida wakakosa ile semina ambayo inatakiwa. Kwa hiyo, unaweza kukuta ya kwamba tunajielimisha juu kule chini hawaelimiki. Kwa hiyo, nashauri hapa kwamba Mfuko huu ufike na utumike zaidi kwenye ngazi ya wanachama na wananchi wa kawaida ili wajengwe na waimarike katika elimu ya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko njia nyingi tumezitumia na naomba Serikali ione namna ya kuzifufua, kwa mfano elimu kwa njia ya radio, elimu kwa njia ya posta na pia elimu kwa njia ya majalida kwa kutumia Mfuko huu. Kwa hiyo, kuna njia ambazo tulikuwa tunazitumia zamani ambazo zilimwezesha mwananchi wa kawaida kufahamu juu ya ushirika. Sasa mimi naomba tuzifufue hizo na tutumie Mfuko huu ambao unakusudiwa kuundwa na Muswada huu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, upo msingi mwingine katika sehemu hii ya pili nao unahusu demokrasia. Dhana ya demokrasia inajitokeza na lazima ionekane wazi katika maeneo makubwa matatu. Moja, katika mikutano ya wanachama wote, pili, uchaguzi wa viongozi wa Kamati mbalimbali na tatu, uwajibikaji wa uongozi kwa wanachama na udhibiti wa wanachama kuhusu mwenendo wa ushirika wao. Upo umuhimu wa kuweka bayana haki na uhuru wa wanachama wa kuchagua na kuchaguliwa na uwajibakaji wa viongozi kwa wanachama, nashukuru Serikali imeliweka bayana katika sehemu ya sita. Imeelezea vizuri kabisa haki na wajibu wa wanachama, imeelezwa vizuri linalotakiwa hapa ni wanachama wetu kufahamishwa kikamilifu ili wajue haki zao na wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile katika nyongeza huku mwisho, katika *schedule* huku, kuna kitu kinaitwa kanuni za mwenendo, mimi nimetafsiri kama ni kanuni za mwenendo lakini hapa imeandikwa *code of conduct*. Hizi nazo ni muhimu, kwa kweli pamoja na kwamba ziko kwenye nyongeza huku mwisho lakini ni kanuni za msingi, kanuni zilizo muhimu ambazo wanachama wanatakiwa wazifahamu ili ziwawezeshe kusimamia ushirika wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda niseme mambo mawili mengine. Moja, ni kwamba management na utawala wa ushirika ni taaluma na watu wamesomea na wamesomea katika viwango mbalimbali. Ushirika nchini utaimarika na utasimamiwa kikamilifu kama Chuo chetu cha Ushirika Moshi kitaimarishwa. Mimi naomba kutoa hoja hapa kwamba sasa wakati umefika wa Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu kamili cha Ushirika ili kiweze kupanua shughuli zake za kutoa taaluma, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika masuala yote yanayohusiana na ushirika. Napenda kutoa hoja ya kwamba sasa wakati umefika kwa Serikali kuleta Muswada na tutauunga mkono wa kukifanya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu kamili tena sio Kishiriki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea hoja hapa watu wanasema, Chuo cha Ushirika Moshi kiwe Kishiriki cha Chuo kingine mahali huko kama kilomita 800.

Mimi napenda kusema ya kwamba kiwe Chuo Kikuu Kishiriki kamili. Kwa sababu hiyo hoja aliyotoa Mheshimiwa Talala Mbise, hapa basi inakuwa na umuhimu wake. Katika Ibara ile ya saba, kipengele cha tatu kwamba Mheshimiwa Waziri atatoa maelekezo kwa Chuo cha Ushirika kuhusu kufundisha na kadhalika itabidi hapa kabadilishwe.

Sasa hivi anaweza akafanya hivyo kwa sababu Chuo cha Ushirika Moshi kipo chini ya Wizara lakini kitakapokuwa Chuo Kikuu kamili hakitakuwa chini ya Wizara ile, kitakuwa kwenye Wizara nyingine ya Elimu ya Juu na Sayansi. Kwa hiyo, hapa mimi nashauri kuwe na marekebisho, pengine unaweza kusema, *the minister may consult with cooperative college and other institutions of learning* kwa ajili ya kufundisha na kadhalika likabadilika hili ili ijiandae kupokea hoja hiyo mpya ya kukifanya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu kamili na kikiwa Chuo Kikuu kamili maana yake

kitaondoka kutoka Wizara hii na kitakuwa kwenye Wizara nyingine ambayo Mheshimiwa Waziri wa sasa wa Ushirika hawezi kuwa na madaraka nacho tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, wenzangu wamezungumzia juu ya mitaala, mimi napenda kusema ya kwamba hili linawezekana. Kama tunataka ushirika uwe ni sehemu ya mfumo wa uchumi na kijamii wa wananchi wetu, inawezekana kabisa tukaanza kufundisha shuleni, kwenye shule za msingi na za sekondari katika viwango mbalimbali na wataalam wanaweza wakatafuta maeneo yanayofaa kwenye shule za msingi na yale yanayofaa kwenye shule za sekondari na lazima watafanya hata mchepuo.

Katika michepuo ambayo ipo sasa hivi ukishafika sekondari, miaka ile ya mwisho ya sekondari unaambiwa uchague kwenda sanaa au ubaki sayansi, huwezi kuona somo la ushirika pale lakini inawezekana likawepo kwa sababu ni taaluma.

Kwa hiyo, mimi napenda kusema ya kwamba kuna haja sasa ya kupenyeza dhana hii ya ushirika ili ianze kufahamika kwa vijana wetu toka mwanzo, tusingubiri mpaka wamekwishakuwa watu wazima ndipo sasa tunaanza kuwazungumzia juu ya ushirika, waufahamu toka mwanzo.

Mimi napenda kusema ya kwamba inawezekana kabisa na ikapangwa mitaala kulingana na viwango vya shule hizi tulizonazo, kiwango cha shule ya msingi wafundishe kiasi gani ushirika, kiwango cha sekondari wafundishwe kiasi gani ushirika na kadhalika. Hii inawezekana na inaweza kutujengea uhalali wa kudumu na uelewa wa kudumu wa ushirika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, napenda kusema ya kwamba Muswada huu ni mzuri tuunge mkono kwa sababu ndio utakaosaidia kutatua matatizo mengi tuliyokuwa nayo katika ushirika na kwa hiyo mimi mwenyewe hapa kama nilivyosema nauunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mjadala huu utaendelea leo jioni. Inaonyesha Waheshimiwa Wabunge wengi wamevutiwa kuchangia mpaka sasa orodha imebaki na Waheshimiwa Wabunge 12 na tulikwishakubaliana ya kwamba wanaotaka kuchangia hatutawanyima nafasi, tutachangia leo jioni kama watabaki tutaendelea, tunataka Waheshimiwa Wabunge wachangie tunavyoona inafaa.

Kwa hiyo, wale wote ambao wameleta nimekwishawaorodhesha na majina yanachapwa na pia kwa watakoleta, tunataka watu wachangie ili kuisaidia Wizara mawazo mengi maana yake hili ni jambo la msingi tunalolifanya kwa ajili ya nchi yetu.

Kwa hiyo, watu wasisite, tutachangia leo, ukilala tutaendelea tena Jumatatu mpaka tumalize ili mawazo yote yaweze kuwafikia walengwa na tuweze kufanya maamuzi ya msingi katika Muswada huu.

Basi kwa sasa hivi nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni. Shughuli zimesitishwa.

*(Saa 6.51 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa kutuletea Muswada huu katika wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Rais, ambayo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, walihusika na kupitia Kamati hiyo basi, Kamati ilibaini matatizo kadhaa ya ushirika na ndio mengi ambayo kwa kweli yamehusishwa katika Muswada. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na sina mashaka kabisa kwamba, kwa uzoefu wenu mliouonyesha, kazi ya ushirika itaendelea vizuri kwa nyongeza hii kubwa ambayo tunaipata baada ya Muswada huu kupata nafasi na baadaye kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata nafasi ya kuhudhuria kikao cha Kamati kilichofanyika Dar es Salaam kama mdau, ninayo mambo machache ambayo nataka niyatoe ili angalau kuboresha zaidi Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu ni suala la elimu ya ushirika. Nimetembea sana vijijini na kwa ujumla kule kwetu karibu kwenye kila kijiji unapata Chama cha Msingi. Lakini lipo tatizo kubwa sana la elimu ya ushirika. Bado nina wasiwasi kwamba, hata Muswada huu ukipita ukawa sheria, kama wanachama wetu hawatapata elimu ya ushirika, bado tutabaki na tatizo pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize maswali machache hapa sihitaji majibu lakini ndio mambo halisi yalivyo vijijini. Ni mwanaushirika yupi anaweza kuhoji uongozi hasa katika ngazi ya *Primary Society*, juu ya mapato na matumizi ya ushirika? Kwa ngazi ile hukuna na yeyote ambaye anathubutu kuhoji basi yako mambo kadhaa ambayo anastahili kuyapata kama ni haki yake anaweza kunyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda kwenye vijiji, baadhi ya Vyama vya Msingi siku wakiona Mheshimiwa Mbunge amekuja ama *DC*, wale wote ambao wanatoa kero pale, baada ya viongozi kuondoka basi inawezekana yule mwanaushirika pembejeo asipate au mambo mengine yoyote yale ya msingi ambayo anatakiwa apate kama mwanachama, hayapati. Sasa tunataka Muswada huu ukipita kuwa sheria, udhibiti hali hii mwanachama, apewe uhuru wa kusema yale anayoyaona kwamba hayampendezi katika kuendesha ushirika wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili ni suala la kuitisha mikutano. Ipo kanuni kabisa ya kuitisha mikutano lakini naomba sana wakati wa kutunga kanuni baada

ya Muswada huu kuwa sheria, kanuni hii iangaliwe upya. Mwanachama anautuhumu uongozi, hawa viongozi ndio wanaotakiwa baada ya wanachama kujiorodhesha wao watoe idhini kwamba mkutano huu ufanyike tarehe fulani na tarehe ile wanatangaza wao sasa huu mkutano hata miaka mingapi hauwezi kuitishwa. Kwa hiyo, naomba sana Wizara kupitia Muswada huu, iwawezeshe hawa wanaushirika wanapoona kwamba, lipo tatizo kubwa sana la viongozi basi iwepo njia rahisi ya kuitisha mkutano ili kujadili matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya niliyokuwa nayazungumza, ambayo hasa yanagusa elimu ya ushirika, ni matumaini yangu kabisa kwamba, elimu ya msingi kabisa ya ushirika itatolewa kwa wanachama wetu ili waweze kuuelewa Muswada huu baadaye utakapokuwa sheria lakini kuelewa haki na wajibu wao katika kuendesha Vyama vya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vyetu vya Msingi vingi sana vimekumbwa na tatizo la ubadhirifu. Mimi kila wakati najiuliza wakati wa enzi za akina Mheshimiwa Paul Bomani, Mheshimiwa Mzee Kahama, waliongoza ushirika enzi hizo hatuna wataalam wengi kama tuliona sasa, lakini ushirika katika kipindi kile ulijenga shule na kulipia ada watoto ambao walikuwa ni wa wanaushirika. Leo hii kipindi ambacho kwa kweli tunao wataalam wa kutosha na wasomi waliobobea ndani ya ushirika, wizi umezidi, wanachama wanadhulumiwa haki zao, tatizo ni nini? Kila wakati tunasema pale ambapo wasomi na wataalam wapo tunapata unafuu wa kuboresha kazi zetu. Sasa hili inawezekana kabisa ni tatizo la watu wanaoingia kwenye ushirika kiholela bila kuwa na mtazamo wa kujulikana historia yake ikoje na hili nitalisemea mwishoni wakati nazungumzia suala la uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uongozi kwanza, niipongeze sana Wizara kwa kuleta Muswada huu, ambao kwa kweli kwenye mapendekezo yake, unaonyesha dhahiri kabisa kwamba, kutakuwa na mabadiliko ya hawa viongozi kujaza fomu. Mimi sikuwa naridhishwa sana na utaratibu wa hapo awali wa viongozi wa ushirika wanavyopatikana na siku moja nilitoa mfano hapa. Lakini suala la kujaza fomu hili sio pekee ambalo kwa kweli linaweza kuwachuja hawa viongozi, vile vile lipo tatizo la namna ya kuwachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimehudhuria mikutano mingi ya viongozi wa ushirika, sijui hii kanuni ilipatikana wapi, tukishakaa kwenye mkutano anatafutwa Mwenyekiti wa muda, sasa pale kila upande unaangalia ni nani ambaye atateuliwa akakae pale ambaye atawaona wao hawa wengine hatawaona. Akishaenda kukaa pale, wewe hata kama una mkono mrefu namna gani, hupewi nafasi ya kuchangi watapewa watu wa kundi lile lingine. Mfano huu unafanana na mfano wa dalali anayeza vitu sokoni, akishasema *top* kwenye 2000 hata kama yuko wa 5000 hapewi kile kitu atapewa yule wa 2000 maana walikwishapatana huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu utaratibu kwa kweli ulikuwa sio utaratibu wa kidemokrasia. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iangalie upya suala la kuendesha mikutano ya uchaguzi, mtu atakapojaza fomu baada ya kujaza fomu wakija pale

wajieleze kama wanavyojieleza viongozi wengine na baada ya hapo suala la “*support kapita*” lisiwepo, watu wapige kura kama utaratibu wa kawaida, viongozi wachaguliwe kwa utaratibu wa kawaida na kura ziwe za siri kwa utaratibu wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, haya mambo yote tunazungumza wawezeshaji wakubwa sana ni Maafisa Ushirika. Leo Afisa Ushirika ndiye ambaye anatakiwa aende akakague Vyama vya Msingi kujua mahesabu yake lakini Maafisa Ushirika kule wanategemea misafara ya *DED*, misafara ya *DC*, misafara ya Wabunge, hawana chochote nafikiri hata *OC* hawapati. Sasa tunategemea nini, huyu anakwenda kukagua Chama cha Msingi ambacho kwa kweli kina fedha anafika pale anapokewa vizuri atalala saa tano kwa kusherehekea mgeni kafika, hivi kesho tunategemea huyu afanye kazi gani? Naomba sana Wizara iangalie suala la Maafisa Ushirika wawezeshwe ili waweze kufanya kazi zao vizuri kama wanavyofanya Idara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu haya, nilipata nafasi nzuri sana ya kuchangia, nashukuru sana suala la viongozi hawa kuitwa Rais halipo na mimi nililikataa hata kwenye Kamati na bado nasisitiza kwamba, ule sio utaratibu, tutakuwa na Marais wangapi katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja na sisi Mheshimiwa Waziri Muswada huu ukishapita, tuko tayari kukusaidia huko vijijini kuhakikisha unafanya kazi zake ipasavyo, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada huu muhimu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nichukue nafasi ya kwanza kabisa, kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Ushirika na Masoko, pamoja na wataalam wao, kwa kuandaa Muswada huu. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nichangie maeneo machache ya Muswada huu na nitakwenda moja kwa moja kwenye vipengele vya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Kifungu cha 15 ambacho kipo ukurasa wa 16. Kifungu hiki kinapendekeza idadi ya chini ya wanachama inayokidhi Chama cha Ushirika cha Msingi kuanzishwa na hapa katika kipengele hiki vyama vya sekta mbalimbali vimependekezwa. Kwa mfano, kipengele hiki kinasema kwamba, Chama cha Ushirika cha Msingi kinachohusika na kilimo kitahitaji wanachama 50 au zaidi kabla hakijaanzishwa. Aidha, kwa upande wa Vyama vya Kuweka na Kukopa, inapendekezwa wanachama wasiopungua 20. Pia kwa Chama cha Ujuzi Maalum, inapendekezwa wanachama 10 na vyama vingine wanachama 10 ndio kiwango cha chini kabisa ambacho kitaruhusu vyama vianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu liko kwenye tofauti hiyo kwamba, kwa nini Chama ambacho kinahusika na kilimo lazima kiwe na wanachama 50 na kile ambacho kinahusika na ujuzi maalum kiwe na wanachama 10 kwa kiwango cha chini na vyama vingine wanachama 10? Nafikiri hakuna sababu ya kutofautisha vyama hivi, tungeweza kuweka idadi sawa kwa vyama vyote kama ni wanachama 20 ieleweke kwamba ni wanachama 20.

Napenda nirejee kwenye Sheria ya mwaka 1991 ambapo ilikuwa kiwango cha chini cha kuanzisha Chama chochote cha Msingi cha Ushirika ni wanachama 10, sioni mantiki ya kuongeza mpaka wanachama 50, tatizo ni nini? Napendekeza tungeweza kuweka kiwango kimoja tu cha wanachama 20 kwa ajili ya kuanzisha Chama cha Msingi. Eneo la kwanza ndio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni Kifungu cha 21(2), kiko ukurasa wa 19. Kifungu hiki ni kipya na kinapendekeza uwezekano wa Chama cha Ushirika kuungana na kampuni. Sasa sielewi utaratibu wake utakuwaje, kweli Chama cha Ushirika kinaweza kuungana na Kampuni wakaelewana na wakaweza kuendesha shughuli yao barabara? Mimi siamini. Napendekeza kipengele hicho kiondolewe na Chama cha Ushirika kiungane na chama kingine cha ushirika, ambacho malengo na maudhui yake yanafanana lakini kampuni, nina wasiwasi. Pendekezo langu ni kwamba, wangeangalia kama kweli utaratibu huu unaweza kutekelezeka, kwa upande wangu nafikiri hautatekelezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la tatu linahusu Kifungu cha 23(2) ukurasa wa 21. Hapa ni lugha tu, napendekeza niongeze masahihisho. Katika kifungu hicho marekebisho yamefanyika na kifungu hicho sasa hivi kinasomeka vizuri. Lakini nipendekeze sahihisho dogo tu la neno moja linalosema "*respectively*", nafikiri lingekuja mwisho wa sentensi ndio Kiingereza kitakaa vizuri. Naomba nisome kifungu kipya kitakavyosomeka: "*No secondary society or federation shall be registered under this Act unless it consists of at least 20 or 10 members as registered societies respectively*", ndio Kiingereza kinavyokaa lakini huwezi kuweka *respectively* katikati, sielewi itakuwaje. Naomba sahihisho hilo dogo lifanyiwe kwa sababu neno hilo "*respectively*" likiwekwa mwisho linaleta maana halisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Kifungu cha 24(2) ukurasa huo huo wa 21. Kifungu hiki kinapendekeza idadi ya wanachama wanaohitajika kusaini fomu za maombi ya kusajiliwa. Kinachoshangaza hapa ni kwamba, Muswada unapendekeza kwamba, wanachama wanaotakiwa kusaini zile fomu za kuomba kusajiliwa wanatakiwa wawe 50, lakini ukienda kwenye Kifungu cha 15 ambacho nimekwishakitaja tuna Vyama vya Msingi ambavyo vinaruhusiwa kuanzishwa kwa idadi ya wanachama 10 ama 20, sasa unaniambia tena kwamba, haiwezekani mpaka wawepo wanachama 50 tena. Nafikiri tungezingatia Kifungu cha 15, kama tumekubaliana kwenye Kifungu cha 15 ni wanachama wangapi basi tuzingatie hiyo usije ukaongeza tena sharti lingine ambalo ni gumu sana ambalo halitekelezeki. Wanachama 50 utawapata wapi, utawapata kwenye Vyama vya Msingi vya Kilimo tu lakini ujuzi Maalum hutapata na vyama vingine vile ambavyo umesema kwamba, wanahitaji wanachama 10 tu kuweza kuanzishwa sasa

unamwambia kujaza fomu wasaini wanachama 50 watatoka wapi? Naomba kifungu hiki kiangaliwe upya na kifanyiwe marekebisho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Kifungu cha 26(3), kiko ukurasa wa 22. Napenda nimpongeze Waziri, kifungu hiki tayari amekisahihisha ni kwamba, kile kifungu hakihitajiki kwa sababu kinafanana na kile kilichotangulia. Kwa hiyo, napenda nimpongeze kwa kuona hilo, hilo sina tatizo nalo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho ningependa nichangie ni Kifungu cha 94(5) kipo ukurasa wa 56. Kifungu hiki kinampa mamlaka Mrajisi kufuta usajili wa Chama cha Ushirika kinachokataa ushauri wake wa kuungana na chama kingine. Hapa inapendekezwa kwamba, Mrajisi atashauri akiona inafaa Vyama viungane lakini pia inapendekezwa kwamba, endapo Chama chochote kitakataa kuungana na Vyama vingine kufuatana na ushauri wa Mrajisi, ana uwezo ama anaweza kukifuta. Mimi sioni hapa demokrasia iko wapi? Chama ni chama cha hiari na kujiunga ama kuungana na Vyama vingine ni hiari yao wanachama, Mrajisi yuko pale kushauri ili kuhakikisha kwamba, Vyama vinafanya kazi inavyotakiwa sasa kama wanachama hawataki kuungana na chama kingine ni hiari yao, wewe kazi yako ni kunishauri lakini usinifute kwa sababu nimekataa ushauri wako.

Kwa hiyo, napenda mamlaka haya ya kufuta yaondolewe "*unless*" unaniambia kuna sharti fulani juu yake kwamba, labda ninashauri kwa kutaka kukuokoa wewe unakataa, naweza kukufuta, lakini kama mimi nafanya kazi vizuri halafu unanishauri unaniambia hapana tukiungana na mwenzangu huyu hatutafanikiwa usiniondoe tukifanya hivyo tutakuwa tumeingilia uhuru wa Vyama vya Ushirika. Kama mlivyoweka kwenye jedwali kule kuna hiyo *International Cooperative Alliance (ICA)*, kuna masharti yake kwamba, Vyama lazima viwe vya hiari, sasa ukinilazimisha niungane na chama kingine sioni sababu ya kunilazimisha. Kwa hiyo, naomba kifungu hiki kiangaliwe upya na kifanyiwe marekebisho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Kifungu kingine cha 130(3) ukurasa wa 76. Napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara na Waziri kwa ujumla, kwa kubainisha kwamba, kanuni za Vyama vya Ushirika zitatungwa kwa Kiswahili. Napenda kuwashukuru na mfanye hivyo ili wanachama waweze kuelewa kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye kifungu kingine cha 15(4), hapa nataka nitoe pongezi tu kwamba, Muswada au sheria hii inatambua Vyama vya Ushirika katika shule zetu na kwamba kila shule ambayo ina mpango wa kuanzisha Chama cha Ushirika inaweza kuanzisha na sheria hii inatambua ushirika wa namna hiyo. Napenda kupongeza kwa hatua nzuri ambayo imechukuliwa, shule zitakuwa na uhuru wa kuanzisha Vyama vya Ushirika na si suala la kuanzisha Vyama vya Ushirika, itakuwa ni kama *training ground* kwa ajili ya wanachama wa baadaye. Kwa hiyo, napenda niwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ya kwenye Muswada, naomba niende haraka haraka kwenye mambo ya jumla. Pamoja na sheria hii nzuri kutungwa na inaweza kuhakikisha kwamba Vyama vitafululiwa lakini sheria peke yake haitoshi, ni

lazima tuifanyie kazi na upande wa Serikali ndio wenye kazi kubwa. Napendekeza mambo yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, usimamizi, tatizo moja kubwa ambalo tunapata katika Vyama vyetu vya Ushirika ni usimamizi na hapa kwenye usimamizi napenda nisisitize zaidi juu ya ukaguzi.

Naishukuru Wizara kwa kupendekeza kwamba, ukaguzi ni lazima na pia napenda niipongeze Serikali kwa kuweka, kulikuwa na kifungu cha *central fund* sasa hivi kimebadilishwa kinaitwa *inspection fund*, kwa hiyo, hii *fund* nafikiri itakuwa ndio ufumbuzi wa suala la ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Nategemea kwamba, *fund* hiyo itatumika kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napendekeza kwamba, baada ya ukaguzi hatua zichukuliwe na hapa tusionene haya na wala tusilindane, Vyama Vingi vimekufa kwa sababu tunaoneana haya na tunalindana. Kwa hiyo, naomba hatua za dhati kabisa zichukuliwe baada ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Watanzania wote waweze kuunda vyama hivyo na viweze kuimarika, ni muhimu itolewe elimu kwa wanachama wote na elimu kwa viongozi.

Napenda niishukuru Serikali na Wizara kwa ujumla na Waziri kwa kupendekeza kwamba, baada ya uchaguzi viongozi lazima wapewe mafunzo iko kwenye sheria. Kwa hiyo, napenda niwashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira limekwishatajwa, sheria hii haiwezi kutekelezeka ama Vyama haviwezi kuundwa kama hatuna Maafisa Ushirika. Wizara ilikwishaahidi kwamba, itaajiri Maafisa Ushirika 300 mpaka leo hawajaajiriwa. Msingoje sisi tukae tuombe vibali vya kuajiri, muwalete hawa Maafisa Ushirika kwenye ngazi ya Wilaya ili tuweze kuanzisha Vyama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kusema ni kwamba, kuna Mikoa mingine ambayo vyama havipo au ni dhaidu sana kwa mfano, Mkoa wa Dodoma. Tunaomba tutoe kipaumbele katika Mikoa hiyo pamoja na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nirejee kwenye hili jedwali la masahihisho lililotolewa katika ile (a) anasema *in the table of contexts*, hiyo *item* ya kwanza ina makosa muirekebishe. Inasema *in item 67*, haiwezi kusomeka 67 kwa sababu hiyo unayotaka ku-*delete* namba 66 haipo kwenye *item 67* iko kwenye *item 68*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na napenda niwapongeze kwa kazi nzuri ambayo imefanyika, ahsante sana. (Makofi)



**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nijaribu kuchangia Muswada ulio mbele yetu. Napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii na ninaamini kabisa kwamba, hoja hii imechelewa tulikuwa tunaitegemea tuipate mapema zaidi ili tuweze kurekebisha ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kusema kwamba, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Ukitazama kazi zilizofanywa na Vyama vya Ushirika kule tulikotoka, mzee wangu, shemeji yangu, Mheshimiwa George Kahama, yeye anafahamu sababu hawa ndio walikuwa nguzo ya ukombozi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kazi nyingi sana zimefanywa na ushirika na nafikiri kwamba, wakati mwingine tusibwate na kuutukana ushirika sababu ushirika ndio ulifanya kazi nzuri ya kusimamia hata ukombozi wa Tanzania na Afrika nzima. Kwa hiyo, kwa wale wote waliofanya kazi hii, napenda kuwapongeza na wamekuwa ni *hero* kwa kutufikisha hapa tulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kusema kwamba, pamoja na sheria hii kuanzishwa sasa ni vema Wizara hii ijaribu kuona kwa nini ushirika tuliokuwanoa na uliokuwa na nguvu zaidi uliokufa. Tusikubali kuzika mambo ya nyuma, ni vema tukayafanyia utafiti halafu tukajenga ushirika tunaotaka kuujenga sasa hivi kutokana na matatizo yale tuliyokumbana nayo mpaka tukafika hapa. Sababu ilikuwa inajulikana kabisa kwamba, ushirika tuliokuwa nao hapa Tanzania kwa mfano, kwenye upande wa *Lake Zone, Victoria Federation* ilikuwa ni ushirika *number one* kwa Afrika nzima. Sasa tusikubali kusema kwamba, wamekufa tusahau, ni vema tukafanya utafiti kwa nini walikufa na mapungufu yaliyosababisha kifo tuyajue na hatimaye tuone namna gani tunaweza kufufua ushirika wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina upinzani kabisa katika Muswada huu, kama nilivyosema nauunga mkono hoja. Nilikuwa natazama mahali pamoja tu palipokuwa panasema kwa Kiingereza kwamba, hasa wakati wanapofanya uchaguzi mkuu, *by exclamation or by the show of hand*, lakini nimeona kifungu kile kimeondolewa na nimefarijika sana sababu kifungu hicho kilikuwa kinawapa nguvu wenye hila ya kuendelea na uongozi kwenye Vyama vya Ushirika.

Ilikuwa kama tunafanya uchaguzi kwenye *hall* kama hili hapa wanaweka watu kumi, kwenye kona hiyo kumi, halafu baadaye mtakapofika kwenye uchaguzi ile *hall* yote inasema waendelea na hicho kifungu. Mimi nilikuwa nakiwinda, kwa bahati nzuri mmekitoa kwa hiyo, *this is excellent*, nawapongeza sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, wakati mwingine lazima tuone tulikotoka kuna makosa, tulikuwa na sheria nzuri sana za ushirika lakini kuna makosa tuliyoyafanya sisi viongozi wa Bunge, Wakuu wa Mikoa, Mawaziri hata wengine wamefanya makosa katika kuangamiza ushirika na tunafikiri kwamba, sasa hivi sheria hii inavyotungwa lazima tuiheshimu. Kule nyuma ushirika umechemsha kwa sababu ya baadhi ya waniasia kutumia ushirika na viongozi wa Serikali katika matatizo ya kujineemesha na hili tunaomba Mheshimiwa Waziri, ulisimamie, uhakikishe tunakaa

kwenye msingi sababu ushirika mwingine umeuliwa na watu na kwa bahati nzuri wengine bado tunao.

Pia nafikiri ile tabia mbaya tuliyokuwa nayo kwa mfano, mambo ya siasa kuyaingiza kwenye Vyama vya Ushirika tuachane nayo, viongozi wa Serikali kutumia ushirika katika kubebana kwa mambo mbalimbali tuyaache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba niseme kwamba, ni lazima ushirika tuenzi, kwa mfano, makosa yalikuwepo na kutokana na tunapokwenda kuna makosa yalifanyika, ukichukua wakati wa uhujumu uchumi, mambo yaliyofanyika wakati wa uhujumu uchumi tuombe kitu hicho kisifanyike tena sababu Mameneja wetu wa ushirika walikuja kufukuzwa siku moja, hawakupewa nafasi ya kujieleza hata ya kukabidhi mali wanaambiwa ondoka. Hii ilikuwa mwaka 1983. Mwaka 1976 wakati Vyama vya Ushirika vinahamishiwa mamlaka za mazao viongozi walifukuzwa kama fisi, hawakupewa nafasi ya kujitetea hapakuwa na *handing over*.

**MBUNGE FULANI:** Kama kimburu.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Kama kimburu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika umefanya kazi kubwa, vita vya Uganda tusingeshinda bila ushirika. Nakumbuka vita vya Uganda wakati vimeanza nilikuwa Mhasibu Shinyanga.

**MBUNGE FULANI:** Ukila fedha?

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Hakuna, nilikuwa sili fedha, waliokuwa wanakula fedha, hela za rushwa zimewamaliza wale wote waliokula rushwa na wote hawapo mpaka kesho, *check your list, I am telling you if you are a thief you will die very soon.* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuachi matatizo ya kufanya vitu vibovu vibovu hivi, hata mkitunga sheria nzuri kabisa, mimi naamini kabisa kwamba, mtu ukiweka saini ya *contract* hata kwa wino wa damu, bado utapoteza kama mtu sio mwaminifu. Kwa hiyo, nafikiri kwamba lazima tuboreshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka vita vya Uganda, wakati tumekopa hela Benki, vita vya Uganda vikaja halafu magari yote yalirudi *scrap*, hakuna mtu aliyeyalipia halafu kule kwetu kwenye biashara ya pamba ikaoza na hakuna mtu aliye-*compensate* lakini leo mtu anaweza kusimama hapa akasema kwamba, watu wa ushirika ni wezi, lakini watu wa ushirika wamesaidia, nakwambia kama tusingekuwa na ushirika, Iddi Amin angefia hapa akatawala Tanzania, *you are laughing instead of crying.* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie suala la *policy* ya Serikali, *devaluation* imeua mashirika yetu ya umma, imeua ushirika lakini leo watu hapa wanadiriki kusema kwamba, kuna wezi kwenye ushirika, hivi mashirika ya umma

yamekufa nani ameiba ila ushirika ndio kuna wezi? Ninachosema ni kwamba, tumefika mahali fulani lazima tukae pamoja na kurekebisha. *Devaluation* imeua watu wengi, unajua mimi nakumbuka wakati nikiwa *Chief Accountant* wa *SHIRECU* mwaka 1986, *exchange rate* ilikuwa ni *fixed exchange rate*, Julai, 1986 wakabadilisha ile *exchange rate* iwe *fluctuated* ikatoka 17 kwenda 41, ni asilimia kubwa sana iliyopanda, lakini tulipoomba Serikali kwamba, itufanyie *compensation* ilikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya maendeleo ni ndefu na kuna mapungufu na matatizo mengi na tukianza kusema kwamba, huyu ndiye amesababisha hii na huyu ndiye amesababisha hii tutaishia pabaya.

**MBUNGE FULANI:** Tutatoana macho.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Tutatoana macho kabisa kama unavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umekwenda na ninapungukiwa na muda lakini napenda niseme, ushirika tunaouanzisha sasa urudie kazi za ushirika. Wakati mimi naacha ushirika Shinyanga, *SHIRECU*, tulikuwa tuna biashara, kwanza, biashara ya ununuzi wa mazao, uchambuzi wa pamba, ukamuaji mafuta, maduka (*distribution*), biashara ya kukoboa mpunga, biashara ya uchukuji. Ukitazama ushirika uliopo hivi sasa, hata Shinyanga mimi wakati naondoka niliwaambia kwamba, msipozingatia hizi kazi, mtakufa na kweli nafikiri watakufa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu wale *competitors* wanao-*compete* na ushirika pale Shinyanga, mimi nina *competitors* wanao-*compete* na ushirika, lakini wao hawafanyi kazi moja, ukiwatazama wale wana *oil milling*, *SHIRECU* imefuta *oil milling* ili wauze zile mbegu wapate *commission* pale. *Competitors* wao wana maduka, *SHIRECU* hawana na ukiwa na maduka na *distribution wing* kama mtu ameua ng'ombe zile hela utazipata, kama mtu ameua kuku zile hela utazipata, maana atakuja kununua sabuni kwako. Kwa hiyo, ushirika lazima urudie zile kazi ambazo zilikuwa ni misingi ya ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nilitaka kusema kwamba, huwezi kuchanganya fisi na kondoo, lazima mmoja ataliwa. Ushirika pamoja na *privatization*, hata ukitazama kwenye *Rochdale Principle*, huwezi ukachanganya hivi vitu, lazima tuchague kitu kimoja tukubaliane kama ushirika ufe au uwepo, wale wengine lazima wawepo sababu ile *difference* ya *interest*. Leo kulikuwa na swali hapa aliuliza ndugu yangu Mheshimiwa Mulyambatte kwamba, ushirika pamoja na kusema kwamba, upo lakini ushirika nafikiri umekufa. Lazima tukae tukubaliane, *we have to go by principles* na tukisema kwamba, maneno ya nini itatuletea matatizo. Mimi nilikuwa nafikiri kabisa kwamba, kama tunataka ushirika tukubali na kama hatutaki tukubali. Uganda sasa hivi ushirika ulishakufa lakini ninaamini kabisa kwamba, kama ushirika utakufa, *we will go back to colonialism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa wanunuzi kwa mfano, wa pamba kule kwetu Shinyanga, kwa bahati mbaya juzi tumepata matatizo makubwa sana, kuna *ginnery* za

pamba zimeungua moto. Halafu baadaye pale *center* wanapoweka marobota pale pakaungua moto, lakini jinsi ilivyoungua moto pale *is a question to be answered* na kama hatuwezi kupata jibu baadaye kilimo cha mazao mbalimbali kitakufa sababu pale imeungua moto *godown* ambayo imejengwa na ile *investment* ilikuwa imejengwa na *Lint and Seed Marketing Board* kwa miaka ya nyuma na *investment* yake ni kubwa na wakati mwingine siyo rahisi kuelezea ulivyowaka ule moto, lakini inavyoonekana Serikali ya Mkoa ilisema kwamba, *there was collusion*. Kulikuwa na *mangumburias* (mambo yasiyoeleweka) na kama ikionekana kulikuwa na *mangumburias*, wale watu binafsi wanaonunua pamba katika nchi hii na *mangumburias*, watu binafsi hawatapewa hela na wale wanunuzi wa nje, kwa hiyo, ushirika *is the answer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimalizie kwa kusema kwamba, Mfuko wa Udhamini, uongezwe ufike mpaka shilingi milioni mia moja. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika kujadili hoja iliyo mbele yetu. Nampongeza sana Waziri, pamoja na wasaidizi wake na wataalam wa Wizara, kwa kutuletea Muswada huu wakati huu. Wenzangu wamesema ni wakati muafaka na mimi nasema nawaunga mkono kwamba, ni wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilosa, ushirika hivi sasa tunaweza kufananisha na mgonjwa aliye katika chumba cha wagonjwa mahututi, unahitaji kuokolewa usife. Tunaona mali za ushirika zinauzwa kwa mfano, pale Gairo kuna ghala moja kubwa la ushirika limekwishauzwa na ndivyo ilivyo kwa mali nyingine, magari yameuzwa, nyumba sehemu nyingine zimeuzwa. Kwa hiyo, mimi naamini tukipitisha Muswada huu na sheria mpya ya ushirika ikitekelezwa kama inavyokusudiwa tutauokoa ushirika hapa nchini, hivyo naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni mjumbe katika Kamati iliyoujadili Muswada huu, sitakuwa na mengi ya kusema ila nitajaribu kusesitiza tu mambo machache yaliyomo kwenye Muswada na Muswada huu wenye lengo la kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika katika wakati huu ambao tumo katika uchumi unaoendeshwa kwa nguvu za soko na ushindani. Hivyo, Vyama vya Ushirika vitakabiliana na ushindani mkubwa sana na visiposaidiwa katika ushindani huu vitapigwa rungu na vitakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika una umuhimu wa pekee Vijijini. Ushirika ndiyo taasisi iliyosaidia kuleta uchumi wa fedha maeneo ya Vijijini. Katika ununuzi wa mazao Vyama vya Ushirika viliweza kuwafikishia wananchi wa kawaida fedha nyingi sana, watu wakajaa mapesa huko Vijijini kutokana na ushirika na ndivyo ilivyokuwa katika karne iliyopita katika maeneo ya Ziwa Victoria kama vile Mwanza, Kagera na vile vile Kilimanjaro na Mbeya. Tunajua kabisa kutokana na ushirika wenzetu wa maeneo hayo waliweza kusomesha watoto wao hata kwenye ngazi ya Chuo Kikuu. Mimi

nilipokuwa Makerere, nilikuwa na vijana waliotoka katika maeneo hayo waliokuwa wanasomeshwa na ushirika katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ushirika, tunazungumzia namna ya kuwafanya Watanzania walio wengi, wawe wawekezaji katika uchumi na ushirika ndiyo njia ya hakika ya kuwawezesha wanachama na wananchi wanyonge kiuchumi na hii inaendana na azma iliyotamkwa wazi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Silaha ya wanyonge ni umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika tunaoufufua lazima utoe fursa kwa lugha ya kitaaluma ujasirishi na ujasiliamali wa biashara. Ushirika uhusishwe na shughuli za uchumi siyo katika kilimo na ufugaji tu, lakini vile vile wavuvi na wauza samaki, wachimba madini wadogo wadogo, maseremala, waoka mikate na mimi katika Jimbo langu kuna wauza maharage na viazi mnaowaona barabarani, wale wanastahili kuwekwa pamoja na kuhamasishwa waunde vyama vidogo au vilivyoitwa kwenye sheria pengine vile *Pre-Registration Cooperative Societies* ambavyo baadaye vinaweza kuwa Vyama kamili vya Ushirika ili mradi watu waweze kuunganisha nguvu zao. Tuchukulie ushirika kama njia ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inavitambua Vyama Vidogo Vidogo vya Akiba na Mikopo. Hivi ndiyo vyenye mwelekeo wa kuwa vyombo imara vya *SACCOS* na mfumo huu wa Vyama vya Akiba na Mikopo umedhihirisha kuwa ni endelevu na unaweza kuanzishwa na wananchi Vijijini na kuwaletea huduma za kibenki huko huko Vijijini. Sisi pale Gairo tunashukuru tunayo *SACCOS*, ambayo imeziba pengo la Tawi la *NBC* lililofungwa. Huu siyo tu ukombozi wa wananchi wa Gairo na ninavyojua hata wananchi wa Wilaya za jirani za Kiteto na Kongwa wanafaidika. Vile vile niseme kwamba, hata huu uanzishwaji wa *SACCOS* ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu limesisitizwa sana na wenzangu waliokwishachangia na mimi natilia mkazo juu ya suala la elimu, kwa kuwa kukosa elimu imekuwa ni kikwazo kikubwa sana cha maendeleo ya ushirika. Watu wanasema mtu asiye na elimu anakuwa mtumwa wa mazingira na atashindwa kujiletea maendeleo. Hivyo, elimu ya ushirika na stadi za biashara ni vigezo muhimu sana katika kufufua ushirika. Wanachama wa ushirika wanahitaji elimu, wanahitaji kuelimishwa, wanahitaji elimu za biashara waweze kujenga uwezo wao wa uwekezaji na kuwa wajasiri katika kutafuta fursa ya kufanya biashara nzuri na kubwa. Pia wanahitaji elimu ya uzalishaji na utafutaji wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la masoko ni la muhimu sana. Hivi sasa sisi wengine tukisimama katika Majimbo yetu tukianza kuzungumzia juu ya ushirika na kuwahimiza watu wazalishe mali, swali watakalokuuliza "masoko yako wapi? Wengine watakukabili na risiti za mazao yao ambayo walikwishauza huko nyuma hawajalipwa mpaka leo. Kwa hiyo, hii inafanya hata ule uhamasishaji wa ushirika kazi yake kuwa ngumu. Lakini ni mategemeo yangu suala la ushirika likitiliwa mkazo na watu wa ushirika wakaelimishwa inavyostahili waweze kusimamia ushirika wao kwa ukamilifu,

tutapata mafanikio katika ushirika. Bahati nzuri suala la elimu ya ushirika halijitokezi vizuri lakini limezungumziwa kidogo katika ibara ya nne, sehemu ya pili na kifungu kidogo cha (v) na vile vile katika ibara ya 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo linastahili kusesitizwa katika ushirika ni suala la uongozi na mfumo wa madaraka. Haya ni mambo muhimu ya kuzingatiwa na bahati nzuri yamezingatiwa kwa ukamilifu katika Muswada huu. Ushirika ni chimbuko la uongozi wa kidemokrasia na utawala. Haishangazi kwamba, viongozi wengi wa kisiasa walijifunza mbinu za uongozi katika ushirika. Tunayo mifano hai hapa Bungeni, Waziri mtoa hoja na Naibu wake na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani ni wanaushirika waliobobea. Kwa kuwa hivi sasa tunachukulia kwamba, ushirika ni chombo cha biashara tunahitaji aina mpya ya viongozi ambao hawaongozi kwa busara tu au kwamba, ni watoto wa wajomba, tunahitaji viongozi wa ushirika wanaoongoza kwa uwezo wao wa kibiashara na uwezo wa kitaaluma wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kuona ni viongozi wanaokubali kuongozwa na wanachama, wanaokubali kuachia madaraka kwa mzunguko na hii imo katika Muswada. Wanaoongoza kwa misingi ya utawala bora, yaani uwazi, uwajibikaji, kutabirika na kuwashirikisha wananchi na wanachama wa ushirika katika maamuzi muhimu ya ushirika wao. Lazima tujiepushe na ushirika unaoundwa kwa kushinikizwa au kwa kulazimisha kama ilivyokuwa zamani, Kijiji kizima mnaambiwa kwamba, hiki kitakuwa ni Chama cha Ushirika. Vile vile lazima tuondokane na viongozi wabadhirifu na wasiofuata maadili, hawa wakiachiwa watauvuruga ushirika na watadhibitiwa tu ikiwa wanachama watakuwa na uwezo wa elimu kuweza kuzuia ubadhirifu na wizi. Huko zamani tulikuta wanaushirika wanasomewa mapato na matumizi, wanabababishwa, hawaelewi, mwisho wanaambiwa unaona upande wa matumizi na mapato vinalingana, mambo sawasawa kumbe humo ndani wenzao wamewaibia wenyewe wanabaki kusema tu ndiyo, sawa, ushirika wetu unaendelea. Kwa hiyo, Maafisa Ushirika wa Wilayani wasiwe vinara wa kusimamia sheria na miongozo bali wawawezeshe wananchi au wanaushirika kujikagua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha shirika la ukaguzi pamoja na kuwa Mkaguzi wa Nje, kitoe fursa ya ripoti za ukaguzi na uongozi kuona kwamba, zinapelekwa kwa wanachama wenyewe na kwa lugha iliyo rahisi waelewe. Ni kwa kufanya hivyo tu ndiyo wanaweza kuzuia wizi na ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niseme kwamba, lazima tuone kwamba, ushirika unakuwa ni huru, unaoendeshwa na kusimamiwa na wanachama wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, narudia tena kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na hasa nafasi hii ambayo ni adimu kwa sababu Sheria hii ya Ushirika ninavyoiona ni sheria ya kihistoria na nilipopata nafasi

ya kuzungumzia, naona angalau na mimi nimekuwa *booked* kwamba nimechangia. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niipongeze Wizara inayohusika na ushirika, kwa kutekeleza program yao ya *Cooperative Reform*. Kwa kweli ndivyo tulivyokuwa tunatazamia kwamba baada ya kuundwa Wizara ya Ushirika, pawepo na mabadiliko ya namna hiyo. Kwa hiyo, naona ninyi mnakwenda *the right direction*, nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii nimeipitia, imezingatia mambo mengi hususan, imezingatia historia ya ushirika, uzoefu wake, matatizo, halafu imezingatia ni nyanja zipi za ushirika ambazo zilipata mafanikio huko nyuma. Kwa hiyo, inalenga kuboresha ushirika katika nchi hii. Vile vile wale wanaokumbuka ushirika wa zamani, nadhani watakumbuka kwamba, matatizo makubwa yalikuwa hasa kwenye (*vision*), mtazamo wa ushirika wenyewe ulikuwaje.

Sasa *vision* ya zamani tunajua wote kwamba, ilikuwa inatazama kwamba ushirika ni mahali pa kuanzia kwenda kwenye ujamaa kamili na ushirika wa sasa hivi nadhani *direction* yetu ni kwamba, tunataka kumkomboa mwanachama kutokana na matatizo yake mwenyewe na vilevile kumuongezea uwezo wake wa kuishi vizuri katika dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Ushirika huu wa sasa ambao Sheria hii imetungwa unatofauti kidogo na Ushirika wa hapo katikati ambao ulikuwa unazingatia kutekeleza Azimio la Arusha. Kwa hiyo, kama tunataka yawe hivyo, lazima maamuzi ya Serikali nayo yabadilike kidogo. Kwa mfano, nilikuwa nafikiri sasa kwamba, baada ya kupitisha Sheria hii, Serikali ingeweza kuona kwamba, Ushirika ni mkakati mmojawapo wa kuondoa umaskini. Vilevile Ushirika utazamwe kwamba, ni mahali pazuri pa kujifunza kuendeleza demokrasia. Vilevile Ushirika nafikiri utazamwe kwamba, ni mahali pa kuwawezesha wananchi wa Tanzania kushiriki katika uchumi wa nchi hii.

Kwa hiyo, tunasikia sikia hapa kwamba, kuna sera ya uwezesaji itakayokuja katika nchi yetu. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, sasa ni nafasi nzuri sana kwa Serikali katika hiyo sera ya kuwawezesha wananchi wa Tanzania kutumia nguvu zao zote katika kuendeleza Ushirika na ndiyo peke yake itakayoweza kuwasaidia wananchi wa Tanzania kushika uchumi wa nchi hii. Vinginevyo hakuna Mtanzania wa kawaida anayeweza kushika uchumi wa nchi hii bila kushirikiana, sasa hiyo sera ya uwezesaji ifanye hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeona kwenye *section 6* hadi *7*, Serikali imeshauriwa au imeelekezwa kwamba, itaweka mazingira mazuri kuviwezesha Vyama vya Ushirika kustawi katika nchi hii. Sasa haya mazingira mazuri ni yapi? Nafikiri nililolizungumza hapo mojawapo kubwa ni kufanya Vyama vya Ushirika vifaidike na utaratibu wa *Micro-Finance*, bila kuwa na utaratibu mzuri wa Serikali wa kuwawezesha *Micro-Finance* kusaidia Vyama vya Ushirika itakuwa matatizo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wamezungumzia hapa habari ya SACCOS, sasa nilikuwa nafikiri zile SACCOS mwanzo wake ni mzuri kwa sababu zinatokana na wanachama wenyewe. Wanachama wanajaribu kuweka tabia ya kujiwekea wenyewe akiba, kwa hiyo, tabia hiyo ni nzuri kwa sababu wanakuwa na uzoefu wa kujiwekea akiba yao. Sasa Serikali ingeingia hapo kuwasaidia na kuwawezesha hao wanachama walioanza kujiwekea akiba wenyewe ili waweze kufanya vitu vikubwa kidogo kuliko sasa hivi katika hali yao ya yionge kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri vilevile kuna makato mengi yanayotokana na Vyama vya Ushirika kuuza kwenye masoko pengine kupitia Bodi, vingetazamwa viwango vyake. Maana kuna mtu ameniambia kwamba, Vyama vya Ushirika vinapeleka Kahawa kwa ajili ya *curing* kwa mfano, sina uhakika lakini nimeambiwa kwamba, *loss* katika *curing* peke yake inakuwa asilimia 21, kwa hiyo, hiyo anabeba mkulima, *loss in curing* pia ada nyingine zinazohusika, kwa hiyo, ingelikuwa vizuri kuviondolea Vyama vya Ushirika. Kama tunaweza kuondoa kwa kipindi fulani kwa wawekezaji kutoka nje wasilipe kodi yoyote katika nchi hii, kwa nini basi Vyama vya Ushirika visiondolewi kabisa vikabaki *free*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nafikiri kwamba, hivi haiwezekani katika nchi hii tukafanya uamuzi wa makusudi, wakati tunakwenda kwenye mfumo wa soko tulitoa kipindi kizuri tu kwa ajili ya benki, kwamba wao wa-*enjoy monopoly* zile; je, haiwezekani tena tukarudisha Serikali ikaamua kwamba, kuanzia sasa ununuzi wa mazao kwenye vijiji kuwapa kipindi maalum Vyama vya Ushirika ili viweze kujijenga upya kuondoa *competition* kwa kiwango fulani. Labda tuseme kwenye ngazi ya kijiji, najua ni ngumu kwa sababu tunakwenda kwenye *direction* ya soko huria. Lakini haiwezekani tukasema kwamba, sasa kwa kuwa tunataka kuviwezesha Vyama vya Ushirika visiwe na ushindani mkubwa kama walivyosema wengine, basi tungeamua kwamba, kwenye ngazi ya ununuzi, *primary society* pasiwe na ushindani, vipewe Vyama vya Ushirika *monopoly* ya kununua kutoka kwenye ngazi ya Vyama vya Ushirika na ushindani mwingine uanze labda kwenye ngazi nyingine. Kwanza, wafanyabiashara binafsi wanatuletea tu vurugu kwenye ngazi ya wakulima kule chini na ni vurugu kubwa na ubora wa mazao unapungua sasa hivi, mpaka kahawa nyingine zinanunuliwa mbichi na kahawa nyingine hazina hata *quality* inayofaa. Sasa kwa nini basi tusiamue kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu pamoja na kwamba tuna sera ya soko huria, lakini tuwape *monopoly* hawa kidogo.

Lingine nilikuwa na wasiwasi na idadi ile ya wanachama kuanzisha Vyama vya Ushirika, hasa kwenye *Savings*, kuanzia na ile idadi ya watu 20. Lakini baadaye nimesoma haraka haraka nimegundua kwamba, panaweza kuwa na *probation* kwa hiyo watakuwa *covered* kule, kama watu 10 wameanza, basi wataanza kwenye *probation* kwanza, halafu baadaye wanakua wale wanaendelea kukua halafu wanapata *registration* ya kudumu.

Vilevile nilikuwa nafikiri kwamba, kwenye *specialize* nako ile *minimum requirement* ya uanachama hii nayo naona ni ngumu kidogo. Kwa sababu *suppose* tuko



watatu, wanne, tunataka kuanzisha biashara ya Uwakili (*Advocates*). Kwa hiyo sisi ma-*advocate* lazima tukae watu zaidi ya kumi, yaani mtafutane ma-*advocate* kumi ndiyo muanze kuunda Chama cha Ushirika, nafikiri hii nayo kwa *specialize* nafikiri mngeishusha kidogo hapo.

Halafu lingine nafikiri uzoefu umeonyesha ili *production* ya mazao iwezekane katika nchi hii, lazima pawe na suala la pembejeo lishughulikiwe na Vyama vya Ushirika. Wakati hizi *union* zilipokuwa zinanunua mazao na kuleta pembejeo vijijini kulikuwa na uzalishaji wa hali ya juu sana, kuliko sasa hivi pembejeo za kilimo au Vyama vyetu vya Ushirika vinanunua tu mazao bila kuleta pembejeo kwa ajili ya uzalishaji, kwa hiyo, haimsaidii sana mkulima. Kwa hiyo, nafikiri hata kwenye hizi *Micro-Finance* na uwezeshaji zingine zingeweza kupewa wakafanya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba, sheria hii ni sheria ambayo inaleta mapinduzi makubwa katika kujenga Ushirika katika nchi hii na kama nilivyosema kwamba, imezingatia historia, mafanikio na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada ulioko mbele yetu. Labda nifanye kama wengine kwa utaratibu kwamba, tunashukuru kwa kutuletea Muswada huu. Lakini vilevile Muswada huu unazungumzia Ushirika wa aina mbalimbali. Upo Ushirika wa wakulima, upo Ushirika wa Waheshimiwa Wabunge, hata kama haikutajwa kwamba Waheshimiwa Wabunge tuwe tunachangiana shilingi 500,000/= kila kikao, upo Ushirika wa walimu na mambo kadha wa kadha kama sikosei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa Arusha nilikuwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw', nilikuwa nimevaa nguo hizi, sasa wakasema wewe mbona unavaa nguo za *green*, wewe ni CCM, nikasema hapana, mimi navaa nguo hizi za *green* kwa sababu mimi ni mkulima, ndiyo maana nguo zangu zinakuwa hivi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitazungumzia Ushirika unaohusu wakulima. Sasa katika haya ya wakulima, labda nitangaze *interest* yangu, niliwahi kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Wilaya ya Karagwe, *very powerful Union* na tulitofautiana na wenzangu na niliwaambia wakanibishia.

**MBUNGE FULANI:** Kikafa?

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Hakikufa kipo. Lakini yale niliyowaambia waliponibishia waliondoka. Sasa katika haya tuna mazoea na binadamu, sisi kwetu tuna methali inasema, kwenye nyumba za nyasi za tembe zile, unakoka moto huku sasa kila siku mjusi anaona moshi. Sasa siku moja nyumba inaungua, mjusi akaambiwa wewe nyumba inaungua, akasema toka hapa inaanguaje, si moshi kila siku

tumeuzoea, kwa hiyo, amezoea sasa nyumba ikaungua na mjusi ukaungua mle. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najua watu tunasimama hapa tunazungumzia kuhusu Ushirika. Kwa sababu ya mazoea siyo ya miaka 40 ya uhuru, ni kwa sababu ya mazoea ya tangu ukoloni kwamba, Ushirika umekuwepo, ulisomesha watu na nini na nini. Lakini ulimwengu unabadilika, sasa unapobadilika lazima na sisi tuliangalie hilo. Kwa hiyo, tunayozungumza hapa tutatofautiana na watu wengine, mimi kwa mtazamo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ushirika tunaotaka kuujenga nchini Tanzania na misingi tunayoiweka na watu wengine wananiambia sasa wewe Mutungirehi unampinga kaka yako, Mzee George Kahama, mnatoka Wilaya moja na mimi nawaambia hapana, kimsingi kaka yangu George Kahama, hana Muswada wa kwake, huu ni Muswada wa Serikali na ni Muswada wa mfumo mzima. Kwa hiyo, mimi ninapopinga napinga *system* nzima na mfumo mzima wa Serikali, siyo Mzee George Kahama. Kwa hiyo, haya ninayoyasema siyaelekezi kwa Mzee George Kahama, ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, nayaelekeza kwa *system* nzima ya Tanzania kwamba, tuache mambo ya mchezo ya kuwachezea watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Ushirika tunaouunda kwa walimu sawa, ushirika wa Wabunge sawa, ushirika wa wafanyabiashara sawa, ushirika wa Waganga sawa, sasa wakulima hawa waliniambia wakati nahutubia wakasema Mheshimiwa Mbunge sisi ni wa kuliwa siyo wakulima. Nikawauliza mnaliwa na nani? Wakasema tunaliwa na Chama Twawala. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa katika kifungu cha 16 cha sheria wanasema tutaunda *Primary Societies*. *Primary Societies* zitaunda Chama Kikuu kwa maana ya *Secondary Society*, the *Secondary Society* zitaunda *Apex Societies*, *Apex Societies* zitaunda *Federation*. Sasa Chama cha Msingi, Chama Kikuu, sijui *Apex*, *Federation*, Bodi ya Kahawa, wote hawa ili wajiendeshe katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kila kilo ya korosho, kilo ya kahawa, kilo ya pamba, wanataka wakate pale ili wajiendeshe wale wote pamoja na magari na vitu watakavyovitumia. *(Makofi)*

Sasa unategemea katika mazingira kama haya, huyu mkulima bei yake ana *realise* lini *to the maximum*. Chama cha Msingi ile *management* wanakula pale mameneja wote wa *Union* na wengine wote, sijui *Apex* wote wanakula pale, ukienda *Federation* wote wanakula pale, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pamba, Bodi ya Korosho, wote wanakula pale. Akitoka mnunuzi binafsi labda *Rely and Traders Company*, yeye hana huu mlolongo, anakwenda ananunua pale kwa bei ambayo inakubalika, kwa sababu hana hii milolongo yote. Kwa hiyo, bei yake itakuwa ni kubwa na atawalipa hawa kwa manufaa ambayo yanakubalika. Kwa hiyo, kwa kipengele hiki, mimi nadhani *we have to revisit our decision* na ninafurahi Waziri, Mheshimiwa Sir George Kahama, aliwahi kwenda Uganda kule, mtaalamu mwenzake Museveni alikuwa anafundisha pale Ushirika, alikwenda pale akasema hii mnawanyonya watu akaifuta, Mheshimiwa George Kahama,

anaijua vizuri, sasa kwa sababu yuko ndani ya Serikali akiyasema hayo watamrukia. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kifungu cha 77 siyo tu kwamba *Union* wako pale, sijui *Federation* wako pale na *Apex* wanasema *Federation* itaunda Mfuko wa *reserve*. Sasa waunde Mfuko wa *reserve fund, federation* ndiyo iuendeshe, unazungumzia kukata kwenye kilo ya mkulima, mkulima hana *NPF*, unakata tu unatumbukiza zikifa huku, wala hakuna anakoshtaki ndiyo maana Mheshimiwa mmoja hapa akasema ukiangalia madeni wanayodai Vyama vya Ushirika na haya Makampuni yote ya Ushirika ni makubwa sana kuliko faida iliyowahi kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mantiki hii hawa wakuliwa, jana tumepitisha hapa sheria ya wafanyakazi ku-*negotiate* na Serikali. Hivi wakulima wana-*negotiate* lini na Serikali *it is unfortunately* kwamba, huwa hawaandamani, huwa hawagomi na huwa hawaelewi. Vinginevyo kwa sababu ni asilimia 80 ya *population* ya Watanzania wangewaondoa madarakani. Hamuwezi mkawa mnawanyonya watu na mnawawekea vitu vya kuwanyonya, mnawanyonya, mnawanyonya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wameunda hivyo wakipata hasara, Mheshimiwa Talala Mbise, alisema Ushirika wao ulipata hasara, akaomba Serikali iwafidie haikuwasikiliza. Mimi niliwahi kuleta hapa madai ya Kagera, bahati nzuri waliwalipa. Sasa wengine hamkuwalipa, kila mwaka wao ni hasara, hasara, kwa sababu ni wa kuliwa. Wizara ya Ushirika na Masoko ina bahati mbaya kama mtu mwenye wanawake wawili. Sasa kama mmoja ndiyo unaangukia kwake yule mwingine sasa ananung'unika nung'unika. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona sera hapa ama sheria ama Muswada ambao una-*propose* kuhusu masoko ya kuwasaidia Watanzania, haijawahi kuletwa, lakini ni Ushirika na ni Wizara vile vile na Waziri ni mmoja wa Ushirika na Masoko. Sasa hizi mbinu unaziunganishaje? Kwa taaluma siyo kuona soko huria, limekopa fedha zake linataka kufanya *business*, hayataki mchezo na hawa watu wa ushirika lazima tuwalinde, lazima tuwaweke kwenye koti na lazima tuwapende! Sasa kama Waziri mhusika wewe unafanyaje na watoto hawa wawili wako chini yako? (Makofi)

Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo yanatutatiza kwamba, aah, huyu amekula njama. Sasa nadhani lazima tukae chini na mimi nataka kuwaambia na iingie kwenye *Hansard* kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utaratibu wa sheria hizi na uendeshaji wa Ushirika hivi, baada ya miaka mitano, kumi au ishirini, itafanikiwa kujenga Ushirika wa mfano, katika Afrika ama katika dunia na mimi nikiwa katika uongozi wa nchi hii aidha, Balozi wa nyumba kumi ama Mbunge, uniambie nijuzulu sifanikishi. Maana imefika mahali alikuwa anasema Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala hapa, waacheni watu wauze mazao yao wanakotaka, mnasema wanafanya magendo, magendo. Magendo maana yake nini, umeshindwa kumtafutia mtu soko, anapata soko lake, wewe unamwambia anafanya magendo, maana yake nini? (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa italeti fedha za kigeni. Fedha za kigeni sasa nataka kuwapa taarifa tulisomewa hapa kwenye bajeti, *foreign reserve* ya Tanzania inaweza ku-*sustain* ku-*import* kwa miezi sita, kwa sababu tunazalisha dhahabu. Sasa huo ni uongo kutoka Benki Kuu na Waziri wa Fedha yuko hapa na Wasaidizi wake. Sasa nataka kuwaambieni kama dhahabu, almasi, katani na pamba, zinachangia *reserve* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Benki Kuu kwa zaidi ya asilimia 30, wafanye utafiti wakileta hapa, wakisema ni sawa mimi najiuzulu kuwa Mbunge na wako hapa wasimame waseme Mheshimiwa Mbunge, kaa chini, tuunde Tume twende tukachunguze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapokea fedha za misaada za *HIPC* sijui na nini, ndiyo mnasema zimetokana na madini, sasa madini mnauza kule mnafanya *retention a hundred percent*, halafu mtu anataka kuuza kahawa yake, mnasema Bodi, mbona kwenye madini hakuna bodi, mbona kwenye samaki hakuna Bodi na Bodi inachukua asilimia fulani ya kahawa, inachukua asilimia fulani ya korosho wanachukua tu wanapeleka kule. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuwaondolee mzigo hawa watu, tumewadhulumu kiasi cha kutosha. Tufike mahali tulete Muswada hapa tunataka masoko, wanataka kuuza mazao wapi. Tunawakopesha wenye mitaji mikubwa, haya makumpuni na tunawa *regulate* vipi? Hapo ndipo mtu amezalisha na ameuza na amepata fedha zake anakwenda kununua ng'ombe, anajenga nyumba, ananunua matrekta anavyotaka. Sasa hayo siyo maruirui, kwa sababu sisi binadamu ndivyo tulivyo, mazoea ni kitu kibaya sana, ndiyo maana hatubadiliki, mtu aliyezoea uchafu amezoea uchafu, asiyezoea kufanya kazi hafanyi kazi, ukimwambia anakuwa mkali kweli kweli kwamba umemtukana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika misingi kama hii, sheria hii nadhani tunaipitisha hapa tunashangilia, lakini Watanzania wataendelea kuwa maskini kwa sababu unaweka watu wa Ushirika ambao wataendeleza unyonyaji, wataendelea kufanya mambo ambayo hayapo. Katika Ulimwengu ambao ni *globalized*, alikuwa anawatania Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala pale, anasema Rais anazungumza *globalization, you sell where you have to sell*, nyie mnazungumza *localization*, ooh tunanunua kwenye kikundi chetu, wewe unauza katika kikundi gani? Kikundi gani wewe unataka kuuza hayo mazao? Ni chama gani cha Ushirika ambacho kime-*computerize*, nenda *SHIRECU* pale, nenda wapi, wana *computerize what!* Ukiwauliza *process* za mazao kama ni kwenye *International Coffee Organization*, wewe *Manager* wa *KCU*, wa *KDCU* au wa *KNCU*, tuambie *process* za *next year season* kuhusu kuuza kahawa, *process* zikoje, Brazil ikoje? Hajui, halafu anapanga bei, anapanga bei gani kama siyo hewa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani pamoja na ukali wote huo, tufike mahali tukubaliane *what we need in this country* ni kwamba, *a person has to produce* halafu apate soko na masoko yako mengi na tuwawezeshe. Siku moja rafiki yangu Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje aliulizwa hapa, masoko yako wapi? Akasema: “Kule Kariakoo walitoa taarifa kwenye gazeti.” Sasa taarifa ya kwenye gazeti inatosha! *Go to America, go to Russia, go to China*, lete hapa, toa taarifa kwamba, tulikwenda kule,

wakasema korosho wanahitaji tani 10,000, tani 20,000, tani 30,000 tunafurahi, lakini ukiulizwa ukasema pale Kariakoo, Kariakoo *what does it mean? Everybody reads in the newspapers.* (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namalizia, siku moja nilikuwa nimelala, babu akaniambia: “Ukiona maua ya mti fulani yanapendeza, siyo kwamba matunda ya mti ule yatapendeza pia, kama maua yanapendeza usije ukadhani kwamba, matunda ya mti ule wa maua yanayopendeza yakishakuwa matunda kabisa na yenyewe yatakuwa matamu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana. (Makofi)

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu. Jana niliondoka nikaenda Dar es Salaam nilimuaga Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko na nikampa maoni ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, wale wachache nilioweza kukutana nao, kuonyesha kwamba, sisi tunafikiri nini katika Muswada huu. Ninapenda kabla sijaanza kuongea kwa *speed*, nitamke waziwazi kwamba, naunga mkono Muswada huu na nitaeleza. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mambo kihistoria, *you are trying to be scientific*, angalia mifumo yote, angalia mifumo ya kijamaa na angalia mifumo ya kibepari, mifumo yote miwili inatamka waziwazi kwamba, kama wanyonge wanataka kujikwamua katika unyonge wao, lazima waingie katika *cooperative development*. Hapa tunazungumza historia wala siyo ushabiki hapa. Kinachozungumzwa hapa mfumo wa kibepari una-*up hold* Ushirika, wanazungumzia habari ya *economic liability*, katika mifumo ya kijamaa wanazungumza habari ya *producer cooperative*, ni ule ushirika wa uzalishaji mali, hakuna ushabiki, yaani hapa mtu akikwambia kafanya ushabiki hapa, hajaipata *concept* vizuri. Kuna mfumo mwingine unajua huu mfumo kwa mfano, mpango, ile ni *component* ya kijamaa siyo ya kibepari. Lakini unapozungumza habari ya ushirika ni *component* ya kibepari na ni *component* ya kijamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabepari wanafika mahali wanawakandamiza hawa wanyonge na hao wanyonge wanafika mahali wanasema kujiondoa katika hali hii *inevitably* kama unataka ni lazima muungane katika ushirika. Mimi natoka Kilimanjaro, watoto waliokwenda shule wakati wa uhuru katika *Primary level*, katika *Secondary level*, katika vyuo na Vyuo Vikuu, wote walipitia katika ushirika. *Lyamungo Sekondary School* ilijengwa kupitia Ushirika, *Kibohehe Sekondary School* ilijengwa kupitia Ushirika, *Siha Sekondary School*, ni *High School* hii, zote zilijengwa kupitia Ushirika. Kwa hiyo, hakuna cha ushabiki, hapa hakuna cha kusema ni Chama cha Mapinduzi wala nini, hii *is a historical fact*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa unazungumza *the political economy of capitalism and the political economy of socialism*, siyo *politicis and economics put together* unazungumzia mahusiano ya uzalishaji mali katika eneo linalohusika, ndicho kinachozungumzwa hapa. Unasema angalia bwana, mimi nilikuwa na *orientation* ya

kijamaa huko nilikotoka ndiyo maana tunazungumza habari ya Azimio la Arusha, nimehama huko. Mimi nimesema siwezi kukaa kama kichuguu, nataka kuingia katika mahusiano ya uzalishaji mali yenye mwelekeo wa kibepari, unasema sasa nafanyaje hapa, ninachofanya nabadili taratibu zangu na ukaaji wangu ili nifanane na mwendo wa dunia, unaambiwa hamna kitu hapo. Mimi naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua ilizozichukua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunalolifanya tusilifanye hapa, sisi ni wa kubeba mizigo milele hapa Tanzania, ushirika ni kauli ya wananchi, ni kauli ya wanyonge, Ushirika ndiyo *fall back position* yako, mtu yeyote anayekutakia mema atazungumza habari ya ushirika hawezi kuzungumza kitu kingine. Tumefika mahali tumeacha watu wameingia kwenye ushirika mle, wameughasi, wameutumia kama wanavyotaka, wanakwambia wewe bwana unaweza kukaa hapa kwa miaka miwili, miaka minne, miaka 20, mnasoma *primary school* mnamwona ni Mwenyekiti wa Ushirika, nakwenda Chuo Kikuu mnamkuta ni huyo huyo. Muswada huu leo hapa unasema huwezi ukaingia mara mbili mfululizo halafu ukaendelea kuwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ambacho naweza nikakizungumza hapa kwanza, hawana kitu kinachoitwa *modes of production*, hakuna, kuna watu akina Morris Dobo, akina Takashi Takashiro, hayo maneno ni ya Kijapan, huwa yanaandikwa hivyo hivyo kama Kiswahili kinavyoandikwa kwa hiyo, unayaandika hivyo hivyo. Wote hawa akina Mart na wengine, wote walizungumzia mambo ya latifundia na nini, wamezungumzia habari ya *social economy formation*. Leo hapa tuko kwenye kipindi cha mpito, hatuwezi tukafika mahali hapa leo, tukasema leo tunavyoanza hapa ndiyo tunaanza na ushirika *proper*, hakuna, humu yataingia mabaki mabaki ya kule nyuma na huku mbele kuna *descending orders* na *ascending orders* zitakutana humo katikati. Lakini safari yetu ni kuhakikisha kwamba, tunafika mahali ambapo tunam-*empower* mkulima wa Tanzania au mwananchi wa Tanzania awe na kauli kamili katika utaratibu mzima wa kuzalisha mali. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hii sauti mimi nilishawahi kuwambieni, siyo ugomvi nataka tu kuweka msisitizo hapa, sigombani hapa. Lakini ukiona tumefika mahali tunataka kuyumbayumba, tunataka tufike mahali tuna *echoe the same sentiments*, wote kwa pamoja, tuzungumze lugha moja. Ninachoshauri hapa inawezekana kabisa leo tuakapitisha Muswada huu, tukaamini kwamba, leo tumezaliwa upya katika Tanzania na hatutegemei tena kwamba, tutakuwa na matatizo katika ushirika, tutajidanganya. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hizi *social economic formations* zina-*change in form, but in content* zinabaki vilevile. Kinachozungumzwa leo hapa, ni kwamba, ushirika tunataka kuupa pumzi mpya. Kutoa pumzi mpya kwa ushirika maana yake ni kwamba, unaupa Ushirika majukumu mapya, kupanga watu upya, kuweka kada ambayo inaweza ikaenda sambamba na matarajio ya wananchi wa Tanzania. Mkienda mkajipanga vibaya, utasema hawa wapangue kwa sababu wamekaa miaka 20, wataweka watu wao kule ndani, Ushirika ule utatafunwa pale. Kinachosemwa hapa ni nini? Utakwenda unasema kuna Mkutano Mkuu wa Ushirika, watakwenda pale,

watakaa, watafanya mkutano, wataitisha mikutano ya dharura. Mikutano ya dharura wanaipenda kwa sababu haina yatokanayo na kama huna yatokanayo, huna taarifa ya mapato na matumizi ya Ushirika, wakikutana watasema tunakutana tu hapa tutazungumzia kitu fulani na kuna nyongeza imekuja, tuondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano ya namna hiyo Mheshimiwa Sir George Kahama, aiondoe. Mkutano ni Mkutano Mkuu wa wanachama wote wakutane pale, wasome *minutes* za mkutano uliopita, wajadiliane kwa kusema tulikubaliana nini kwenye mkutano uliopita, ndicho kilichotokea katika nchi hii. Watu wawili, watatu *smart* wameingia pale, wamesoma Sheria wanajua, wanatembea nayo mkononi, ukiikuta ile sheria imechakaa, imekaa pale utafikiri alikuwa anatengeneza maandazi ilivyokuwa tu imeivaiva hivi, anakusomea kipengele hiki, unajua lazima tuwape Ushirika uwe na nguvu na nini. Naomba nitahadharishe hapa, ndani ya Ushirika tunaambiwa kwamba, washirika wale wana uhuru wa kuamua mambo yao na kufanya mambo yao kama wanavyotaka. Ushirika ule ndani yake lazima ubebe wajibu kwa wanachama na nchi yao, huwezi tu ukasema sisi ni uhuru, kwa hiyo, uza haya matrekta yote ya ushirika yamekwenda na mashamba yote uza achana na hawa wananchi sijui nini, haiwezekani hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi nimeleta mapendekezo 11 na nimeshamkabidhi Mheshimiwa Sir George Kahama na nina hakika kwamba, sitokuwa na muda, najua yataingia huko kwa maandishi na haya mengine yataingia kwa kuzungumza.

Nizungumze jambo moja, huyu mtu anayeitwa Mrajisi, anazungumzwa zungumzwa humu na huo uhuru unaozungumzwa wa kwamba, Ushirika utakuwa na uhuru wa kufanya mambo kama unavyotaka simuoni hapa. Nafurahi kwa *amendments* hizi ambazo zimetolewa hapa imejitokeza kwamba, kweli sasa tumepunguza. Mrajisi atumike tu kufanya *intervention* pale anapooni mchezo unachezwa *rough*, lakini hawezi kufika pale kwa mfano, unazungumza humu ndani, unasema mrajisi akitoa ushauri usipofuatwa hicho Chama cha Msingi au chama hicho kitawajibishwa. Lakini hatuambiwi humu ndani ya Muswada huu kwamba; je, Mrajisi akitoa ushauri halafu wakafika mahali waka-*makeup* kufuatana na ule ushauri ambao ametoa, Mrajisi anafanywa nini? Ni lazima iwe *a true way traffic system*. Wao wameshauri Ushirika hapa, halafu wamefika mahali wame-*wait up*, utatuambia kwamba ilikuwa kuwaje? Hilo nilitaka nilizungumze hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, katika huu Muswada ukurasa wa 34, kwenye ile *clause* namba 53, inasema maneno yafuatayo: "*A registered society which one of its objectives is the disposal of any article which is the produce of agriculture or animal husbandry, shall provide in its by-laws: - (a) that every member who produces any article has entered into an implied contract to dispose of the whole or any specified amount proportion or description thereof to or through the society.*" Hapa unajua anasema nini? Macho yangu mabovu yananisumbua sumbua, usije ukafikiri kwamba Kizungu, kinanipiga chenga, aah! (*Kicheko*)

Anachosema hapa ni kwamba, kama wewe umeingia kwenye Ushirika huwezi ukauza yale mazao uliyonayo kwa mtu mwingine. Leo tunazungumza nini hapa kuhusu soko huria? Ushirika ukishajiunga nao haukuruhusu tena ukaingia *contract* na watu wengine kule pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa safari iliyopita tukasema tu-*frustrate move* ya soko huria kule kwenye Kijiji ambapo ndipo tunakozalisha. Binafsi niliomba, nikasema, Mheshimiwa Waziri, chonde chonde, kwenye Jimbo langu la Siha nawaomba kabisa hii kitu inaitwa soko huria msiniletee, wenzangu wanaosema wanataka kuchukua, wachukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya miaka miwili tumepata baki na tumepata nyongeza. Tumepata shilingi shilingi tu kwa kilo moja, siyo hela nyingi, baada tu ya hiyo *move* tuliyoifanya hapa.

Mheshimiwa Sir George Kahama, leo ukienda tena, *already* tunao watu katika Vijiji vyetu ambao wanaonyesha kwamba, wamepata vibali vya Serikali na wanataka kufanya biashara kule. Soko huria halijihusishi na *production*, soko huria huwa halishughuliki kabisa, liko katika *distribution level*, limo humu ndani linazungumzwa na wewe umelisema hapo. Unasema, tunapitisha hapa tunataka ku-*protect* Ushirika. Lakini wakati huo huo unataka kum-*protect* mlanguzi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishauri na ninaendelea kushauri, nilisema kwamba, ni lazima *operational areas* za soko huria ziainishwe. Soko huria liende kwenye mnada likutane na hawa wakulima wakati wametoka kwenye Ushirika wao. Hili jambo tumelizungumza hapa, Mheshimiwa Prof. Maghembe amelizungumza hapa, Wabunge wameimba hapa, sijui kuna tatizo gani? Mzee wangu, Mheshimiwa Sir George Kahama, ninakuheshimu sana, utueleze vizuri hivi tatizo hili mpaka uwapeleke kule Kijijini, kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu mashamba yaliyo katika Ushirika. Katika Jimbo langu kuna mashamba yanaitwa Leemi, Pongo na Kipupu. Mashamba haya yanamilikiwa na Washirika. Serikali imeruhusu kwamba, wanaweza wakaingia ubia na watu. Kwenye Shamba la Kipupu kulikuwa na Bwana mmoja anaitwa Baker, amekimbia na kwenye Shamba la Pongo kuna Bwana mmoja anaitwa Jicat.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusaidiane, hivi Chama cha Msingi kikisema kwamba, pesa itakayotokana na Ushirika ipelekwe kwa ajili ya ujenzi wa Shule au kwa ajili ya zahanani, huyu Mbia akielezwa anaweza akasema nini pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kwenye Jimbo langu la Siha, yapo mashamba ambayo yanaendeshwa na Vyama vya Msingi, ambayo yametamka *categorically* kwamba, wakulima watakaolima katika hayo mashamba watakuwa wanalipa kodi kwa kiasi cha Sh.10,000/=, lakini anakuja Mwekezaji pale anasema Sh.30,000/=! Nitaomba nipate matamko kwenye hayo mashamba.



**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nizungumzie kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake, kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni. Uzuri wa Muswada huu ni kwamba, naona na sisi tutapata nafasi ya kuusemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge akisimama hapa anasemea zao lililoko katika Jimbo lake, wengine wamesemea korosho, wengine wamesemea kahawa, wengine pamba na mimi niseme zao lililoko katika Jimbo langu na Majimbo mengine.

**WABUNGE FULANI:** Ng'ombe.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana niliuliza swali kuhusu Ushirika wa Wafugaji. Hatujawahi kuona Ushirika wa Wafugaji, japokuwa wafugaji wana mtaji mkubwa sana wa kuanzisha Ushirika, lakini wamesahaulika kabisa, sijui kwa nini? Siyo kwamba tunaomba mtupe mtaji, sisi tuna maji, tunachoomba ni elimu na kutuanzishia Ushirika wa Wafugaji. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania ifahamu kwamba, ng'ombe ni zao. Kila mtu hapa anavaa kiatu, kinatokana na ngozi, mpaka vifungo vilivyoko kwenye mashati yenu vinatokana na ng'ombe. Pia, maziwa, hata chakula cha kuku mnaokula kila siku kinatokana na damu ya ng'ombe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kusema kwamba, kwanza tunahitaji elimu na pia ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, mimi mwenyewe nimeanzisha Ushirika katika Jimbo langu. Kuna Vyama vya Ushirika vilivyopo na tuna Vyama karibu nane sasa. Kuna wengine wenye madume 150, wengine 60 na wengine 80, wananepesha na kuuza. Sasa tunataka elimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, aje katika Jimbo langu awape Wananchi elimu kwa sababu wanahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirika una faida sana, Mheshimiwa Waziri katika Mkoa wake kulikuwa na Ushirika uliokuwa unaitwa KNCU, walipofilisika Serikali iliwapa Shilingi milioni 500 ili waanzishe tena Ushirika. Hivi jamani Wafugaji hawataki wasaidiwe kama walivyosaidiwa watu wa Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirika unaleta umoja na unaleta msaada mkubwa sana, lakini Ushirika umeuawa kabisa kwa rushwa. Arusha tulikuwa na ACU na REVACO, lakini Vyama hivyo vyote vimekufa na kilichoua ni rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kusema kwamba, zamani katika Awamu ya Kwanza tulikuwa tunasema kila siku, Ushirika ni ukombozi. Lakini ule ukombozi wetu umekuja kufa kwa ajili ya rushwa na nikagundua kwamba, rushwa ndiyo imezaa

ubinafsishaji. Baada ya kumaliza Mashirika yote ndiyo ubinafsishaji ukaja katika Awamu ya Tatu na umeletwa na ...

**MBUNGE FULANI:** Rushwa. (*Kicheko*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Kwa hiyo, rushwa ndiyo imeua Ushirika na Ushirika ukazaa ubinafsishaji. Ndiyo maana katika Awamu ya Tatu tunasema sasa tunaimba ubinafsishaji.

**MBUNGE FULANI:** Mtoto wa rushwa.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Lakini tunachobinafsisha ni yale Mashirika yetu ya Umma yaliyomalizwa na rushwa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, bado kuna huyo adui rushwa, sijui huu Ushirika unaouanzisha tena kama utaepukana na huyo adui? Ninachokwambia ni kwamba, pambana na rushwa, kama huwezi kupambana nadhani hata huu Muswada tunaoupitisha hautatufaa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili angalau niendeleo katika hizi saa za mwisho nieleze yale niliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umeandaliwa vizuri sana, lakini nina mashaka kama utasaidia sana wakulima hawa maskini tunaowasema. Huu Ushirika uliokufa haukuwa Ushirika wa kumsaidia mkulima, ulikuwa ni Ushirika wa kusaidia mabepari. Ndugu yangu pale, Mheshimiwa Mwanri, ameeleza juu ya Ushirika wa kibepari na kijamaa. Ushirika wa kijamaa unaleta faida kwa wachache, wale maskini walio wengi, lakini Ushirika wa kibepari unaleta faida kwa wachache wale waliofanikiwa na kunufaika na ndiyo msingi wa Ushirika wetu uliopo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya ni lazima tuelewe kwamba, Ushirika tunaousema tunataka uwe Ushirika wa nani. Sasa tunazungumza juu ya *Apex Federation* na nini, hivi tuna shida gani hapa, tunazidi kunyang'anya nguvu ya mkulima huyu mdogo! Miaka yote tangu mwanzo tumeweka kuwa *union* ndizo zichukue shamba, kahawa au zao lolote. Wakishapewa *union*, mkulima hana mamlaka tena, inakuwa ni mali ya *union*. Wanauza kule na ndiyo wenye haki ya kuwagawia wakulima, lakini wakulima ndiyo wamekuwa wanapata viporo vya watu wasiofanya kazi, wamekula wamesaza. Hali hii imewakatisha wakulima tamaa na wameshindwa kubadili hata maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka Bodi ya Mazao kama kahawa. Hivi Bodi ya Mazao ya Kahawa inaleta faida gani kwa mkulima? Inakusanya mazao ya mkulima, inasimamia kule na ndiyo yenye mamlaka ya kutoa taratibu na sheria za mazao hayo

ambayo mkulima maskini hana habari nayo. Sasa hili kwa kweli litaua Ushirika hata huu tunaouunda. Pamoja na maandalizi mazuri ya utaratibu huu, hatutakwenda mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu baada ya kuona kwamba, *union* zinadhulumu wakulima, tumeanzisha vikundi. Wenye uzalishaji wa kahawa wenyewe ndiyo wameunda vikundi na tukawaambia watakaokuwa Viongozi katika vikundi hivyo ni wale wenye kahawa nyingi ya kutosha, ukiweka mwenye kahawa ndogo umeweka fisi wa kula mbuzi wako. Hakuna mwenye kahawa gunia moja kuja kulinda kahawa ya watu wenye magunia 100 au 200, haiwezekani! Atawaibia tu na hivyo Ushirika umekufa. Mnaweka mtu hajui hata uzalishaji wa kahawa wala matatizo ya kahawa, eti ndiye anakuwa Katibu au Meneja! Atakula tu, hana uchungu na hajui matatizo ya mazao yale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi vimejiuzia kahawa vyenyewe, wale wenye kahawa wamekusanya kahawa yao wakapeleka Moshi imeuzwa na wamelipana kwa kila kilo Sh.700/= na wengine Sh.800/=, lakini hivi ninavyoongea leo, zile *union* zote zimelipa wakulima Sh.300/=! Leo mtu anazungumza juu ya *union* kama si usaliti wa misingi ya uzalishaji ni nini?

Kama ni msingi, Vyama vya Ushirika viwe vya Msingi, wakulima wenyewe ndiyo waungane na mazao yao na wasivamie wazalishaji, wenyewe waone uwezekano wa kutunza yale mazao na kuona kwamba hayapotei wala hayadhulumwiwi na mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bei inayouzwa kule kwenye soko ndiyo wapewe wakulima. Gharama zikatwe, lakini siyo kwenda kulipia watu mishahara. Yaani mkulima alipie watu wa Bodi ya Kahawa mishahara! Bodi ya Kahawa inakusanya fedha nyingi sana, lakini *returns* zao kwa wakulima hazipo. Hili linaua hata nia ya kuzalisha kahawa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi wakulima walizalisha kahawa wakaenda kuuza, wale waliokuwa na kahawa nzuri na bora ikapata bei nzuri, waliuza kwenye Sh.1,800/= kwa kilo. Lakini *union* zimechukua zile fedha zilizouzwa kwa kahawa hiyo zikawagawia wote eti kusawazisha bei. Hivi kama si kudhalilisha wakulima hawa maana yake ni nini? Nasema kwa kweli kama tunazungumza Ushirika tuwe wakweli na tusije tukaanza kupinda pinda. Sasa hivi kule hakuna mwenye imani ya Ushirika, watu wako kule wakishaingia kwenye Ushirika lengo lao ni kudhulumu tu!

Mheshimiwa Waziri, hata watendaji wako wa Wizara ndiyo wamekuwa kwenye mikutano ya kusawazisha bei ya wenye kahawa nzuri na mbaya wote wapate sawasawa. Afisa Ushirika wako wa Mkoa alikuwemo. Nimezungumza na Mkuu wa Mkoa pale, anasema, si wao wameeleza. Sasa, wao wameeleza, yeye anafanya kazi gani? Wanaoua Ushirika ni Watendaji hawa ambao hawana hamu wala hawana uwezo wa kuendeleza Ushirika na hata huu tukiweka hautakwenda popote, itabaki ni hadithi tu ya kwenye haya makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tunachosema ni kwamba, Chama cha Msingi kisibanwe kwa kuuza mazao. Wao wavutiwe na bei, kwamba ni wapi watauza mazao yao kwenye bei nzuri. Huwezi ukasema Ushirika wa Kutengeneza Meza ni lazima uuze kwenye *union* yao au kwenye *Apex*, waache watafute bei. Pia, kwa huu Ushirika wa utawala wa ufundi, basi na *TBS* iingie kuwezesha ufundi wao ukubalike. Lakini sasa kama tutaacha hali hii, uzalishaji wa mazao hautabadilika wala hautaendelea hata kidogo, hili tulifahamu, hautakwenda mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mali ya Ushirika inahesabika kama ni mali isiyo na mwenyewe, ni sawa na mali ya Serikali. Wengi wanafikiri mali ya Serikali haina mwenyewe. Hata dreva akishika gari la Serikali ataliendesha anavyotaka, maana halina mwenyewe. Hata likianguka, liki-*burst* si lake. Ndiyo maana hatuwezi kwenda na utekelezaji unakuwa mgumu kwa sababu ya watu wenye fikra hizo na ndiyo wengi, ndiyo maana tunakwama. Mfano, ukileta mradi watu watasema ni wa Serikali, ni wa umma, hauna mwenyewe. Kila anayeweza anadonoa pale. Kama linajengwa daraja, anayewahi *cement* sawa, anayewahi nini sawa, basi haliishi linabaki gofu au linatengenezwa kwa matengenezo ya kiwango cha chini linabomoka, eti ni mali ya umma na Ushirika ndivyo unavyokwenda hivyo. Sasa, hatuwezi kwenda mahali tukafanikisha hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia haya mambo ya kumlinda mtu achaguliwe mara mbili, yaani akae nje, halafu aje arudi, hivi kweli tunautakia mema Ushirika? Kama mtu amefanya vizuri wampime mara ya kwanza akiweza kupita aendele, lakini mara ya tatu aachie wengine. Hii ya kumpa mtu mpaka tena akae huko nje, ajifunze mbinu za kuja kudhulumu na aingine tena, aah! Kwa kweli kwa hilo tutakuwa tunaunda sheria ambayo ni kisu cha kujichoma sisi wenyewe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa mazao, ninafika mahali naanza kuwa na wasiwasi. Leo Bodi zinazosimamia mazao ziko Wizara ya Kilimo na Chakula, haziko Wizara ya Ushirika na Masoko. Lakini mtu anayetaka Ushirika wa kufaidika na kuleta maendeleo ni Wizara ya Ushirika na Masoko, sasa hapo sijui kama watu hatutakuja kugongana humu ndani. Wa Ushirika atasema watu wauze, atafute masoko, wa Kilimo ndiye anayeleta mbolea na nini, hivi kweli tutakwenda? Kama tunataka Wizara ya Ushirika na Masoko iwe na nguvu, basi ichukue na jukumu la kutafuta pembejeo za kuwezesha mazao yastawi vizuri ili yatoshelze. Si suala la kusimamia vitu vilivyozalishwa tu huku hujui vinavyozalishwa, hujui vinapatikanaje, unasimamiaje? Utakuja kuwa *redundant* katika usimamizi wetu. Haifai kuchukua vitu nusu nusu halafu tukaanza kuhangaika navyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ni lazima tujue kwanza hivi viwanda vidogo vidogo vinapata wapi *material* ya biashara ya vitu wanavyotengeneza. Kwa hiyo, Ushirika labda iwe ni kiungo katika Wizara ya Viwanda na Biashara, pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula. Kuwe na Wizara tatu zimeungana, zimepeana majukumu, tamko lao liwe moja, vinginevyo hatutakuwa na tamko lolote lenye maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kama tunataka Vyama hivi vya Msingi viendeleo kweli, basi moja iwe ni kuwawezesha wawe na Benki yao, hakuna sababu ya kusema Chama cha Ushirika hakina uwezo. Uwezo wanao kwa sababu wanazalisha, ni kwa nini wasilazimike kutoa? Tatizo linalofanya vitu hivi visifanikiwe ni kwamba, kulikuwa na amana hapo nyuma, zilikatwa fedha za wakulima kwa lengo la kuja kuwasaidia kuwapa pambejeo na kadhalika, fedha hizo zimepotea. Pale Ushirika ulipofutwa, fedha zao zilipotea. Leo ukiwaambia wanakumbuka kule kwenye tatizo la nyuma na hii ni kawaida kwa kila mtu. Huwezi ukamwambia mtu ashiriki Ushirika wakati yeye alipoteza au baba yake naye alipoteza hela zake zote za amana, leo umwambie kwamba endelea. Kwa kweli kuvumilia kuna kiwango ni lazima tujue, huwezi kuendelea kuvumilia tu vinginevyo utakuwa ndiyo mjinga wa kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mrajisi bila kuwa na misingi ya ukaguzi wa Vyama hivi, kufuatiliwa na kuwa na usafiri wa kuona yanayofanyika katika Ushirika ni ya kweli na yanakwenda sawa sawa hatutakwenda mahali. Tuna hivi viwanda, mimi ninacho kimoja kule Mbozi na Waziri nimekwishamwambia. Kuna watu wamejiunga na Chama, lakini tangu kimeanzishwa hakuna hata gawio!

Wapo watu wametuna pale wanatumia tu na Serikali ina *share* zake 34 kwa 100. Sasa, zile *share* wala hawashtuki kuwa wana haki ya kupata gawio pale, hakuna anayeshughulika. Halafu unafikiri huyu mkulima ndiyo atapata kitu pale! Wapo watu wanaishi kwa damu ya watu wengine na wanaona ni sawa na Mungu aliwaumba hivyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda namna hii, ni lazima tufike mahali tukubaliane, kama ni Ushirika iwe ni kwa Kijiji au Chama cha Msingi na wao ndiyo watajali hata mazao yao, watayalinda, watayasimamia na yatawaletea maendeleo.

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halinga, kengele ya mwisho hiyo.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono kwa maandishi tu, lakini kwa mafanikio sina uhakika. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache kabla ya kuahirisha Shughuli za Bunge. Moja ni kwamba, wachangiaji tulionao wamebaki kama watano, ambao wataendelea kuchangia siku ya Jumatatu tarehe 10. Kwa uzoefu ninaouona, hawa wataamaliza katika kile kipindi cha asubuhi. Kwa hiyo, baadaye tutakuwa na *Merchant Shipping Bill*. Kwa wale ambao hawana Miswada, ili kujiandaa vizuri kwenye hizi siku za *weekend*, Katibu anasema nakala zake ziko hapa, tunaweza tukachukua tukasoma kwa ajili ya kuchangia Muswada huo utakaokuwepo Jumatatu.

Matangazo mengine ni yale ambayo Mheshimiwa Spika alitangaza ya semina na matembezi. Kuhusu hayo matembezi Mheshimiwa Joel Bendera ndiyo anafahamu na hizo semina mbili ni ya kesho na ya kesho kutwa na zote zitaanza saa tano asubuhi.

Basi baada ya hapo, naona shughuli zilizopangwa leo zimeisha. Kwa hiyo, ninaahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.59 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu  
Tarehe 10 Novemba, 2003 Saa 3.00 asubuhi)*